# Nipashe

Ijumaa Februari 28, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580166

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Makinda afichua mbinu kufikia usawa kijinsia uchaguzi 2020

UKURASA 3




UKURASA 13

# Saudi Arabia yawazuia waumini kuingia hija

UKURASA 2




Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam jana, akiwataka viongozi wa dini nchini kufanya maombi kufuatia kuzuka kwa ugonjwa hatari wa corona. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## DC APIGA MARUFUKU NGOMA ZA VIGODORO

UKURASA 10




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Rugemalira akubaliwa kuwasilisha hoja kuondolewa kesi ya uhujumu

UKURASA 2


MICHEZO NIYONZIMA ARUDISHA UFALME WAKE YANGA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Saud Arabia yazuia waumini kuingia hija

**Romana Mallya na mitandao**

SERIKALI ya Saud Arabia imezuia wageni wote wanaoingia nchini humo kwa safari za kidini, wakiwamo wanaotembelea miji mitakatifu katika dini ya Kiislamu, Makka na Madina kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Corona.

Wakati Saud Arabia ikitangaza zuio hilo, Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakary Zubeiry bin Ally, amewaomba masheikh, maimam, maustadhi, waislamu na Watanzania kwa ujumla, kuomba dua na kufanya toba ili maradhi makubwa na madogo yawaepuke, hasa ugonjwa wa Corona.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudia ilitangaza jana marufuku hiyo ya muda, lakini haikutaja ni lini hasa marufuku hiyo itaondolewa.

Mamilioni ya watu huingia Saudia katika kipindi cha mwaka mzima kufanya ibada ya Umra na wengi zaidi huingia kwa pamoja kufanya ibada ya Hija.

Tofauti na Hija, Umra hufanyika katika kipindi chochote cha mwaka, na kwa sasa marufuku hiyo inawalenga mahujaji raia wa nchi za nje wanaoenda kuitekeleza.

Hata hivyo, bado haijulikani kama ibada ya Hija, ambayo inategemewa kuanza mwishoni mwa Julai kama itaathiriwa na zuio hilo lililochagizwa na kusambaa kwa virusi vya Corona duniani.

Saudia pia imewapiga marufuku watu kutoka nchi zilizokumbwa na virusi hivyo kuingia nchini humo. Mpaka sasa, Saudia bado haina mtu ambaye amethibitika kuambukizwa virusi hivyo.

Makka, ndiyo mji ambao Mtume Muhammad alizaliwa, na kuna msikiti mtakatifu zaidi. Madina ndipo alipofariki na kuzikwa.

Watalii ambao si wa kidini wanaotoka katika nchi ambazo virusi vya Corona vimethibitisha kuingia, pia watakataliwa kuingia Saudia.

Saudi Arabia imeeleza kuwa tangu Oktoba, imetoa viza zaidi ya 400,000 za watalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

Matukio zaidi ya virusi ambavyo husababisha ugonjwa kupumua Covid-19, yanaendela kujitokeza, huku milipuko ya ugonjwa huo ikibainika China ambako ulianzia.

Mpaka sasa, zaidi ya watu 2,700 wameshafariki dunia kutokana na ugonjwa wa Covid-19.

Toka virusi vya Corona viripotiwe Desemba, zaidi ya watu 80,000 kutoka mataifa takribani 40 tayari wameshaambukizwa virusi hivyo. Wengi wao wakiwa China.

Iran, ambayo imetenganishwa na Saudia kwa mkondo mwembamba wa bahari, mpaka sasa imesharipoti vifo 19, ambayo ni namba kubwa zaidi ya watu kwa mataifa ya nje ya China.

Hata hivyo, vifo hivyo vinatokana na wagonjwa 139, hali ambayo inawafanya madaktari wa magonjwa ya kuambukiza kuhofia kuwa nchi hiyo inaweza kuwa na wagonjwa wengi zaidi inaowaficha.

**MUFTI ZUBEIRY ANENA**

Mufti Zubeiry alisema jijini Dar es Salaam, jana, kuwa ugonjwa wa Corona umeenea katika nchi mbalimbali duniani na kwamba baa linapotokea, halimlengi mtu mbaya peke yake.

"Balaa linapotokea halimlengi mtu mbaya peke yake, linamwendea hata aliyekuwa mwema. Balaa linaposhuka, linamwendea mtu mbaya na mwema ambaye yupo pamoja kimaisha na yule mtu mbaya," alisema.

Mufti alitaka watu warejee kwa Mungu kwa kutubu, kufanya ibada na kujinyenyekeza kwake ili aondoe tatizo hilo.

"Ibada kubwa tunayotakiwa kufanya kipindi hiki ni kumwomba Mungu kwa dua mbalimbali katika maeneo mbalimbali ikiwamo misikitini," alisema.

Alisema ni wajibu viongozi wa dini kuwaomba maimamu, mashehe, walimu na waslamu wote kuliomba balaa hilo liondoshwe duniani.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akihakiki taarifa zake za mpigakura kwenye Daftari la Kudumu Wapigakura katika Kituo cha Shule ya Sekondari SOS, Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina. **PICHA: OMR**

# Rugemalira akubaliwa kuwasilisha hoja ya kuondolewa kesi ya uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imekubali mfanyabiashara James Rugemalira kuwasilisha hoja za awali, kuomba kuondolewa katika kesi ya uhujumu uchumi baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kushindwa kumwondoa jana katika kesi hiyo ilipopangwa kutajwa.

Mapema Februari 13, mwaka huu Rugemalira, alidai kuwa amewasilisha nyaraka katika taasisi tisa za Serikali ikiwamo Benki Kuu Tanzania (BoT), Usalama wa Taifa (TISS) na DPP kwamba kama hataondolewa kwenye kesi hiyo atawasilisha maombi hayo.

Madai hayo aliyatoa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi. Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi bado haujakamilika na aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili wa utetezi, John Chuma, alidai kuwa mteja wake Rugemalira aliwasilisha maombi ambayo mpaka sasa hawajapata majibu yoyote.

Wankyo alikiri kupokea nyaraka mbili kutoka upande wa utetezi moja ikiwa inamhusu Rugemalira, lakini alitaka kujua kama nyaraka hizo zipo kwenye kumbukumbu ya mahakama.

Hakimu Shaidi alisema mahakama yake imeziona nyaraka hizo na zipo kwenye kumbukumbu yake.

Wankyo alidai kuwa upande wa Jamhuri uko tayari kutoa majibu kwa njia ya mdomo wakati wowote baada ya upande wa utetezi kuwasilisha hoja zao ikiwa mahakama itaruhusu.

Hata hivyo, Wankyo alidai kuna jambo hilo limekuwa likijitokeza kwa mshtakiwa Rugemarila kuweka utaratibu wa kujitetea na kujieleza mwenyewe mahakamani, hivyo aliomba kujua kama anao uwakilishi au anajiwakilisha mwenyewe.

Akijibu hoja hiyo Rugemalira alidai kuwa hajui Simon ana matatizo gani na jambo hilo kwa kuwa sheria inamruhusu na kuiomba mahakama isizingatie hoja hiyo.

Awali Rugemarila alidai mahakamani kuwa aliandika barua kwa Kamishna wa TRA kupitia mjumbe wa Takukuru aliyetembelea gerezani akielezea jinsi Benki ya Standard Chartered Hong Kong, inavyokwepa kodi huku akieleza kuwa wanaostahili kujumuishwa kwenye kesi ni benki hiyo na si yeye.

Vile vile, alidai pia aliandika notisi taasisi tisa ikiwamo Usalama wa Taifa (TISS), akitaka DPP awasilishe hati ya kuachiwa na asipofanya hivyo atawasilisha hoja ya kuiomba mahakama imwondoe katika kesi hiyo. Hakimu Shahid aliuagiza upande wa utetezi kuwasilisha hoja zao kwa maandishi Machi 2, 2020 na upande wa mashtaka ulisema utatoa majibu kabla ya Machi 12, 2020.

Kadhalika Hakimu Shahid alisema kuwa endapo upande wa utetezi utakuwa na hoja za nyongeza baada ya kupata majibu watapaswa kuyawasilisha Machi 14, 2020. Kesi itatajwa Machi 12, mwaka huu.

Wengine kwenye kesi hiyo ni Harbinder Sethi na Joseph Makandege.

Katika kesi ya msingi, uhujumu uchumi namba 27/2017, Makandege anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000, pia ya yapo madai ya utakatishaji wa fedha.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka hayo Desemba 20, 2019, baada ya kuunganishwa na washtakiwa Seth na Rugemalira katika kesi ya uhujumu uchumi.

Makandege anadaiwa kuwa, kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Kenya, Afrika Kusini na India, akiwa na wenzake, walikula njama ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Pia anadaiwa kuongoza genge la uhalifu, katika nchi hizo, akiwa si mtumishi wa serikali akishirikiana na watumishi wa umma kwa kuratibu na kufadhili mpango wa uhalifu.

Katika shtaka la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Makandege anadaiwa kuwa kati ya Januari 23, 2014 na Februari 2014, alijipatia Dola 380,000 katika Benki ya Stanbic iliyopo Kinondoni na Dola 600,000 katika Benki ya UBL Bank (T) Ltd., iliyopo Wilaya ya Ilala, fedha zilizotoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa nyakati tofauti.

Sethi na Rugemalira, walifikishwa mahakamani hapo zaidi ya miaka miwili.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh 309,461,300,158.27. Kwa mara ya kwanza walifikishwa mahakamani Juni 19, 2017.

## Kitambulisho cha NIDA champeleka Mrundi jela

**Na Tiganya Vincent,** URAMBO

PASCHAL Damian (37), mkimbizi kutoka Burundi amehukumiwa kwenda jela miaka minne, baada ya kutiwa hatiani kwa makosa ya kuingia nchini kinyemela na kukutwa na kitambulisho cha Taifa, cheti cha kuzaliwa na kadi ya mpigakura ya Tanzania.

Pamoja na kupewa adhabu hiyo, Mahakama ya Hakimu Mfawidhi ya Wilaya ya Urambo imeagiza kwamba mtuhumiwa huyo akimaliza kutumikia adhabu hiyo arudishwe nchini kwao.

Adhabu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Urambo, Hassan Momba, baada ya raia huyo wa Burundi kukiri makosa yake mawili yaliyokuwa yanamkabili.

Awali, upande wa mashtaka ukiongozwa Mkaguzi wa Udara ya Uhamiaji, Chambuko Funga, ulidai kuwa Januari 24, 2020 mshtakiwa alikutwa katika Kijiji cha Kaliua Mashariki wilayani Kaliua Mkoa wa Tabora bila kuwa na kubali kinachomtambulisha kuwa na uhalali wa kuingia nchini.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa raia huyo wa Burundi ni Septemba 12, 2017 alitoa taarifa za uongo kwa Ofisa Uhamiaji, Zuberi Kumbukwa, kwamba ni raia wa Tanzania, huku akijua kwamba ni kuiongopea mamlaka.

Aliongeza kuwa siku hiyo mshtakiwa baada ya kutoa taarifa za uongo, alifanikiwa kupata kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho (Nida) No 19830414-4574-00002-20.

Aidha, alikutwa na cheti cha kuzaliwa No 02348757 kilichotolewa Septemba 19, 2017 ambacho kilimwezesha kupata kwa urahisi kitambulisho cha Taifa na kadi inayomruhusu kuwa mpigakura halali wa Tanzania.

Hakimu Momba katika hukumu yake, alisema anatoa adhabu hiyo ili liwe funzo kwake na wengine wenye tabia za aina hiyo kwani makosa aliyotenda mshtakiwa yanahatarisha usalama wa nchi.



Meneja wa Uwekezaji wa mradi wa kampuni ya Yapı Merkezi, Yetkin Gen Mehmen, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kusomewa shtaka la kusafirisha nje fedha kiasi cha dola 84,850 kinyume cha sheria. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Neno la Makinda uchaguzi 2020

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA mstaafu, Anne Makinda, amewataka wanawake kuacha woga na kujitokeza kushiriki katika uchaguzi mkuu mwaka huu bila kujali kudhalilishwa, ili kuleta usawa wa kijinsia kwenye nafasi za uongozi.

Makinda alitoa kauli hiyo jana katika maadhimisho ya kongamano la kitaifa kuhusu Siku ya Wanawake itakayoadhimishwa Machi 8 mwaka huu.

Alisema wanawake wasijali lugha chafu zitakazokuwapo dhidi ya kundi hilo wakati wa mchakato wa uchaguzi kwa kuwa shida yao ni kuwa wabunge na madiwani ili kuwatumikia wananchi. Alisema hakuna mwanamke makini atakayeshindwa kwenye uchaguzi huku, akimtolea mfano Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jenista Mhagama, ambaye ni Mbunge wa Peramiho.

"Kuna wanawake wengi wabunge wa majimbo wamefanya kazi nzuri, hata mimi nilifanya kazi nzuri nilipofika miaka 40, nikaona niache nisiwe kikwazo," alisema. Aliwataka wanawake kutokubali kuipoteza fursa ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, akiamini kuwa wasipofanya hivyo, Tanzania itaendelea kuota ndoto kwenye suala la usawa wa kijinsia na wanawake kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi.

"Kipindi cha kina Kawawa, wanawake walikuwa wanapigana vita kwa upendo kabisa, sasa hivi kuna ubinafsi mwingi na mkifanya ubinafsi hatuwezi. Hata asasi za kiraia utakuta kila asasi ina agenda tofauti na mwenzake, sasa vita inapiganajwe?" Alihoji.

Alibainisha kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali, bado kuna tatizo la mtazamo hasi kwa baadhi ya jamii kuhusu usawa wa jinsia na kuendelea kuwapo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, mila na desturi zenye kuleta madhara ya upungufu wa rasilimali za kutekeleza mipango kuelekea 2025. Makinda alisema suala la haki ya wanawake kushiriki kwenye siasa kama wapigakura au wagombea wa nafasi mbalimbali linaonekana kuwa na jitihada ingawa zinafanyika kwa kusuasua.

Alisema hadi sasa kwa ngazi ya ubunge, tangu mfumo wa chama kimoja licha ya kuwapo kwa utaratibu wa viti maalum, Bunge lingekuwa na wastani wa wabunge wanawake asilimia kati ya sita na saba tu.

"Mimi nasema miaka 25 ya Beijing hatujafanya vizuri, wanawake ondoeni woga, acheni kukimbia kivuli chenu, wanawake hata kabla ya kwenda, unaanza kuwaza utakavyoshindwa hata bado kujaza fomu unawaza kushindwa, ni mapambano matusi utakuwa nayo, dharau, kutukanwa, 'malaya' utaambiwa, lakini wewe shida yako ni nini, si kuwa mbunge tu, kuwa diwani, acheni woga. "Nafahamu kuna wakati mwingine vyama vyetu vya siasa ni kipingamizi, wakati mwingine sisi wenyewe ni kipingamizi hasa wanapotokea wanawake wawili wapo jimbo moja, kutakuwa ni ugomvi tu, wanaume wanasema waache waendelee kugombana, wote wanakosa nafasi tumepoteza wenyewe," alisema.

Aliwataka wanawake kote nchini kujiandaa kwa ajili ya uchaguzi mkuu ili kufikia usawa huo.

"Tumegawanyika hivi kweli, tutakuwa tunashindwa wakati wote ambao wanatamani kugombea majimbo ya uchaguzi, shime twende kwa nguvu moja," alishauri. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliwataka wanawake na wanaume kuwa mabalozi wa kubadili mitazamo waliyonayo na washirikiane kwa lengo la kuleta usawa wa kijinsia.

"Tusikatishwe tamaa na maneno ya kuturudisha nyuma maana mwanamke ukiwa kiongozi, utaambiwa umelala na wanaume wote, pambana hayo maneno yapo kwa kuwa hawataki kuona wanawake wameshika nafasi za uongozi," alisema.

Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika, Dk. Getrude Mongela, alisema mwaka huu ni wa uchaguzi, hivyo wanawake wapambane kuingia mjengoni na kuwataka kwenye uchaguzi huu kuchagua wanaume wanaoelekea kuelewa ajenda ya 50 kwa 50. Mbunge wa zamani, Anna Abdallah, alisema kinamama watakaojitokeza, wasaidiwe na wanawake walioko kwenye nyanja mbalimbali za uongozi kama wao hawataki kugombea tena.

Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta, aliwataka kinababa kuwaunga mkono wake zao ili wawe wengi bungeni.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**Invitation to bid: No. ITB/2020/SUP/002**

**ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENT(S) FOR THE SUPPLY OF DIESEL FUEL – BULK DELIVERY**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Tanzania, invites qualified suppliers to make a firm offer for the establishment of Frame Agreement(s) for the supply of Fuel (Diesel) Delivered in Bulk to the destinations mentioned below.

UNHCR may award Frame Agreement(s) with initial duration of 2 (two) years, potentially extendable for a further period of 1 (one) year, for supplying its operation in Tanzania. The successful bidders will be requested to maintain their quoted price model for the duration of the Frame Agreement(s).

**2. Eligibility:**

Fuel Companies, authorized resellers, wholesalers, or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be downloaded from link here
**https://drive.google.com/drive/folders/1TsJo5j3LqD-ZeHWG5dT80gr-80nFka6l**

**CRUCIAL DATES FOR THIS INVITATION TO BID**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Tuesday 17th March 2020 at 23.59 hours EAT |
| Suppliers' conference meeting | Wednesday 18th March 2020 at 11.00hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Tuesday 14th April 2020 at 16.00 hours EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to access the tenders.*

215649302

# Serikali yakunwa utendaji Polisi

Na Romana Mallya

SERIKALI imeridhishwa na kasi ya utendaji wa Jeshi la Polisi, ikibainisha kuwa katika kipindi cha miezi 14 iliyopita, matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo mkoani Simiyu katika mkutano wa mashauriano ulioandaliwa na serikali na kuwashirikisha wafanyabiashara na wawekezaji.

Masauni alisema takwimu za kuanzia Januari mwaka jana hadi Februari mwaka huu, zinaonyesha matukio ya aina hiyo yaliyojitokeza na kuripotiwa ni manane tu.

"Matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha yaliripotiwa katika mikoa ya Songwe, Tabora, Njombe, Mjini Magharibi, Temeke na Kinondoni. Watuhumiwa 22 walikamatwa," alisema.

Masauni alisema mafanikio hayo yamechagizwa na mafunzo mbalimbali waliyopewa askari wa jeshi hilo kupambana na aina tofauti za uhalifu.

"Ninalipongeza Jeshi la Polisi kwa kugundua na kudhibiti mianya ya uhalifu. Niwaombe wawekezaji pamoja na wafanyabiashara nchi nzima, endeleeni na shughuli zenu bila ya wasiwasi," alisema.

Masauni alisema kipindi cha nyuma kulikuwa na matukio ya wafanyabiashara na wawekezaji kuvamiwa na majambazi na kuporwa kiasi kikubwa cha fedha wakati wakienda benki au nyumbani.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kupitia intelijensia, wamedhibiti matukio hayo.




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florence Lwoga (kulia), akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa kanzidata ya kudumu ya watoa huduma za fedha. Katikati ni Naibu Gavana, Dk. Benard Kibesse na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya DCB, Godfrey Ndalahwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara 1,950 wapewa elimu ya kodi

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewafikia wafanyabiashara 1,950 wa Mkoa wa Iringa wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi iliyofanyika kuanzia Februari 17 hadi 27, mwaka huu.

Kampeni hiyo ni kwa ajili ya kuwaelimisha baadhi ya wafanyabiashara wa Wilaya za Kilolo, Manispaa ya Iringa na Mufindi.

Akizungumza baada ya kuhitimisha kampeni hiyo mkoani humo, Ofisa Msimamizi wa Kodi Mwandamizi wa TRA, Catherine Mwakilagala, alisema kampeni hiyo imeleta mafanikio makubwa kwa kuwafikia na kuelimisha idadi hiyo ya wafanyabiashara.

"Mamlaka ya Mapato Tanzania tumehitimisha kampeni ya elimu kwa mlipakodi katika mkoa huu wa Iringa na kampeni hii imefanikiwa sana kwa sababu tumewafikia walipakodi 1,950 ambao wote tumewapatia elimu ya kodi na wamepata nafasi ya kutoa maoni na changamoto zao ambazo tumezipokea na nyingine tumezipatia ufumbuzi," alisema Mwakilagala.

Meneja wa TRA mkoani humo, Lamson Tulyanje, alitoa wito kwa wafanyabiashara wote waliotembelewa na maofisa wa TRA kwenye maduka yao na waliopata elimu kupitia semina wakati wa kampeni hiyo, kutumia elimu waliyoipata kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na hiari.

"Elimu ambayo wameipata wafanyabiashara mbalimbali kwenye kampeni hii ya elimu kwa mlipakodi, ni vizuri waitumie katika kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati ili serikali iweze kutimiza majukumu yake ya kuwapatia huduma mbalimbali wananchi," alisema Tulyanje. Richard Kilawa, mfanyabiashara wa duka la vifaa vya ujenzi kutoka Halmashauri ya Mji wa Mafinga mkoani humo aliishukuru TRA kwa kumfikishia elimu ya kodi dukani kwake na aliahidi kuendelea kulipa kodi kwa hiari.

"Ninashukuru sana TRA kunitembelea dukani kwangu na elimu yao imenifundisha kulipa kodi kwa hiari. Hivyo, nitawashawishi wafanyabiashara wenzangu walipe kodi kwa hiari ili tujenge nchi yetu," alisema Kilawa. Naye mfanyabiashara wa mbao wa halmashauri hiyo, Maura Ng'umbi, alisema kupitia elimu iliyotolewa na maofisa wa TRA wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi, imemsaidia kujua umuhimu wa kulipa kodi stahiki kwa manufaa ya taifa.

## Wakulima 300,000 pamba wakumbukwa

Na Mwandishi Wetu, SIMIYU

WAKULIMA zaidi ya 300,000 wa pamba nchini wakiwamo wa Mkoa wa Simiyu wameahidiwa fursa ya kufunguliwa akaunti za benki kwa ajili ya matumizi ya msimu huu wa zao hilo.

Ahadi hiyo imetolewa na Benki ya NMB, na kwamba imeanza mchakato wa kuwafuata wakulima wote waliopo maeneo ya vijijini na kuwafungulia akaunti bila gharama yoyote kwa ajili ya kuhakikisha katika msimu wa mwaka huu hawapati usumbufu wa kupokea malipo yao.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa Benki hiyo, Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, wakati akizungumza kwenye mkutano wa majadiliano ya kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wa mkoa huo uliongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki.

Alisema kuwa mpango ambao wamejiwekea watahakikisha wanawafikia wakulima wote kwa haraka kabla ya msimu mpya wa kuanza kuuza pamba haujafika Juni, 2020.

Aliongeza kuwa kutokana na serikali kusisitiza msimu wa mwaka huu wakulima watalazimika kufungua akaunti benki na malipo yao yatafanyika kwa njia ya benki, NMB imejipanga kuhakikisha inafanikisha jambo hilo.

Aidha, Magesse alisema kuwa benki yake imejizatiti katika kuboresha sekta ya kilimo nchini, kwani imekuwa ikiwawezesha mikopo mbalimbali wakulima wa mazao ya kimakakati zaidi ya milioni moja.

"Tumeendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha kilimo hapa nchini, kama benki kubwa nchini tumewasaidia wakulima katika mazao ya kimkakati kama pamba, korosho, kahawa, tumbaku na mazao mengine ya chakula kama mahindi," alisema meneja huyo.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuitumia benki hiyo katika huduma mbalimbali za kifedha kwani ni benki yao kutokana na serikali kumiliki hisa asilimia 30, huku akiwahakikishia mikopo yenye riba nafuu.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, aliitaka NMB kuhakikisha inakamilisha zoezi la kuwafungulia akaunti wakulima kwa haraka na wakati kwani msimu mpya wa ununuzi wa pamba umewadia.

Mtaka alisema kuwa serikali imetoa maagizo kuwa wakulima wote wanatakiwa kufungua akaunti kwani malipo yao yatalipwa kwa njia ya benki, hivyo aliitaka benki hiyo kuhakikisha inawafuata wakulima walipo na kuwafungulia.

# Changamoto za uwekezaji kutatuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, amesema serikali itafanyia kazi changamoto na mapendekezo yote yaliyotolewa na wawekezaji mkoani Shinyanga.

Pia ameahidi uboreshaji wa mazingira ya biashara na kuwekeza nchini.

"Serikali itaendelea kuyaboresha mazingira ya biashara ikiwamo kupunguza kodi, tozo na ada mbalimbali ili kurahisisha na kuvutia uwekezeji na biashara nchini," alisema Kairuki na kuongezea kuwa sheria mpya ya uwezeshaji itasaidia kulinda na kuchochea ukuaji wa uwekezaji na biashara.

Akizungumza mjini Shinyanga katika mkutano wa wazi wa majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara wa mkoa huo, aliwaondoa wasiwasi kuwa serikali imeazimia kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025 sambamba na kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa uwekezaji na biashara kukua.

Kairuki alisema mikutano ya majadiliano moja ya mambo mengi inalenga kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji na wafanyabiashara ili kufanikisha azma ya serikali ya kujenga uchumi imara pamoja na kuvutia mitaji mikubwa katika biashara na uwekezaji.

Aliwapongeza washiriki wa mkutano huo ambao waliibua hoja muhimu zilizopatiwa majawabu na manaibu mawaziri katika sekta husika, hivyo mapendekezo yote yaliyotolewa yatawasilishwa serikalini kupata ufumbuzi wa kudumu.

"Niziombe mamlaka za serikali ziwe na utaratibu wa kufanya ukaguzi kwa pamoja katika viwanda na maeneo ya biashara na uwekezaji ili kumwezesha afanye kazi zake kwa nafasi tofauti na hali ilivyo sasa kwani kila mamlaka huenda kwa wakati wake," alisema Waziri Kairuki.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa kero zote zitafanyiwa kazi na kuzitaka taasisi za kifedha kujitafakari katika utoaji wa mikopo yenye riba kubwa wakati serikali ilishafanya maboresho katika riba.

"Serikali inawatoza wenye benki asilimia 7 ya riba ya mkopo kutoka benki, hivyo wanakila sababu ya kujitafakari juu ya riba wanazotoza kwa sasa ya zaidi ya asilimia 18 jambo ambalo siyo sahihi," alisema Dk. Kijaji.

Alisema zaidi ya kodi na tozo 164 zimefutwa na serikali ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alisema mkoa wake umefanya jitihada kubwa ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ambapo hadi sasa kuna jumla ya viwanda 729 kati ya hivyo, 13 ni viwanda vikubwa, 11 viwanda vya kati na 705 ni viwanda vidogo ambavyo vimeajiri Watanzania 10,150.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa fursa ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi na ufugaji ni kubwa katika Mkoa wa Shinyanga na kuwaomba kuwekeza zaidi katika sekta hiyo.

## Utitiri wa kodi wawakera wafanyabiashara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UTITIRI wa kodi kwa wafanyabiashara na wawekezaji mkoani Shinyanga umedaiwa kuwa kero na kusababisha mapato kidogo na baadhi wakidai kuzifunga biashara zao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda, na Kilimo (TCCIA), mkoani Shinyanga, Meshack Kulwa, alisema hayo wakati akisoma taarifa kwenye mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji mkoani humo.

Alisema kero kubwa wanayokabiliana nayo wafanyabiashara na wawekezaji mkoani humo ni utitiri wa kodi ambao unasababisha baadhi yao kushindwa kuzimudu kulipa, huku wengine wakifunga na kufungiwa baadhi ya biashara zao kwa sababu ya kushindwa kulipa kodi hizo.

"Kero kubwa dhidi ya wafanyabiashara na wawekezaji ni kuwapo kwa utitiri wa kodi, hivyo tunachokiomba kwa serikali ituondolee zile kodi ambazo ni kero, ili nasisi tuendelee kufanya biashara tukue kiuchumi na kulipa kodi," alisema Kulwa. "Pia tunaomba pale kunapotokea mgogoro wa ulipaji kodi kati ya mfanyabiashara na serikali, itafutwe suluhu na hata kupitia kwenye chama chetu cha TCCIA, na siyo kwenda tu kufunga biashara au kiwanda, na kisha kutuchafua kwenye vyombo vya habari," aliongeza.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema, serikali itaendelea kuzifuta kodi, tozo na ushuru ambazo ni kero kwa wafanyabiashara, ili zibaki zinazoweza kulipika, ikiwa hakuna ukusanyaji wa mapato serikalini bila kuwapo na wafanyabiashara wala wawekezaji. Alisema kwa kipindi cha miaka minne ya utawala wa Rais John Magufuli, wamefuta kodi, tozo na ushuru 168 ambazo zilikuwa kero kwa wafanyabiashara, lakini cha ajabu mapato yamezidi kuongezeka, tofauti na hapo awali kwa sababu walipakodi walikuwa wachache kwa kukwepa kulipa kodi kutokana na utitiri huo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia uwekezaji, Anjellah Kairuki, alisema serikali itazishughulikia kero zote zilizotolewa na wafanyabiashara hao likiwamo suala la utitiri wa kodi na tozo mbalimbali, huku akiwataka viongozi wa serikali kufuata taratibu za ufungaji wa biashara, na wafanyabiashara nao walipe kodi kwa hiari.

Pia alitoa wito kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kwenda kuwekeza mkoani Shinyanga, ambapo kuna fursa nyingi ya viwanda vya nguo, na ngozi, huku akipongeza utengwaji wa maeneo mengi kwa ajili ya uwekezaji, na kubainisha ndiyo sera hasa ya rais kuhakikisha wawekezaji hawapati shida ya maeneo na yasiwe na mgogoro.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WATER

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency

RURAL WATER SUPPLY AND SANITATION AGENCY

**Bid No.AE-102/2019/2020/CS/M - 001**
**For**
**Engagementof Private Operators in Operation and Maintenance of Rural Water Service Projects.**

**EXPRESSION OF INTEREST (EOI)**

**Date: 28th February, 2020**

1. The Rural Water Supply and Sanitation Agency (RUWASA)havebeen mandated, by the Water Supply and Sanitation Act No.5 of 2019, to manage the entire water service provision in rural parts of mainland Tanzania. At community level, water services provision is managed by legally established organizations known as Community Based Water Service Organization (CBWO's). These Organizations are formed, registered and regulated by RUWASA.

   Traditionally, the private sector has been extensively involved in design and construction of water service projects at different levels. In efforts to enhance efficiency and effectiveness of organizations and services,RUWASA's intends to expand involvement of Private Sector in provision of water services through strategic collaboration with CBWSOs in operation and maintenance of services and infrastructures at community levelsfor the financial year 2019/2020.

2. The main objective of this exercise is to invite potential private service providers interested in entering into a long – term concession – style contract with, preferably, a group of CBWSO's.

3. The Scope of service shall include but not limited to the following activities;

   i. System operation and maintenance
   ii. Revenue collection
   iii. Rehabilitation, replacement and expansion
   iv. Annual Budget and Planning

4. This is, therefore, toinvite eligible and qualified potential private service providers to indicate their interest in providing the specified services. The interested private service providers must provide information indicating that they are qualified to perform the services by submitting their profiles, description of similar assignments, experience in similar conditions, and availability of appropriate skills among staff.

5. A private service provider will be selected in accordance with the procedures set out in the Public Procurement Act No. 7 of 2011 and the Public Procurement Regulations – Government Notice No. 446 of 2013 together with their Amendments of 2016.The shortlisting will be based on the required capabilities and experience.

6. Interested and eligible private service providers may obtain further information from the office of the Secretary, Tender Board, NBC Bank, Second Floor 2, PMU office, P.O.Box 412, Kuu Road, 40473, Dodoma from9.30 AM on Monday to Friday 3:00 PM inclusive except on public holidays.

7. Expressions of Interest (EoI) in one original plus two copiesmust be enclosed in a sealed envelope properly addressed and delivered to the Secretary, Tender Board, NBC Bank, Second Floor 2, PMU office, P.O.Box 412, Kuu Road, 40473, Dodoma at or before 11.30 am, **27th March, 2020**.The envelopes containing EoI must be clearly marked **"Expression of Interest on Engagement of Private Operator in Operation andMaintenance of Rural Water Service Projects"**

8. Late submissionshall not be evaluated irrespective of the circumstances.

**Director General**
**RUWASA**

215649502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ndivyo mvua zinavyoanza mmechukua tahadhari?

**UTABIRI** uliotolewa na Mamlaka za Hali ya Hewa Tanzania (TMA) mwezi huu, unaeleza kuwa baadhi ya mikoa itapata mvua nyingi mno ambazo zinazotarajiwa kuanza wiki ya kwanza ya Machi.

Mikoa hiyo ni Pwani, Dar es Salaam, Tanga na maeneo mengine ya Kanda ya Ziwa yanatajwa.

Umebakia muda mfupi kabla ya mvua kuanza kwa hiyo tunategemea kuwa kila mmoja amechukua tahadhari kuhusu mvua hiyo ambayo itaanza wakati wowote kuanzia sasa.

Tunawakumbusha viongozi kuwa ni vyema kufuatilia na kuhimiza watu kubadilika. Kwa mfano wanaoishi kwenye mikondo ya maji wawe wamehimizwa na tayari wameshaondoka.

Lakini pia ni vizuri kuwaeleza wachimbaji wadogo migodini kuhusu usalama wao. Ni bora kuchukua tahadhari kwani mashimo ya migodi yanapojaa maji watu wengi hupoteza maisha kutokana na ukosefu wa huduma za kuokoa na uokoaji.

Aidha, miundombinu kama makaro ya majitaka, visima na madimbwi yaliyoko kwenye makazi ya watu wakati mvua inatarajiwa kunyesha tena kwa wastani wajuu yawe yamefunikwa na kuwekewa tahadhari ili kuepusha watu na wanyama kutumbukia.

Tunasema hivi kwa sababu watoto wamekuwa waathirika wakubwa wa ajali zinazotokea kwenye madimbwi.

Wengi wamepoteza maisha kutokana na uzembe unaosababishwa na wajenzi au wauza majina na hata wahusika wa nyumba kushindwa kufunika makaro ya vyoo na majitaka, mashimo ya maji safi, visima vya maji safi au taka.

Kwa sababu mamlaka ya hali ya hewa imeshatoa maelekezo, hatutegemei tena kuona kuwa madaraja na makalavati mabovu yataendelea kuumiza watu wakati taasisi hasa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kuwa mvua inatarajiwa kuwa nyingi.

Tunategemea hata kwa kiasi kidogo wawe wameshachukua tahadhari na muda wote watakuwa karibu na wananchi kufuatilia na kuweka sawa huduma za usafiri hasa kwenye maeneo korofi.

Baadhi ya mambo ambayo yanahitajika kutazamwa kwa jicho la pili ni kuta za uzio na miti inayoelekea kudondoka. Mara nyingi kuta hizo zimesababisha maafa na watu kupoteza maisha.

Ni vyema wananchi watakoa taarifa serikali za mitaa kama wana wasiwasi na ukuta au miti inayoelekea kuanguka iliyo jirani na makazi yao ili kuepusha hatari ya kuleta maafa.

Kwa upande wa shule za msingi, baadhi ya majengo yakiwamo vyoo hutitia wakati wa mvua. Hili nalo ni suala la kuangalia wakati huu wa msimu wa mvua.

Tunawashauri walimu, kamati za shule za misingi na bodi za shule za sekondari wachukue hatua mapema ili kuokoa maisha na kuepusha uwezekano wa wanafunzi kujeruhiwa au kupoteza maisha. Tunapenda pia kutoa angalizo kwa wanaofuga samaki hasa mitaani kwenye makazi ya watu. Hawa nao wamekuwa ni chanzo cha maafa. Mamlaka hasa za uvuvi na maliasili ziwahimize kuboresha mabwawa yao na kuweka mazingira ya kuzuia maji ya ziada ili kuepusha hatari ya kusababisha maafa iwapo maji yataongezeka na kubomoa miundombinu.


Inaamanisha kuwa mabwawa hayo yanaweza kujaa maji na kubomoa nyumba za watu. Aidha, kuna uwezekano wa watoto kutumbukia kwenye mabwawa hayo iwapo hayataimarishwa na kuwekewa vizuizi vya kuwakinga watoto wanaopita kandokando ya sehemu hizo.

Kwa ujumla suala la kujiepusha na madhara ya mvua ni jukumu la watu wote ili kulinda maisha yao. Lakini tunawakumbusha viongozi kuwa wana jukumu kubwa la kufanyakazi ya ziada ili Pamoja na kuwahimiza wananchi kulima na kuzalisha mali kwa wingi ni vyema kuwakumbusha kujali kwanza maisha yao kwani kazi na juhudi zozote hazitakuwa na maana kama hakuna maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Machinga kuuza panga, upinde, hakuna usalama

**NI** rasmi marufuku kwa ujasiriamali mitaani kwa nyenzo na silaha hatari kama mapanga, visu, majambia, lakini, ukweli tunaokutana nao mitaani, tangazo na agizo hilo la kiserikali limeingia sikio moja na kutokea lingine.

Hii inatokana na ukweli kwamba hakuna mabadiliko kwa wajasiriamali, mambo ni kama siku zote, wanauza silaha hizo kwenye mkusanyiko wa watu na wengine kuzipanga barabarani.

Lakini, ikumbukwe wakati akiwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Kamishna Suleiman Kova, alipiga marufuku kwa yeyote au kikundi kuuza mapanga, visu, manati, pinde na mishale barabarani.

Kuchukuliwa hatua hizo, ni kuwakumbusha wauzaji mtu hawezi kufanya biashara hiyo bila ya kuwa na leseni na kwamba hizo ni silaha ambazo jeshi linafahamu vilivyo madhara yake, hivyo ni muhimu wauzaji wafuate taratibu.

Mmachinga anaweza kuuza panga barabarani kwa nia nzuri, lakini kukawapo ugomvi jirani na anapouzia silaha hizo na kujikuta, inaegeuzwa ama kwa hiari au nia tofauti watu wanamnyang'anya na kuzitumia kusababisha madhara makubwa.

Baadaye Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro, alipokuwa Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, naye alipiga marufuku biashara hiyo, lakini kama nilivyosema, bado silaha zimeendelea kuuzwa kama kawaida.

Mbaya zaidi, zinauzwa kwenye mkusanyiko wa watu wa aina mbalimbali, hali inayoonekana kuwa ya kawaida sana, kumbe ni hatari dhahiri. Hivyo, kuna haja ya kuchukuliwa hatua kabla madhara kutokea.

Uuzaji silaha kwenye mkusanyiko wa watu mbalimbali, daima siyo salama. Ni kwa sababu, hata wasiokuwa na akili timamu nao wamo na wanaweza kuzitumia kuwadhuru wengine.

Matukio ya kutumika silaha kuumiza au kuua watu wengine, yanaweza kutokea katika mazingira popote, lakini kuuza silaha hizo kwenye mkusanyiko wa watu, madhara yake yanaweza kuwa makubwa zaidi.

Ninasema hivyo, kwa sababu watu wanaweza kuhoji mbona tindikali haiuzwi madukani, lakini watu wanamwagiwa, au kwamba kupiga marufuku uuzaji wa silaha hizo kwenye mkusanyiko hakuwezi kuzuia madhara.

Inawezekana hilo likawa na ukweli. Tusimame katika usemi, kinga ni bora kuliko tiba. Kwanini kusubiri hadi madhara yatokee, ndipo hatua zichukuliwe?

Kwa kuwa Jeshi la Polisi lilishapiga marufuku, basi kinachotakiwa sasa ni hatua ya utekelezaji wake.

Ikumbukwe, katika mkusanyiko huo, mtu anaweza kuchukua kisu kinachouza au panga na kujeruhi wengine, hapa muuzaji na aliyeumiza wengine atachukuliwa hatua za kisheria.

Hivyo, sioni kwanini wauzaji wanashindwa kutambua madhara ambayo wanaweza kusababisha na badala yake wanaendelea kufanya biashara hiyo kwenye mkusanyiko kama kawaida.

Nakumbuka kuna wakati katika marufuku ya Kamanda Kova, alisema jeshi lipo katika mchakato wa kupendekeza sheria mpya ya matumizi ya silaha na umiliki, ili kudhibiti matumizi mabaya, yakiwamo uuzaji wake holela.

Ni vyema, vijana wanaojishughulisha na umachinga wakauza vingine kama nguo na viatu, kuliko hayo ya silaha ambazo zimezuiwa kuuzwa kiholela.


Vinginevyo, wanaweza kujikuta wakasababisha madhara makubwa bila wao kutarajia na hawawezi kujitetea, kwa sababu tayari Polisi lilishapiga marufuku, lakini bahati mbaya wauzaji na hata wanunuzi wamekuwa wagumu kuelewa.

Wanachokifanya baadhi ya Machinga kwa sasa, ni kwamba wameshasikia marufuku hiyo ya serikali ikaingia katika sikio moja na kutokea lingine, hali inayosababisha waendelee na ubishi kung'ang'ania biashara hiyo.

Uuzaji holela wa panga, visu, jambia na silaha nyinginezo za jadi katika maeneo ya mjini kama Dar es Salaam, unaibua hofu kwa wengine, hivyo ni vyema ikaachwa.

Wakati mwingine, mtu anaweza kukuta Machinga wanavizia foleni za magari na kwenda kutafuta wateja ambao ni abiria. Ni utaratibu usio salama kwa watu wote. Hapo polisi ikaingilia kati kupiga marufuku.

# HABARI PICHANI



Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akiangalia karatasi zinazotumika kuchapia magazeti alipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja wa kiwanda hicho, Balasabramanian.



Mkurugenzi wa Radio One na Capital Radio, Deo Rweyunga (kushoto), akielezea jinsi redio hizo zinavyofanyakazi kwa ujumbe wa NMB Benki ulioongozwa na Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (wa pili kushoto).



Mkuu wa Channel wa ITV na Capital Televisheni, Macharia Koigi, akielezea jinsi matangazo yanavyorushwa kwa ujumbe wa NMB Benki ulioongozwa na Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (wapili kushoto).



Mkurugenzi Msaidizi wa Radio One na Capital Radio, Abdallah Mwaipaya (kushoto), akifafanua jambo kwa ujumbe wa NMB benki ulioongozwa na Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (wa pili kushoto).



Mkuu wa Idara ya Habari na Matukio wa ITV, Stephen Chuwa, akitoa maelezo kuhusu urushwaji wa vipindi kwa ujumbe wa NMB Benki ulioongozwa na Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi.



Ujumbe wa NMB Benki, ukipata maelezo ulipotembelea kituo cha redio cha East Africa. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**

# RC: Hata wanaume wanafanyiwa ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema vitendo vya ukatili wa kijinsia havitokei kwa wanawake pekee bali hata wanaume wanapigwa na kunyanyaswa na wanawake.

Hayo yalisemwa kwa niaba yake jana mkoani hapa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alipokuwa akipokea msafara wa kutokomeza ukatili wa kijinsia ulipowasili jijini hapa.

Alisema jamii imekuwa ikiweka nguvu katika kuwatetea wanawake kwa kuwa wamekuwa wakitoa taarifa ya kufanyiwa vitendo vya ukatili, hivyo nguvu pia inahitajika ya kutoa elimu kwa wanaume ili kutoa taarifa ya vitendo hivyo.

Chalamila aliongeza kuwa serikali inaendelea katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa dhidi ya wanawake na watoto kwa kuanzisha mipango na sera mbalimbali zinazosaidia kutoa elimu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika mapambano ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Sisi mkoa wa Mbeya tuko vizuri tunapambana na vitendo vya ukatili. Juzi tu tulipata taarifa kutoka kwa mtoto kuwa anafanyiwa vitendo vya ukatili na baba yake na tumeshamchukulia hatua za kisheria," alisema.

Akizungumzia malengo ya msafara wa kijinsia, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Imelda Kamugisha, alisema msafara huo umelenga kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia katika familia na jamii kwa ujumla.

"Kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, tumekuja na msafara wa kijinsia ili kutoa elimu kwa wanajamii kuhusu kupambana na vitendo vya ukatili," alisema.

Balozi wa Kampeni ya Twende Pamoja, Nurdin Bilal 'Shetta', alisema suala la mapambano ya ukatili wa kijinsia ni la jamii yote, hivyo wameungana na serikali katika kuhakikisha elimu inaifikia jamii ili kuondokana na vitendo hivyo.

# Raia Uturuki ahukumiwa kulipa mil. 100/-

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJA Uwezeshaji wa Kampuni ya Yapi Markezi, inayojenga reli ya kisasa (SGR), Yetkin Mehmet, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 100 baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kushindwa kujieleza kuhusu Dola za Marekani 84,850 alizokutwa nazo uwanja wa ndege.

Hukumu hiyo ilitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas, dhidi ya mshtakiwa huyo ambaye ni raia wa Uturuki.

Kadhalika mahakama hiyo imezitaifisha dola hizo na kuwa mali ya serikali.

Wakili wa Serikali Mkuu, Shadrack Kimaro, alidai kuwa Februari 13, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, mshtakiwa alikutwa na Dola 84,850 na kwamba alishindwa kuzitolea maelezo kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, mshtakiwa alikuwa akisafiri kwenda Uturuki kwa ndege ya Shirika la Ndege la Uturuki (Turkish Airlines). Mshtakiwa alikiri kutenda kosa hilo na mahakama imemtia hatiani kwa kosa moja.

Akiwasilisha hoja ili mshtakiwa apewe adhabu, Kimaro alidai ni mkosaji wa mara ya kwanza, hivyo aliomba apewe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Wakili wa utetezi, Augustine Shio, aliomba mahakama impe adhabu ndogo mshtakiwa kwa sababu ni mkosaji wa mara ya kwanza na anategemewa katika ujenzi wa reli hiyo ya kisasa akiwa meneja uwezeshaji.

Hakimu Simba alisema kwa kuzingatia hoja za pande zote mbili, Mahakama inampa adhabu mshtakiwa ya kulipa faini Sh. milioni 100 na akishindwa ataenda jela miaka mitatu.

Alisema Mahakama pia imeamuru Dola 84,850 alizokutwa nazo zitaifishwe na kuwa mali ya serikali. Hadi jana mchana, mshtakiwa alikuwa anahangaika kulipa faini ili kunusurika na kifungo.



Mteja akiangalia viatu vilivyopangwa chini kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Mwisho jijini Dar es Salaam juzi. Wafanyabiashara wadogo hawajapata maeneo maalum ya kutosha kufanyia shughuli zao, kitendo kinachosababisha wavamie maeneo hata yasiyo rasmi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Adai kuvamiwa baada ya kuibua tuhuma za ufisadi

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MAOFISA wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, wamedaiwa kumfanyia upekuzi usio halali Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kwamba, Abdi Makinda, kwa kile kilichoelezwa kutaka kumbambikia kesi ili kumnyamazisha kufuatilia ufisadi wa Sh. milioni 36 za mradi wa josho la mifugo zilizotolewa na serikali ya kijijini kwake.

Makinda alimwambia mwandishi wa habari hii kuwa maofisa watatu walimfanyia kitendo hicho wiki moja baada ya kulalamikia ufisadi huo na kuiandikia barua halmashauri akiitaka kueleza vigezo vilivyotumika kumlipa mkandarasi fedha zote kabla ya mradi kukamilika.

Alisema anaamini kwamba kitendo hicho cha maofisa hao kimefanywa kama kumdhalilisha na kumtisha asifuatilie ubadhirifu wa fedha hizo na kwamba amechukua hatua ya kufungua jarada polisi kulalamikia tukio hilo baada ya kuambiwa aache kimbelembele.

"Naamini kuwa tuhuma hizi zinalenga kunitisha na kuninyamazisha ndiyo maana nimefanyiwa haya baada ya kuandika barua.

Kama ni suala la kawaida mbona tuhuma hizo hazijatokea miaka yote kabla ya mimi kulalamikia suala hili? Iweje baada ya barua nihusishwe na wizi wa maliasili?" Alihoji Makinda.

Alisema hofu yake sasa ni kubambikiwa kesi kutokana na kile alichodai kuonekana adui kwa kulalamikia tuhuma hizo huku akihoji uhalali wa kuhusishwa mhandisi wa ujenzi na meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) katika tuhuma za wizi wa maliasili badala ya polisi au Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Gratian Makota, licha ya kukiri kutokea kwa tukio hilo, alitaka kutohusishwa na taarifa ya mwenyekiti huyo aliyoitoa kwenye halmashauri, huku akidai upekuzi wake ulikuwa wa kawaida tu.

"Ni kweli huyo mwenyekiti hata mimi alinilalamikia suala hilo na mimi nikamshauri kama anaona hakutendewa haki aende Polisi. Ameenda Polisi na maofisa hao wameitwa kuhojiwa sasa sisi tunahusikaje?" Alihoji Makota.

Alitaka mwenyekiti huyo kupuuzwa kwa madai kuwa kuficha ufisadi si kigezo cha kumfanya awe juu ya sheria na akifanyakosa asiguswe na kwamba atashughulikiwa na atakamatwa tu endapo atajihusisha na makosa kama wengine.

Kwa mujibu wa Makota, maofisa waliokwenda kufanya upekuzi huo kwa mwenyekiti ni ofisa maliasili, Meneja wa Tarura na Mhandisi wa Ujenzi ambao walikwenda huko baada ya kupata tuhuma za kujihusisha na biashara za mazao ya misitu bila kufuata utaratibu wa kisheria.

HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma kuiba maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (Kuwasa), imemkamata Msoud Nchumbo, mkazi wa Mtaa wa Sazia, Kata ya Nyihogo mjini Kahama, ikimtuhumu kujiunganishia maji ya mamkala hiyo kinyume cha taratibu.

Akizungumza kwenye eneo la tukio, Meneja Biashara wa Kuwasa, Misana Shija, alidai Nchumbo alikuwa akiiba maji ya mamlaka hiyo kwa kuyachepusha ili yasipite kwenye mita.

Shija alidai kukamatwa kwa Nchumbo kunatokana na taarifa za ankara za malipo yake kutobadilika kila mwezi, jambo ambalo liliwashtua na kuamua kufuatilia kwa karibu na kubaini amefunga mabomba yanayopitisha maji kwenye maeneo mbalimbali ya nyumba yake bila kupita kwenye mita.

"Mteja huyu hivi karibu alikuwa na malalamiko juu ya mita yake kuwa ni mbovu na kutaka ihamishiwe ndani, lakini cha kushangaza kaja kuunganisha mpira wa maji hadi bafuni na chooni, maji ambayo hayapiti kwenye mita na ukiangalia ana familia kubwa sana.

"Msoma mita wetu kila mwezi anaposoma mita ya Msoud Nchumbo anakuta mita haisogei na huku ana familia kubwa na anatumia maji kila siku. Baada ya taarifa hii, tulichukua hatua ya kumkagua na kubaini wizi huu.

Sheria itachukua mkondo wake na atarejesha gharama za maji aliyotumia," alionya.

Msimamizi wa Huduma ya Maji Kata ya Nyihogo, Mary Michael, alidai: "Nilifika nyumbani kwa Nchumbo, nikaifunga mita, lakini cha kushangaza kulikuwa na mtu bafuni anaoga na nilipotoa taarifa ofisini na kuja kufanya ukaguzi, walibaini wizi huu."

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyihogo, Cosmas Bukango, alisema kitendo hicho ni kuhujumu uchumi wa mamlaka na kupoteza mapato yake.

Bukango alisema Nchumbo anashikiliwa na Jeshi la Polisi wilayani Kahama wakati taratibu za kisheria na uchunguzi zikiendelea ili afikishwe mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, anayeshughulikia Sekta ya Ujenzi, Elius Mwakalinga (wa pili kushoto), akitoa maagizo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Eliazary Rweikiza (kulia), alipokuwa akikagua ujenzi wa barabara ya Isyonje-Makete yenye urefu wa Km 96.4, inayounganisha mkoa wa Mbeya na Njombe, juzi. **PICHA: WUUM**

# Muhimbili watibu saratani kidigitali

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili, Tawi la Mloganzila, imetoa mafunzo kwa madaktari bingwa wa upasuaji kutoka hospitali za mikoa ya rufani ya kufanya upasuaji wa kuondoa uvimbe wa saratani ya ziwa bila kulikata.

Mafunzo hayo yalianza Jumatatu ya wiki hii na kushirikisha madaktari 12 kutoka Hospitali za Rufani ya Bugando, KCMC, Benjamin Mkapa na Mbeya na wanatarajia kuwafanyia upasuaji wagonjwa wanane kwa siku tatu.

Daktari Bingwa wa Upasuaji ambaye ni Mtaalamu wa Upasuaji wa Saratani za Matiti, Dk. Caspar Haule, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafunzo hayo yatakayofanyika kwa siku tano katika hospitali hiyo.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo madaktari kufanya upasuaji wa kuondoa uvimbe wa saratani ya ziwa bila kulikata katika hospitali za mikoa nchini.

"Madaktari tulianza kukutana Jumatatu kwa ajili ya kukumbushana kuhusu majukumu yetu na leo (juzi) tumefanyia upasuaji wagonjwa watano na wengine watatu tutamalizia (jana). Hii ni mbinu mpya ya upasuaji wa kuondoa uvimbe wa saratani kwenye ziwa bila kulikata lote," alisema.

Alisema kati ya operesheni hizo nane wanazofanya, wagonjwa wanne wanafanyiwa upasuaji wa kuondoa uvimbe bila kukata ziwa na wengine wanne wanakatwa ziwa.

Alisema sababu za wagonjwa kukatwa ziwa ni kuchelewa kugundua tatizo kwa sababu ugonjwa wa saratani ya ziwa hauna maumivu hadi unapofikia hatua mbaya.

Alisema huduma hiyo walianza Aprili mwaka jana kwa kufanya utafiti kwa wagonjwa 162 na kati yao 152 walifanyiwa upasuaji na 20 waliondolewa uvimbe bila kukata ziwa.

Alisema lengo la kuwapo kwa huduma hiyo ni kuwasaidia wagonjwa kuendelea kuishi miaka mingi zaidi hasa vijana ambao wanagundulika kuwa na tatizo hilo kutibiwa bila kukatwa ziwa.

Alisema mgonjwa hupona baada ya siku 14 tangu afanyiwe upasuaji wa kuondoa uvimbe.

## Mwanasheria azipa mbinu Azaki

**Na Elizabeth Faustine, MWANZA**

MWANASHERIA wa Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB), Neema Kimambo, amezitaka Asasi za Kiraia (Azaki) kuwa sauti moja kuhakikisha mikataba ya ununuzi wa umma inakuwa wazi, ili kuimarisha utawala bora na kuondoa rushwa.

Alitoa rai hiyo jijini Mwanza wakati akiwasilisha mada kwa washiriki wa warsha ya siku moja ya Azaki mbalimbali kuhusu utekelezaji wa mikataba wazi kwenye ununuzi wa umma nchini.

Kimambo alisema ununuzi wa umma ndiyo msingi na kiini cha matumizi ya serikali yoyote na kwamba udanganyifu na ukosefu wa usimamizi unaweza kuathiri wananchi na serikali kwa ujumla.

"Wakati Tanzania inapambana kutatua tatizo la miradi ikamilike kwa wakati na ufanisi uongezwe, bado kuna tatizo la kutowekwa wazi kwa baadhi ya miradi.

"Rais John Magufuli anashughulika hasa kupambana na rushwa kuhakikisha kila hesabu katika miradi inatumika ipasavyo, lakini bado tunahitaji kuongeza kasi kwenye uwazi," alisema.

Aliongeza kuwa Mpango wa Maendeleo Endelevu (SDGs 2030) unaeleza kuwa ifikapo mwaka 2030 rushwa iwe imeondolewa, kupungua kwa umaskini na kuwapo kwa uwazi kutafanikisha malengo hayo ya milenia.

"Tukiwa katika mchakato wa kuandaa mwongozo kwa wabunge kuhusu suala hili, ni wakati wa Azaki kufuatilia kwa kujadili fedha za wananchi zinatumikaje. Je, zinatumika ipasavyo? Hii itakuza uwajibikaji na maendeleo," alisema.

Mmoja wa washiriki katika warsha hiyo kutoka Taasisi ya Sayansi ya Jamii (Tasaja), Emmanuel Ndomondo, alisema ni wajibu wa wananchi na Azaki kufuatilia ununuzi wa umma wenye uwazi ili kuleta manufaa kwa jamii.

"Ifikie wakati suala hili la uwazi tuone ni letu sote, sababu kila pesa inayonunua kitu kutoka serikalini ni ya wananchi, ni wajibu wetu kuhoji na kufahamu matumizi yetu," alisema.

Ofisa Miradi kutoka TCIB, Annexius Mwoza, alisema kwa sasa unaandaliwa utaratibu kuhakikisha wananchi kuanzia ngazi ya serikali za mitaa wanaona mikataba inayoingiwa na serikali.

"Sababu ni kodi ya wananchi, hii ni kuunga mkono juhudi za serikali hii. Rais anatafuta pesa nchini kwa shida ili zifanye miradi mbalimbali, lakini baadhi ya wasimamizi wanamwangusha. Mfano, suala la hivi karibuni la Zimamoto, kungekuwa na mikataba yenye uwazi kwa umma, pengine yasingetokea yaliyotokea kwa kina Kangi Lugola," alisema.

# Watendaji wabanwa mapato kushuka

**Robert Temalilwa,** BAGAMOYO

MKUU Wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa, ameiagiza halmashauri ya wilaya hiyo kueleza sababu ya kushindwa kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uchimbaji wa mchanga ambao ndiyo chanzo kikuu cha mapato yao.

Pia ameutaka uongozi wa halmashauri hiyo kutoa maelezo ya kina kwanini mashine za makusanyo (posi) zinazimwa na kushindwa kukusanya mapato kwa muda mrefu.

Akizungumza na watumishi na madiwani wa halmashauri hiyo juzi, Kawawa alisema wanapaswa kubadilika kwa kuhakikisha wanasimamia na kufuatilia mapato pasipo kujenga uongo na udanganyifu. "Haiwezekani mapato ya mchanga yanashuka licha ya vyombo vya ulinzi na usalama kubaini mianya na udanganyifu hasa katika eneo hili la mchanga, mmefikia hatua ya kuidanganya hadi Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), mnapotosha taarifa na takwimu sahihi za makusanyo ili kujinufaisha.

"Ninahitaji maelezo pia kwanini mnazima mashine, mnazima kwa kipi? Nahitaji maelezo na nakala nyingine ielekezwe kwa Mkuu wa Mkoa na nyingine Tamisemi (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)," aliagiza.

Aliongeza kuwa kuzimwa kwa posi ni kukiukwa maelekezo ya Tamisemi, akisisitiza kuwa halmashauri ni eneo lenye heshima na hadhi yake, hivyo inapaswa kuendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ally Issa, alisema hali ya mapato hairidhishi kutokana na chanzo mama cha mchanga kuyumba, akibainisha kuwa makusanyo yamefikia asilimia 43 wakati walitakiwa kufikia asilimia 50 kwa kipindi cha miezi sita ya mwazo ya mwaka wa fedha.

Alisema wamebaini machimbo holela ya mchanga 23 na sasa wako katika mkakati wa kuyafunga baadhi ya machimbo na mengine kuyarasimisha na kuongeza usimamizi ili kudhibiti utoroshaji.

Ally alisema machimbo ambayo yamesharasimishwa ni pamoja na Nzole, Fukayose na Mapinga.

Kuhusu kuzimwa kwa posi, Ally alisema kuna mashine zimeharibika na hazifanyi kazi, na tayari wamenunua posi mpya 43 ili kutatua tatizo lililojitokeza.

Ofisa Mazingira wa Bagamoyo, Cleophace Murugwa, aliwataka wachimbaji kufuata taratibu za kupata kibali na leseni ili kuepuka usumbufu.

# DC apiga marufuku 'vigodoro' usiku

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa, amepiga marufuku ngoma na miziki nyakati za usiku bila utaratibu maarufu kama 'vigodoro'.

Amesema ngoma hizo zikiambatana na muziki zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa mmomonyoko wa maadili kwa wananchi.

Kawawa alitangaza marufuku hiyo wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Nianjema, wadau wa maendeleo na wakuu wa idara wakati wa mkutano wake wa kikazi kwa ajili ya kusikiliza kero na changamoto za wananchi. Alisema katika baadhi ya maeneo ya wilaya hiyo, kumekuwapo na wimbi la ngoma ambazo zinachezwa nyakati za usiku, hali inayosababisha kero na usumbufu kwa watu wengine.

Kutokana na hali hiyo, alisema ameamua kuchukua hatua ya kupiga marufuku kwa lengo la kuondokana na matukio ambayo yamekuwa yakijitokeza hasa wakati wa usiku.

Aidha, alisema wananchi wa Bagamoyo wanatakiwa kubadilika na kuwa na mtazamo chanya kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo, badala ya kutumia muda wao kukesha nyakati za usiku wakicheza ngoma ambazo hazina faida yoyote katika Taifa.

Alisema yeyote atakayebainika kukiuka marufuku hiyo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kwamba yeyote anayehitaji kufanya shughuli nyakati za usiku ahakikishe anapata kibali maalum kutoka katika ofisi yake kwa kuzingatia taratibu na kanuni zilizowekwa.

Diwani wa Nianjema, Abdul Pyalla, alikiri kwamba suala hilo la vigodoro limekuwa kero kwa wananchi, hivyo atahakikisha anashirikiana na Mkuu huyo wa Wilaya, kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia muda wao katika shughuli za maendeleo.



Vipande vya chupa vikiwa vimezagaa katika Barabara ya Maktaba, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa waenda kwa miguu, lakini pia kwa magari kwani vinaweza kusababisha pancha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ahimiza matumizi chokaa mazao kurutubisha ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

KATIBU Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Iringa anayeshughulikia masuala ya uchumi na uzalishaji, Eliya Mvanda, amewahimiza wakulima kutumia nishati ya chokaa mazao ili kurutubisha ardhi iliyopoteza thamani.

Hatua ya matumizi ya chokaa mazao itasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na hatimaye kuongeza tija kwa mkulima mmoja mmoja na taifa.

Mvanda aliyasema hayo jana mkoani Iringa wakati akizindua mradi wa 'Kuboresha Udhibiti wa Tindikali ya Udongo kwenye Ardhi ya Kilimo Tanzania'.

Alisema mradi huo umekuja wakati mwafaka wakati serikali imeweka kipaumbele katika kuimarisha afya ya udongo hasa katika kubatilisha tindikali katika udongo.

Nishati hiyo inazalishwa na Kampuni ya Dodoma Cement kama mzalishaji wa chokaa mazao na katika kipindi cha 2020/2021 inatarajia kusambaza bidhaa hiyo nchini ili kubatilisha tindikali katika udongo na kuleta tija kwenye kilimo.

"Kampuni hii ina uwezo wa kuzalisha chokaa mazao tani 15,000 kwa mwaka, kiwango hicho kitaongezeka mara tatu zaidi na kufikia tani 45,000 kwa mwaka ifikapo 2021," alisema.

Katibu Tawala huyo alisema kutokana na utafiti uliofanywa na Taasisi za Kitaaluma na Utafiti za TARI Uyole, SUA na za kimataifa, umeonyesha rutuba katika udongo kwenye baadhi ya maeneo ya Tanzania imepungua kutokana na kulimwa na kutifuliwa mara kwa mara bila kuwa na mikakati thabiti ya kuhuisha udongo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Dodoma Cement, Charles Numbi, alisema lengo ya kampuni hiyo kuzalisha tani 15,000 za chokaa mazao kwa mwaka kwa ajili ya kukidhi mahitaji katika mikoa ya Iringa, Rukwa, Katavi, Njombe na Ruvuma, ambayo imeathirika zaidi za tatizo la tindikali.

Alisema kampuni hiyo inashirikiana na Idara za Kilimo katika halmashauri za mikoa ya Iringa, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Katavi na taasisi binafsi za ADP-Mbozi na RUCODIA.

Numbi alisema watawajengea uwezo wakulima na wauzaji wa pembejeo wa mikoa hiyo, kwa lengo la kuboresha uuzaji na usambazaji wa chokaa mazao kwa wakulima takribani 50,000 na ardhi ya kilimo isiyopungua hekta 20,000 katika mikoa hiyo.

Kampuni hiyo yenye makao yake makuu jijini Dodoma, imejikita katika uzalishaji na usambazaji wa chokaa mazao (Agriculture Lime), inayotumika kwa ajili ya kutibu udongo ulioathiriwa na tindikali kwa takribani miaka mitano sasa.





# DC ataka vikundi vitumie mkopo kuboresha biashara

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, amevitaka vikundi 147 vya wajasiriamali vilivyoko Halmashauri ya Jiji la Arusha vilivyopewa mkopo usio na riba wa zaidi ya Sh. milioni 805.6 kuzifanyia kazi iliyokusudiwa ya kuboresha biashara zao, ili wazirudishe kwa wakati kwa ajili ya kusaidia na wengine.

Pia aliwaagiza maofisa maendeleo ya jamii wa jiji hilo, kuwa makini na usajili wa vikundi ili kuepuka usajili wa vikundi hewa. Aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akikabidhi hundi ya zaidi ya Sh. milioni 805.6 kwa vikundi hivyo, ambavyo kati yake vinne vya watu wenye ulemavu.

Alisema endapo mtu atapatiwa fedha hizo na kuacha kuzirejesha anakwamisha wenzake kupewa mkopo huo kwa ajili ya kufanyia kazi. "Pia nawaomba nyie vijana muige kinamama vikundi vyao vinaongoza kufanya vizuri, lakini nyie mkipewa mnaenda kucheza 'Pool Table' na kuzifanyia mambo yasiokusudiwa na matokeo yake mnashindwa kurejesha nawaomba mkahamasishane kurejesha fedha hizi," alisema.

Aliwataka maofisa maendeleo ya jamii kujipanga kutoa elimu kwa wajasiriamali kabla ya kuwapatia fedha hizo, ili wafahamu jinsi ya kuzitumia na kuzirejesha. Kuhusu vikundi hewa alisema endapo atakuta kata yoyote ina vikundi hewa, atawachukulia hatua kali maofisa maendeleo ya jamii kwa sababu ndiyo waratibu wa vikundi kwenye kata zao.

Aliagiza kila kikundi kitakachopatiwa mkopo wasipungue watu 10, isipokua vya watu wenye ulemavu ambao wameruhusiwa kuwa watano na siyo vinginevyo. "Nikikuta kikundi kina watu wawili maana yake hawa wapiga dili tu, hawastahili kupewa mkopo na nikikuta vikundi vya namna hii, namchukulia hatua Ofisa Maendeleo ya Jamii maana sehemu nyingine wanakula nao," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, alisema mikopo wanayotoa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo wananchi wanapaswa kuishukuru serikali kwa kuwajali.

"Sisi tuliagizwa na serikali kutenga sehemu ya mapato yetu ya ndani kutoa mikopo hii, hivyo mkiipata tumieni vizuri hakuna vitu vya bure, pamoja hauna riba, lakini mnapaswa kuirejesha kama mlivyopewa ili tuwape wengine wahitaji," alisema. Alisema kuna changamoto ambayo anaifuatilia ya baadhi ya maeneo, Maofisa Maendeleo ya Jamii wanatengeneza vikundi hewa, hivyo akibainI kuna ukweli wahusika watachukuliwa hatua.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Manamsiu Dossi, alisema mkopo huo umetolewa kwa vikundi 147 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyopo kwenye kata 25 za halmashauri hiyo, kwa awamu ya piili ya mwaka wa fedha 2019/2020.

# Aomba msaada kumtibu mtoto ubongo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKAZI wa Mianzini Wilaya ya Arusha, Veronica Laurence Sulley, anaomba Watanzania kumsaidia Sh. milioni 22 ili ampeleke mtoto wake Paskalina Aloyce Kyara (10) nchini India, kutibiwa tatizo la ubongo linalomsumbua kwa miaka tisa sasa.

Akizungumza kwa masikitiko na Nipashe jijini Arusha, Veronica alisema, mtoto huyo alimzaa Aprili 17, 2010 akiwa mzima, lakini alipofikisha mwaka mmoja akaanza shida ya kushindwa kugeuka, kuonyesha ishara yoyote anapohitaji kula, wala kuchezesha viungo vyake vya mwili.

"Hapo nilianza safari ya matibabu yake Hospitali ya Mkoa Mount Meru, Selian, KCMC, Muhimbili ambako walinishauri niende nchini India na baadaye watu wenye mapenzi mema walinichangia fedha nikampeleka India Septemba 2, 2019, katika Hospitali ya Zydus, ambako walimpa matibabu," alisema.

Alisema baada ya kupata matibabu kwa muda mfupi aliona matokeo mazuri kwa mwanawe, kama vile kumudu kuonyesha ishara anapohitaji chakula, kuchezesha viungo mikono na miguu, jambo ambalo awali hakuweza kufanya hivyo, alikua wa kugeuza tu.

"Lakini kule India niliambiwa yale matibabu awamu ya kwanza, hivyo ninapaswa kumrudisha tena mwaka huu kwa ajili ya matibabu makubwa zaidi ya yale ambayo yatagharimu Sh. milioni 22 na akipata matibabu hayo atapona mwanangu, naomba mnisaidie sina uwezo wowote," alisema.

Alisema kutokana na hali yake kuwa duni alipatiwa barua Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Arusha ya kibali cha muda cha kuchangisha fedha hizo kwa wananchi, ambacho kilitolewa Januari 9, mwaka huu na kinatakiwa kuisha Machi 8.

Veronica alisema kibali hicho kinakaribia kuisha muda wa kuchangisha, bado hajafanikiwa kupata fedha hiyo, hivyo anaomba watu wenye mapenzi mema wamchangie kupitia akaunti aliyofungua Benki ya CRDB yenye namba 0152415093700 na namba yake ya kiganjani ni 0689899140.

"Ninaamini nikimpeleka awamu hii mtoto wangu atapona, kwa sababu alikuaa hata kula ugali hawezi, lakini nilipompeleka kwa miezi michache anakula ugali sasa, hii ni hatua kubwa sana kwake maana nyuma alikuwa anaishi kwa chai na uji tu," alisema.



Mkazi wa Mianzini jijini Arusha, Veronica Laurence Sulley, akiwa amempakata mwanawe Paskalina Aloyce Kyara (10), mwenye shida kwenye mfumo wa ubongo wake, akiomba Watanzania kumchangia Sh. milioni 22, kupitia akaunti ya Benki ya CRDB yenye namba 0152415093700 na namba yake ya kiganjani ni 0689899140, ili ampeleke nchini India kwenye matibabu. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# TRA yakamata shehena mapipa 50 ya kemikali

**Na Mary Mosha,** ROMBO

MAMLAKA ya Mapato nchini Mkoa wa Kilimanjaro (TRA), imekamata shehena ya mapipa 50 ya kemikali (spirit) lita 12,500 yenye thamani ya Sh. milioni 15.53 iliyokuwa ikisafirishwa kutoka nchini kwenda Kenya kupitia njia zisizo rasmi.

Akizungumza jana katika kituo cha forodha cha Holili, kilichopo Wilaya ya Rombo, Meneja wa TRA, Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema mapipa hayo ya kemikali, yalikamatwa Februari 24, mwaka huu yakisafirishwa kwenda Kenya kupitia njia za panya.

Mwangosi alisema, kemikali hizo zina thamani ya Sh. 15,531,480 na zilikuwa zikisafirishwa na gari lenye namba za usajili T 568 BQJ aina ya Mitsubishi Fusso ambalo linashikiliwa kwa ajili ya uchunguzi.

Katika hatua nyingine meneja huyo alisema kuwa, wamefanikiwa kukamata simu za kiganjani aina ya Itel takribani 1,076 zenye thamani ya Sh. 14,854,998 zikitokea nchini Kenya, kuingizwa nchini kupitia njia zisizo rasmi.

Simu hizo zilikuwa zikisafirishwa na gari lenye namba za usajili T 355 DDT aina ya Toyota TownAce ambalo linashikiliwa na mamlaka hiyo.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2014, kuingiza bidhaa au kutoa nje ya nchi bila kufuata sheria ni kosa na adhabu yake inaweza kuwa kulipa faini au kutaifisha bidhaa pamoja na chombo kilichotumika kusafirishia bidhaa hizo.

Alisema, mamlaka hiyo imefanikiwa kukamata mifuko miwili ya mirungi yenye uzito wa kilogramu 120 na aliyekuwa akisafirisha aliitelekeza na kukimbia.

Alitoa wito kwa wananchi wanaojishughulisha na vitendo vya magendo kuacha tabia hiyo kwa kuwa vitendo hivyo vinachangia kupoteza mapato halali ya serikali na kupunguza uwezo wa kutoa huduma muhimu kwa wananchi.

"Bidhaa za magendo zinaathari katika uchumi wa taifa kwa sababu zinaleta ushindani wa bidhaa usio na afya sokoni, lakini pia zinaathari katika usalama wa afya za wananchi na taifa kwa ujumla kwa sababu bidhaa zisizo na viwango na ubora zinaweza kuingizwa na kuuzwa kwa wananchi," alisema Mwangosi.

Samson Mlay ni mfanyabiashara anayetumia kituo cha forodha cha Holili, alisema ipo haja ya Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhakikisha wanazidi kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili kuona umuhimu wa kulipa kodi.

# Mbunge aonya wanaonyemelea jimbo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MBUNGE wa Jimbo la Mbulu Vijijini, mkoani Manyara, Flatei Maasay, amewataka wajumbe wa mkutano mkuu wa Chama Cha Mpinduzi (CCM) wa wilaya hiyo kutohadaiwa kwa kuombwa kura kwa njia ya simu na baadhi ya watu wanaonyemelea nafasi ya ubunge.

Maasay akizungumza jana kwenye mkutano huo uliofanyika katika Kata ya Yaeda Ampa, alisema muda wa kufanya kampeni bado, hivyo wagombea wasiwasumbue wajumbe hivi sasa.

Alisema siyo jambo zuri kwa mwenye nia ya kugombea ubunge wa jimbo hilo kuanza kuomba kura kwa wajumbe kwa kupiga simu na kuanza kujitambulisha kuwa atakuwapo kwenye kinyang'anyiro.

"Yaani siyo jambo zuri jamani mwanaume mwenzio anakupigia simu na kumwomba kura au mnakutana barabarani anaanza kukueleza umpigie kura wakati muda bado," alisema Maasay.

Alisema kura zinapaswa kuombwa sehemu husika na muda ukifika na siyo sasa kama wanavyofanya baadhi ya watia nia wanaosumbua watu kwa njia ya simu au kukutana uchochoroni na kuanza kuomba kura.

Alisema wagombea wanapaswa kusubiri muda wa kuchukua fomu na kugombea na siyo kujipitisha na kuanza kuhadaa wajumbe kwa sasa, ilhali yeye bado ni mbunge wa jimbo hilo.

"Muda wangu utaishia baada ya Bunge la Bajeti na hapo nitakuja tena kwenu kwa kuwa tumeshirikiana kufanikisha maendeleo katika sekta ya elimu, afya, maji, miundombinu na mengine mengi," alisema Maasay.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Yaeda Ampa, Emmanuel Baynet, alimtaka mbunge huyo, kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa wananchi wa Mbulu bado wana imani kubwa kwake.

"Wewe hivi sasa usiwaze uchaguzi wa mwaka huu wa 2020, waza uchaguzi wa mwaka 2025, kwa kuwa wananchi wanakupenda kama mheshimiwa Philip Marmo aliyeongoza kwa miaka 25 nawe utakuwa hivyo tutakupa kipindi kirefu," alisema Baynet.

Alisema wakati anagombea ubunge mwaka 2015 hakuwa na fedha, lakini alipewa ubunge na mwaka huu atachaguliwa tena kwa kuwa walimkopesha ubunge na amewalipa maendeleo.



Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini mkoani Manyara, Flatei Maasay, akizungumzia mikakati ya maendeleo ya eneo hilo katika mkutano na wananchi wa kata ya Dongobesh juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbowe ashindwa kuhudhuria uzinduzi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MBUNGE wa Hai na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ameshindwa kuhudhuria uzinduzi wa Baraza jipya la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, mkoani Kilimanjaro licha ya kuombwa kwa barua kushiriki. Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai (TEO), Noel Nnko, alilieleza baraza hilo kuwa mbunge huyo hajatoa taarifa za ushiriki wake licha ya katibu wake wa jimbo kupewa barua kwa kusainishwa.

"Hatujafahamu ni kwanini mbunge wetu ameshindwa kufika hapa kushiriki shughuli za uchaguzi wa viongozi wa baraza hili na hata kuja kuzungumza na wananchi wake. Tulimkabidhi katibu wake barua ya kuitwa kushiriki mchakato huu kwa barua, lakini hawakutokea," alisema Nnko. Alipotafutwa kuzungumzia madai hayo, Mbowe ambaye ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB), hakuweza kupatikana kutokana na simu yake kuita bila majibu baada ya kupigiwa mara kadhaa. Baraza hilo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai, linaundwa na wenyeviti 17 wa vitongoji na wajumbe wa baraza sita wanaotokana na Viti Maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kwa mujibu wa mtendaji huyo, wajumbe wa baraza hilo walimchagua Mwenyekiti wa Serikali ya Kitongoji cha Jiweni, Godfrey Kivuyo kuwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai na Makamu wake ni Fadhili Ng'anzi.

Eneo lenye makazi ya watu wengi ili kukidhi vigezo vya kupewa hadhi ya mji kamili, umeelezwa na kufafanuliwa kwenye kifungu cha 27 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Namba 7 ya mwaka 1982 na kifungu cha 5 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji), Namba 8 ya mwaka 1982.

# Serikali kutafuta fedha uchunguzi wa magonjwa Hai

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imesema kuanzia sasa, itatafuta fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kila baada ya miezi mitatu kutokana na uhitaji mkubwa uliojitokeza.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Yohana Sintoo, alisema wanalazimika kufanya hivyo kutokana na mwitikio mkubwa wa wakazi wa Hai na wilaya za jirani kutafuta huduma za uchunguzi na tiba kupitia kliniki tembezi ya madaktari bingwa.

Alikuwa akizindua kambi maalumu ya uchunguzi wa mifupa, magonjwa ya wanawake, koo, watoto, macho na pua katika Hospitali ya Wilaya ya Hai inayoendeshwa na madaktari bingwa wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi).

"DMO (Mganga Mkuu wa Wilaya), nakuagiza liandikie hili kwamba tunaona sasa ni vizuri kliniki hii ikafanyika kila robo mwaka, badala ya miezi minne na kama kuna sehemu au vikao mnafanya mjadili hilo, na nafikiri kuna haja tukafanya zoezi hili kila baada ya miezi mitatu kwa sababu ni lazima tuende na wepesi fulani ambao ni muhimu pia na sisi tuwe tayari kwa sababu ya hali halisi.

"Na kwa sababu sisi wafanya maamuzi tupo, basi tupeleke pendekezo hili, mimi nadhani nina nafasi yangu ambayo nitahitaji niandike angalau, hii kliniki tembezi ifanyike kila baada ya robo mwaka na mimi naliona hili ni jema, kwa kuwa miezi minne ni mingi sana na wagonjwa wanaweza kufa kabla ya kufika hiyo miezi minne."

Kwa mujibu wa Sintoo, licha ya kuwapo kwa uhitaji huo, ofisi yake inafahamu kwamba kuna changamoto ya rasilimali na namna ya kujipanga kwa maana ya madaktari waliopo, lakini pili vifaa ambavyo vinahitajika.

Mratibu wa kliniki hiyo tembezi, Dk. Elirehema Shirima, alisema moja ya tatizo wanalokutana nalo katika kambi hiyo ni ufinyu wa vitendea kazi vinavyotumiwa na madaktari bingwa kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa, hivyo kuwalazimu madaktari bingwa kuja na baadhi ya vitendea kazi vyao binafsi. Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Irine Haule, akitoa ufafanuzi kuhusu uchangiaji wa gharama za uchunguzi, alisema bima zote zinaruhusiwa katika kliniki hiyo tembezi, ikiwamo bima afya ya jamii (iCHF) inayotumika katika Wilaya ya Hai.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto, Dk. Anjelika Massao, akizungumzia kliniki hiyo, aliiomba serikali wilayani Hai kutafuta fedha za kugharamia kliniki hiyo kufanyika kila baada ya miezi mitatu kutokana na changamoto za afya wanazokutana nazo.



## UZOEFU MIAKA 18

Darasa la mjasiriamali maembe, mboga za majani zinazokaushwa

Ukurasa 14

UCHUMI



# BUFE

Ijumaa Februari 28, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

## Mashimo yalipochimbwa saruji yalivyogeuzwa hifadhi ya kitalii

Ukurasa 19

# MZEE MASELE; MWASISI ANAYEIJUA USHIRIKA NYANZA 'KICHWA NYAYO' TANGU MZIZI WA 1955



Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

BIASHARA

UZOEFU MIAKA 18

# Darasa la mjasiriamali maembe, mboga za majani zinazokaushwa

**Na Beatrice Shayo**

- ‘Alibipu’ soko Ujerumani, tenda kibao
- Bidhaa zake miezi tisa bado ziko safi



Bidhaa zake zilizokaushwa ndani ya vifungashio.

Iara Ibihya, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Claphijo Enterprises.

“HAIKUWA rahisi. Nimeandaa bidhaa zangu kwenda kuziuza katika onyesho moja la mkoa wa Mbeya, sitaweza kuisahau hii. Siku niliendia na mboga zangu nimezikausha vizuri nikaziweka, watu walikuwa wanapita utadhani wananiwekea heshima ya mwisho.”

Ni maneno ya Iara Ibihya, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Claphijo Enterprises, inayohusika na usindikaji mboga na matunda kwa kuaushio la mionzi ya jua.

Ibihya ambaye ni maarufu kwa jina Claphijo, anasema hakukata tamaa, aliendelea kutafuta masoko na kujenga uhusiano mzuri uliosaidia kujulikana hadi nje ya nchi.

“Sikukata tama, kwa sababu Mbeya hawana tabia ya kukausha mboga, hali ya hewa yao ni nzuri wakati wote, wana mboga ‘freshi’ nikajipa moyo wakati ule,” anasimulia Claphijo.

Anasema licha ya sasa amepiga hatua katika shughuli zake za ujasiriamali ndani na nje ya nchi, hata kupata tuzo mbalimbali bado hafahamiki.

“Ifike wakati sisi wajasiriamali ambao tunafanya vizuri ikafahamika umepiga hatua fulani, basi hapa nyumbani tutambuliwe kama wanavyotambuka wenzetu.

“Hivi kwa mfano nilivyoshinda mshindi wa jumla tuzo ya ‘Mwanamke Mjasiriamali Tanzania’ na ‘Mwanamke Bora Katika Ujasiriamali’ zilizotolewa na Sekta Binafsi nchini (TPSF) ningekuwa nimeshinda mashindano ya urembo si ningejulikana?,” anahoji .

““Tunapozungumzia Tanzania ya Viwanda, ukaushaji ni njia mojawapo kwamba wangeiangalia kila halmashauri wakatengeneza jengo linalokidhi viwango vinavyotakiwa, halafu wajasiriamali wakafanya usindikaji,” anasema.

Anaeleza kuwa upo ubunifu mkubwa ambao wanaufanya ingawa serikali haijatoa kipaumbe cha kuwatambua ama kuwapa motisha licha ya mkakati wa nchi ni kufikia uchumi wa viwanda.

“Kuna maonyesho yalifanyika nje ya nchi nilialikwa kuiwakilisha Tanzania katika masuala ya ujasiriamali kufika pale nilimuona waziri wa kilimo nilikwenda kumsalimia hakunipatia ushirikiano jambo ambalo lilinishangaza nikajisikia vibaya kwa nini hata nilikwenda kumsalimia,” anasema.

Aliongezea kuwa “Waanze kubadilisha vipaumbele wenzetu wanashinda wanapelekwa hadi bungeni sisi tunaishia nyumbani na tuzo zetu tutafahamika lini katika hizi kazi zetu,” anasema

**IKOJE BIASHARA?**

Claphijo anazungumzia biashara yake ya usindikaji mboga na matunda, kwamba alianza nayo mwaka 2002, bada aya kugundua kuwapo mazao mengi wakati wa mavuno.

‘Kipindi cha maembe, mananasi yanakuwa mengi hata mboga zinakuwa nyingi. Inapofika wakati wa jua kali hivi vyote havipatikani na mkulima anakata tamaa. Hii inasababisha vijana kukimbia kilimo baada ya kuona hakilipi,” anasema

Anasema alipokuwa mtoto alimsaidia mama yake kukausha mboga na viazi na ndipo wazo lake lilipoanza na kuamua kwenda Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (Sido) kujifunza kukausha kitaalamu na kutafuta makaushio.

Claphijo anasema tangu alipoanza, kuna mafanikio ya kiwango kikubwa, wateja wakivutiwa na mboga, pia matunda yaliyokaushwa na haikuwa rahisi sana kwa upande wa mboga, kadri muda ulivyoenda wakaanza kuzielewa na kuzipenda.

“Soko langu lipo ndani na nje ya nchi. Wajasiriliamali wengi wanalia hakuna masoko, lakini kwa matunda yaliyokaushwa soko halitoshelezeki,” anasema

Mzalishaji huyo anasema, kila alipokuwa akisikia maonyesho alijitahidi kuhudhuria na kuonyesha bidhaa zake, huku akiendelea kutafuta mtandao wa masoko.

“Nikaja na wazo jingine, kwa nini shule za watoto wetu wanakula maharage kuanzia Januari hadi Desemba au mama anatoka kazini aje kutafuta kisamvu akatwange, anatumia muda nikaona hapa kuna soko,” anasema

Mbunifu huyo mama wa watoto watatu, anasema baadaye akajielekeza katika fursa nyingine za mtu kupata maembe ya kukausha hata kama sio msimu wake

Anaeleza kuwa soko la bidhaa hizo lipo, japo wajasiriamali wenzake wanaliona ni gumu lakini mwenyewe analitetea kwamba muhimu ni kuzingatia viwango vinavyotakiwa katika usindikaji.

> **“Nikaja na wazo jingine, kwa nini shule za watoto wetu wanakula maharage kuanzia Januari hadi Desemba au mama anatoka kazini aje kutafuta kisamvu akatwange, anatumia muda nikaona hapa kuna soko,” anasema**

Claphijo anasema, mwaka 2013 aliende nchini Ujerumani kwenye maonyesho akiwa na bidhaa ya maembe ya kukausha na waliipenda mno bidhaa hiyo, wakanunua na kumpa tenda ya kupeleka bidhaa huko.

**STAILI ANAYOKAUSHIA**

Anasema, ratiba yaje ya kawaida huwa anaamka mapema na kuandaa bidhaa zake kwa ajili ya kuweka katika kaushio la mionzi na inapofika majira ya saa 12 anaanza kuziweka.

Mama Clahijo anaismulia Nipashe, kwamba kabla ya kuweka bidhaa, ni lazima kaushio la mionzi litegeshewe upande upepo unakotoka na kinachofanya kazi ya kukausha hapo ni hewa ya joto, kitaalamu ‘hot air’ inayotoka nje.

“Kitendo cha hewa ya moto kuingia na kutoka, ndipo bidhaa inavyokauka. Inaweza kutumia siku

INAENDELEA UK. 15

# Darasa la mjasiriamali maembe, mboga za majani zinazokaushwa

INATOKA UK. 14

mbiili hadi tatu na bidhaa ina uwezo wa kukaa hadi miezi tisa bila ya kuharibika," anasema CIaphija.

Anaongezeza: "Kama utakosea kutegesha kaushio lako bidhaa badala ya kukausha itajikuta inajipika hapa inahitajika utaalamu. Hata nyama inakauka vizuri. Unaikata kama slesi unaiweka na viungo inakauka vizuri.

"Nyanja ninazikausha, siku ukitaka kuitumia unaweka maji kwa muda wa dakika 10 ili irudi katika hali yake. Hata hizi mboga, utaziloweka katika maji kwa muda ili irudi katika hali yake."

Anasema unapofanyika ukaushaji wa bidhaa hizo, lengo ni kuondoa maji, hivyo mtu unapohitaji kutumia bidhaa hizo, kuna maelekezo ya muda yanayowekwa katika vifungashio ili mteja kutafuata, pindi anapohitaji kutumia bidhaa hizo.

"Kisamvu unakiloweka usiku na mchicha ni dakika 10 sasa unakuta watu wengine hawasomi maelekezo anakuja kukuambia nimechemsha muda mrefu hakijaiva. Kisamvu fuata maelekezo niliyoyaweka katika vifungashio, wengi ni wavivu katika kusoma," anasema.

**VITAMINI ZINAPATIKANA**

Mtaaluma huyo anasema, bidhaa zake ameshawashirikisha wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Anasema, walifanya utafiti kwa ajili ya kuhakikisha vitamini zote zinapatikana na kuongeza:"Hata vifungashio navyovitumia, vimetengenezwa kwa ajili ya bidhaa zilizokaushwa."

**CHANGAMOTO**

Anasema kwa sasa amesimamisha uzalishaji, kutokana na kubomolewa eneo alilokuwa ameweka kaushio la mionzi ya jua, ili kupisha ujenzi wa barabara.

Ni Kifaa kililokuwa na uwezo wa kusindika nusu tani kwa wakati mmoja na kwa sasa anatafuta eneo mbadala, ili aweze kuendelea na shughuli zake za usindikaji kama ilivyokuwa awali.

"Kwa kuwa nimepata changamoto ya kupata eneo la kuweka hili kaushio langu ... bado naendelea kutafuta lakini kwa sasa nimejikita katika kutoa mafunzo pamoja na kutengeneza makaushio," anasema

CIaphija anasema, changamoto kubwa anayokutana nayo ni kwamba kaushio la mionzi ya jua linategemea jua linapokosekana uzalishaji unasimama.

"Unaweza kuamka asubuhi, unawahi kuweka bidhaa zako katika mashine ghafla mvua imekuja inanilazimu kuwa na mbadala, yaani kama nimeweka matunda itabidi niyatoe nikatengeneze juisi kama ni matunda aina ya nanasi nitatengeneza 'jam' nzuri ukiwa 'food processer' unakuwa mbunifu," anasema.

"Kwa sasa hivi sifanyi usindikaji, lakini siwezi kufa njaa. Natengeneza pilipili zenye ladha ya ukwaju, karoti, mbilimbi. Nikieenda nazo kanisani zinakwisha hata hapa nyumbani nauza.

"Pia, natengeneza 'chili oil' (mafuta ya pilipili) kutoka Rwanda huyu, jamaa nilikuwa nakutana naye katika maonyesho, nikajaribu kumuomba anifundishe anakataa nikasema sikubali, nikajifunza mara ya kwanza hadi mara ya tatu nikajua," anasema.

Anachojivunia ni ameweza kutoa elimu kwa wajasiriamali, kutengeneza makaushio ya usindikaji na kutengeneza mtandao wa soko katika nchi mbalimbali.



Kifaa kinachotumika kukausha mboga na matunda. PICHA: ZOTE BEATRICE SHAYO.



Vipepeo kwa ajili ya kuuzwa. **PICHA: MTANDAO.**

# Biashara ya vipepeo inavyoneemeka Kenya

**Kilifi, Kenya**

PATA simulizi ya biashara ya vipepeo katika Kaunti ya Kilifi, Pwani ya Kenya, ambako kwa muda mrefu sasa wamejikidhi kimaisha kupitia biashara hiyo ya vipepeo.

Mfanyabiashara mzoefu, Charo Ngumbao, anasema wao hushika vipepeo wa kike, lakini kuna kipepeo wa kiume wanaowapa mapato mazuri zaidi.

Mbali na mapato, kipepeo huyo ni kipenzi cha wale wa kike ambao hutamani kumfuata kwa wingi kutokana na uzuri wake na madaha aliyonayo.

Ngumbao anakiri kipepeo huyo huwapatia kipato cha juu zaidi katika biashara yao ana anafafanua: ``Huyo kipepeo tunamuita 'Dhahabu ya Arabuko'... anapepea kwa madaha, maana yake anajua yeye ndiye dume anayependwa zaidi na vipepeo wa kike katika msitu wa Arabuko Sokoke.

"Sokoni zile pupa zake zinang'ang'aniwa sana, zaweza kupata dola mbili na nusu ama tatu kwenda juu (Sh. 6,600 hadi 8,800),'' anasema Ngumbao mwenye uzoefu wa miaka 20 sasa.

Ngumbao anaeleza jinsi biashara hiyo ilivyobadilisha maisha yake akisema:``Ukweli ni kwamba ni biashara nzuri sana, watoto wangu wamesoma na ni biashara ambayo haina hasara kubwa kuiendeleza.

"Nilikuwa mharibifu wa msitu kwa ukataji wa miti, lakini nilipoanza biashara hii nimeona mabadiliko makubwa. Napata kati ya shilingi za Kenya elfu ishirini hadi arobaini kwa mwezi. Kuna wengine hata wamenunua mashamba kwa mapato haya ya vipepeo.

``Tuna njia mbili za kushika hawa vipepeo. Kwanza kuna ile ya mtego na nyingine ya neti. Katika hiyo ya mtego, tunaweka tembo la mnazi tumechanganya na ndizi. Waweza nasa vipepeo kama hamsini, wakulima tunachagua wale unawahitaji.

"Zaidi huwa tunaangalia wale wa kike kisha hao wengine tunawarudisha waendelee kuzaana. Tunawapeleka nyumbani tunawaweka kwenye banda zao tumejenga wanaendelea kuzaa halafu tunapeleka sokoni kuuza zile pupa.''

Makavasi ya Gede ndilo soko kubwa la wafanyabiashara hao wa vipepeo.

Naibu Msimamizi wa Makazi hayo, Mathias Ngonyo, anasimulia zaidi:``Hapa huwa wakulima wanaleta pupa ama vizeruzeru. Wana viongozi wao huleta hizo pupa. Kwanza tunavikagua tuone kwamba viko hali nzuri kisha tunaziweka kwa maboksi halafu tunazipeleka uwanja wa ndege kusafirishwa kwa wateja wetu huko Uingereza na Uturuki ambazo ndizo soko zetu kubwa.''

Wafanyabiashara wanakiri biashara hii imewasaidia sana kiuchumi na kuendesha maisha ya kila siku.

**BBC**

BIASHARA

MZEE MASELE;

# Mwasisi anayeijua Ushirika Nyanza ‘kichwa nyayo’ tangu mzizi wa 1955

- Jukumu la JPM; Kairejeshea mali zote
- Karani mpimaji 1960, aliyestaafu ‘GM’
- Alia soko huria limeua ubora pamba

**Na Anthony Gervas,Mwanza.**

USHIRIKA ni damu ya ushindi wa uchumi kwa mzalishaji myonge. Mzizi wa ushirika unazama mbalimbali sana hata kugusa mustakabali wa ukombozi wa kisiasa.

Katika historia ya muda mrefu nyenzo hiyo iliyotumiwa na ukokoloni na kufanikisha uzalishaji na kisha ikatumwa vinginevyo, katika manufaa ya mavuno sokoni.

Ni ushirika uliokutanisha watu, kuwaunganisha na kufungua mlango mpya wa umma kujikomboa, zikiwamo harakati za Mwalimu Julius Nyerere, kuleta uhuru wa nchi.

Hapo ndipo inakuja simulizi zenye umri wa miaka 65 sasa. Hapo katika Ukanda wa Ziwa, kulikuwapo kilichojulikana chama cha ushirika imara kilichowahi kutamba sana; Victoria Federation of Cooperative Union Limited (V.F.C.U).

Kimsingi, ulikuwa Muungano wa Vyama vya Ushirika Kanda ya Ziwa, vilivyokuwa vimeundwa kutoka katika mikoa mitatu ya sasa; Mwanza,Shinyanga na Mara.

Historia inayoanza kudokezwa na mmoja wa magwiji waasisi, Mzee Enock Masele (80), anataja siku kamili ya kuasisiwa ni mwaka 1955, chini ya usukani wa kwanza mwasisi, marehemu Paul Bomani, ambaye ana mengi katika historia ya kutumikia serikali nchini, ikiwamo Baraza la Mawaziri.

Ni katika zama harakati za siasa chama cha TANU zikiwa na umri wa mwaka mmoja, Mwalimu Nyerere, alijitahidi kupenyeza propaganda za kudai uhuru wa wananchi, ikiwamo kupitia vikundi kama vyama vya ushirika.

Pia, ni mwaka huo huo ambao Rashid Kawawa alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Shiriksho la Wafanyakazi Tanganyika (TFL) na kutikisa serikali ya kikoloni kwa mengi baadaye, hata akamshawishi Mwalimu Nyerere kuingia naye katika ubia wa kisiasa,

Mzee Masele anasimulia kwamba, Bomani baada ya kuanzisha vyama hivyo, alifanya kazi na Mwenyekiti wake, Mustafa Mabenga, aliyetoka wilaya ya Ukerewe, aliyetumikia tangu 1955 akiwa mwenyekiti hadi 1959. Bomani alikuwa Meneja Mkuu wa vyama hivyo.

Anasema, mwaka 1960, Meneja Mkuu Bomani, alistaafu na nafasi hiyo akamuachia ndugu yake Emmanuel Bomani, aliyefanya kazi kuanzia 1960 hadi 1968,naye akastaafu.

Mzee Enock Masele anasimulia zaidi kwamba, muungano huo ulikuwa ni wa vyama vya ushirika vya wakulima wa zao la pamba Kanda ya Ziwa katika mikoa hiyo.

Mzee Masele anasimulia kwamba, kabla ya V.F.C.U kuanzisha baadhi ya viwanda vya kuchambua pamba maarufu kama ‘ginery’ vilimilikiwa na jamii ya Wahindi, anavyoviita kwa majina; Nassa, Buchosa, Nyamililo, Nyambiti,Ukerewe na cha Magu, kilichoitwa Gwiging’holo bageni.

“Wahindi hao waliondoka baada ya wakulima kugoma kuwauzia pamba yao kutokana na manyanyaso waliokuwa wakiyapata wakati wa kuuza pamba yao, ndipo walipoamua kuanzishwa kwa muungano huo wa mikoa mitatu ya wakulima wa pamba na kuunda (V.F.C.U)



Jengo la Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza Cooperative Union Limited (1984), ambalo zamani lilikuwa makao makuu ya Muungano wa Vyama vya Ushirika vya Wakulima wa Pamba, katika mikoa ya Mwanza,Shinyanga na Mara. PICHA **ZOTE: ANTHONY GERVAS**



Kiwanda cha kuchakata pamba cha Nasa ilipokuwa mkoani Mwanza (sasa Geita), kikiwa katika hali mbaya.**PICHA: MTANDAO.**

> **“Wahindi hao walipewa majina mengi na wakulima; mabepari, makabaila, kupe na wanyonyaji. Baada ya kuchoshwa na manyanyaso hayo, ndipo viwanda hivyo walivyoondoka vilirejeshwa katika ushirika wao uliokuwa umeanzishwa na wakulima chini ya mwasisi marehemu Paul Bomani 1955,”anasema**

“Wahindi hao walipewa majina mengi na wakulima; mabepari, makabaila, kupe na wanyonyaji. Baada ya kuchoshwa na manyanyaso hayo, ndipo viwanda hivyo walivyoondoka vilirejeshwa katika ushirika wao uliokuwa umeanzishwa na wakulima chini ya mwasisi marehemu Paul Bomani 1955,”anasema


Mzee Enock Masele, mwasisi wa Victoria Federetion Union Limited na Meneja mstaafu wa Nyanza Cooperative Union Limited (1984), akiwa nyumbani kwake, jijini Mwanza.

**ALIVYOJIUNGA**

Mzee Masele anasimulia mwaka 1960, alianza kazi alipoajiriwa,katika nafasi ya Karani wa Kupima Pamba Vijijini, inayotoka katika vyama vya msingi katika Kiwanda cha Kuchambua Pamba wilayani Magu - Gwaging’holo bageni, yenye maana “kateni tamaa wageni.’

Anasema kuwa baadaye, alipandishwa daraja hata akawa Mhasibu Msaidizi, chini ya Meneja osmas Chenyenge na mwaka 1966 akawa Mhasibu Mkuu wa Victoria Federetion of Union Limited.

**USHIRIKA WAVUNJWA**

Masele anafafanua kuwa mwaka 1967 (VFCU), ushirika ulioasisiwa mwaka 1955 ulivunjwa na kuanzishwa Nyanza Co-operative Union Ltd, mwaka 1968.

Anasema Tume ya Kusimamia Wafanyakazi wa Ushirika Tanzania, ilimhamishia katika Kanda ya Manawa (Ginery) ya wilayani Kwimba, alikoendelea kuwa Mhasibu hadi mwaka 1971 na baadaye alirudishwa makao makuu, mjini Mwanza.

Mwasisi huyo ambaye ni mahiri wa kumbukumbu zake, anasema baadaye alikwenda kusoma katika Chuo cha Ushirika Moshi (The Cooperative College Moshi) ambako alihitimu mwaka 1973 na kurudi tena makao makuu mjini Mwanza.

Anasema, elimu hiyo ilimfanya akwee na kupanda zaidi katika nafasi ya Meneja Msaidizi na mwaka 1974 alirudishwa masomoni tena alikopata Diploma ya Uongozi wa Ushirika aliyohitimu mwaka 1976.

Mzee Masele anasema, wakati huo anarejea kutoka masomoni, alikuta mabadiliko makubwa, kuwa vyama vya ushirika vilivunjwa na mali zote zikakabidhiwa katika Bodi ya Pamba, ambacho kilikuwa chombo cha serikali kinachosimamia zao la pamba kwa wakulima nchini.

Anasema mwaka 1977 alipelekwa kuwa Meneja wa Kanda ya Buyagu hadi mwaka 1978 mwishoni aliporudishwa tena katika makao makuu ya Mamlaka ya Pamba, akiwa Meneja Msimamizi.

**YAZALIWA NYANZA**

Mzee Masele anasema mwaka 1984 ndipo serikali iliagiza mali zote kurudishwa na kukabidhiwa katika vyama vya ushirika.

Ni katika kipindi hicho kukatokea mabadiliko ya kila mkoa unajitegemea kwa shughuli zake za ushirika, Mwanza, ikawa na Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (Nyanza Co-operative Union Ltd 1984 -NCU) na Shinyanga Shirecu, vivyo hivyo Mara.

Anasema tangu mwaka huo 1984, aliajiriwa kama Meneja Shughuli (Operation Manager) katika makao makuu Mwanza, akisimamia ununuzi, usafirishaji, ugawaji fedha za kununua pamba za wakulima vijijini.

“Mwaka 1987 ulitokea mtikisiko ndani ya ushirika NCU na kusababisha wakuu wote wa idara kuachishwa kazi...Meneja Mkuu aliyekuwa ni Andrew Mashamba,” anasimulia.

Mzee Masele anaendelea: “Ndipo mimi nikapewa kuwa Kaimu Meneja Mkuu hadi mwaka 1988 na 1989 nikathibitishwa kuwa Meneja Mkuu hadi nilipostafu mwaka 1999,baada ya kutimiza miaka 60 kazini,” anasema.

Anasema fursa alizowahi kuzipata kwenda nchi za ulaya kutokana ufanyakazi bora wake ndani ya ushirika ni pamoja na kwenda nchini

Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Uturuki, India na Singapore kwa ajili ya kutafuta soko la kuuzia pamba katika kampuni za ulaya.

**PAMBA SOKONI**

“Pamba ya Tanzania katika soko la dunia hasa Ulaya, waliipenda sana kwa sababu ilikuwa ikivunwa kwa madaraja na kuuzwa. Kulikuwa na Daraja A na B. Daraja A ilikuwa pamba safi na nyeupe iliyokuwa ikivunwa na wakulima kwa kutumia mikono na kuchambuliwa na Daraja B ilikuwa ni pamba chafu(Fifi),” anafafanua.

Mzee Masele anaendelea na simulizi ya soko kwamba, pamba safi iliuzwa kwa bei kubwa katika soko la dunia, tofauti na iliyokuwa ikivunwa katika nchi zingine.

Anasifu kwamba pamba ya nchini ilikuwa na kiwango bora zaidi kuliko kwingineko walikochambua kwa kutumia mashine na hawakuwa na kiwango cha ubora kufikia nchini.

Kwa mujibu wa Mzee Masele, wakati pamba nyingi za soko la kigeni ilikuwa inakatika nyuzi zake, kutoka Tanzania ilikuwa na kiwango cha juu mno.

Analaumu mzizi wa kuingia soko huria katika mfumo wa uuzaji pamba, ndio umechangia kuharibu ubora na sheria na kanuni za utunzaji madaraja aliyoyataja.

“Soko huria lilipoingia tu tayari sheria na taratibu za madaraja hazikufuatwa. Pamba haikuchambuliwa tena na wakulima, nyeupe ilichanganywa na ile chafu nyekundu(fifi).

“Hapo ndipo bei ya pamba Tanzania katika soko la dunia lilipokufa, kwa sababu wanunuzi wake soko la dunia hawakuipenda tena,” anasema Mzee Masele.

Analalamika kuwa ndio zama ambazo ubabaishaji ukavamia soko huria, kuwapo wanunuzi walioweka uchafu kama mchanga, maji, mawe na mafuta kuongeza uzani, jambo linaloharibu ubora wa pamba, ikiwemo kuozesha mbegu zake.

Mageuzi ya mfumo huria katika uchumi wa nchi yaliingia mwaka 1985, na sehemu kubwa ya utekelezaji wake kisera na kisheria, ni baada ya kufanyiwa maboresho yaliyotekelezwa zaidi kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa 1990.

**MALI ZA NYANZA**

Licha ya kustaafu, ana mengi kuhusu maendeleo ya Ushirika Nyanza, anasema akiwa katika miaka 17 ya maisha ya ustaafu, alijikuta anapata salamu kutoka uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, akimhitaji.

**Kulikoni tena?**

Ni mwaka 2016, alipoteuliwa kuwa kati ya watu sita, akivalishwa kofia ya Mwenyekiti wa Bodi ya Urejeshaji Mali za Nyanza Co-operative Union Ltd, zilizouzwa, akisema alifanya kasi hiyo hadi mwaka 2018 na kufanikiwa kuzirejesha mali zote.

Anazitaja mali zilizorejeshwa kutoka Chama Kikuu cha Ushirika (1984) NCU, ni pamoja na Kiwanda cha Kukamua Mafuta ya Kula (Nywela), nyumba tatu za kuishi wafanyakazi wake zilizoko Isamilo jijini Mwanza, ghala la kutunzia mali za ushirika lililopo Igogo.

Zingine kwa mujibu wa Mzee Masele, ni ofisi ya kampuni ya usafiri Kauma iliyokuwa na gereji pamoja na kituo cha mafuta, kiwanda cha Oil Mill cha Shoki, kilichouzwa na kutumika kuchakata minofu ya samaki sangara.

• ***Soma zaidi makala ya Ushirika Uk.18.***

• ***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na ,simu: (+225)0682 86 92 44,Kanda ya Ziwa.***

## BIASHARA KATIKA PICHA


Wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wakifanyia shughuli zao katikati ya barabara za mitaa ya eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, na kusababisha usumbufu kwa watembea kwa miguu. **PICHA: JUMANNE JUMA**


Mchuuzi wa matunda akitafuta wateja katika eneo la Mji Mpya, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**


Mchuuzi wa matunda ya aina mbalimbali katika Manispaa ya Moshi, Maisara Msechu (kulia), akimhudumia mteja wake, katika eneo la makutano ya barabara kuu katika manispaa hiyo, mapema wiki hii. **PICHA: JAMES LANKA**

BIASHARA

# Ushirika Kahama unavyopigana kuibuka kupitia tumbaku, pamba

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KATIKA ufuatiliaji wa safari ya ushirika nchini kihistoria, daima kuna nafasi ya kuhusisha majina ya Chama cha Ushirika Shinyanga (SHIRECU) na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Mwanza (Nyanza), hapo ukitaja mikoa ya Kanda ya Ziwa na hiyo ina asili ya kuwa chama kimoja, wakiwa wadau wakuu wa walima pamba.

Pia, kuna magwiji wengine wa ushirika kitaifa, kama vile Chama cha Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro (KNCU), vivyo hivyo cha mkoani Kagera, wao wakibobea zaidi katika zao la kahawa.

Mikoa ya Kusini Lindi na Mtwara, kulikuwapo kwa walima korosho na Tabora kupitia, ikilishika zao la Tumbaku.

Kwa sasa vyama vingi vya ushirika havipo imara na hata baadhi ya mali zake kutoweka. Migogoro mingi iliyotokea, inatajwa kuwa na mzizi wa msuguano binafsi na kuwafanya wakulima wahangaike, badala ya kufanya kazi ya kutetea maslahi ya wakulima.

Serikali kimsingi, imeliona hilo na iko katika jitahidi za kurudisha uhai wa ushirika kama ilivyokuwa awali, ili kumuondolea mkulima kero na afanikshe jitihada zake.

Tayari inaelezwa kuwa, viongozi wengi waliokuwa wabadhirifu wa mali za wakulima wameondolewa.

Katika Chama cha Ushirika Wilaya ya Kahama (KACU), kwa sasa kimekuwa chombo kilicho mstari wa mbele kumsimamia mkulima wa pamba na tumbaku, pia kumdhamini katika mikopo kama vile ya mbolea na mbegu zinazotolewa na baadhi ya kampuni.

Kuna baadhi ya kampuni zimefika wilayani Kahama kutoa mikopo ya Mbolea kwa wakulima wa Tumbaku, kupitia udhamini wa KACU, hata wakulima wameongeza kiwango cha uzalishaji shambani.

**KINACHOHITAJIKA**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anasema serikali kwa sasa imedhamiria kuhakikisha ushirika wa zamani unarejeshwa, ikiwamo baadhi ya mali zake kama vile kufua viwanda vyake vilivyokufa, kumhakikishia mkulima uwezo wa kulima mazao ana anajua mahali pa kuuza ushirika, pasipo kudhulumiwa.

Anataja baadhi ya viwanda vinavyohitaji kufufuliwa na serikali inaendelea kurudisha mali nyinginezo.

Dk. Titus Kamani, Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, anasema nchi zote duniani zilizoendelea kiuchumi, wakulima wake wamejiunga kwenye vyama vya msingi na ushirika na kuziuza kwa bei nzuri, kulingana na soko la dunia lililopo wakati huo.

Hata hivyo, anaeleza masikitiko yake kwa baadhi ya vyama vya msingi wilayani Mbongwe na Masumbwe, kutojiunga na Chama Kikuu cha Ushirika - Mbogwe na Msumbwe (MBCU), kwa madai ya kushindwa kununua hisa.

Anasema, kati ya vyama vya msingi 89 vilivyopo Wilayani Mbogwe na Msumbwe, ni 54 pekee ndio vilivyojiunga na chama kikuu hicho, wakati vingine 35 vinajiendesha vikiwa huru.

"Mnapokuwa nje ya ushirika mnauza mazao yenu kwa bei ambayo haiendani na thamani ya mazao yenu. Wenzenu Rombo wamejiunga wote kwenye ushirika, wanauza mazao yao kwa bei nzuri na kila mwaka wanagawana gawio, kwanini ninyi mko matabaka?" anahoji Dk. Kamani

"Mnapokuwa kwenye ushirika, mnaweza kuagiza pembejeo za kilimo na kuzigawa kwa wakulima kwa wakati na anakuwa na uhakika wa masoko. Nawataka waache kuingiza siasa kwenye ushirika," anasema.

Pia, katika mustakabali huo, anamtaka Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika MBCU, Benedictor Bulugu, kutoa elimu muhimu ya ushirika kwa vyama vya msingi vyote vilivyopo Mbogwe na Masumbwe, ili wajiunge na ushirika kupata mwelekeo mzuri wa soko la tumbaku na pamba.

Dk. Kamani ana ushauri kwamba, kuanzisha chama cha kukopeshana (saccos) ndani ya ushirika, ambao wakulima watakopa fedha za kununua pembejeo za kilimo wakati zitakapochelewa na kuacha kuweka mazao yao rehani kwenye tasisi za kifedha.

**HALI HALISI**

Martha Mkupasi ni Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, mkoani Geita, anayeahidi atahakikisha vyama vya msingi visivyojiunga na ushirika mkuu, vinajiunga akivitetea vilishindwa kujiunga kutokana na changamoto zilizokuwapo kwenye msimu wa zao la pamba uliopita.

Anaeleza, katika msimu uliopita wakulima wa zao la pamba, hawakulipwa fedha zao ipasavyo, licha ya kuingizwa kwenye akaunti za vyama mama (amcos) na viongozi walizitmia tofauti na hata walipowabana, walizirejesha na zikafikishwa kwa wakulima.

Mkazi, Catherine Agostino, anasema baada ya kampuni ya ununuzi wa zao la tumbaku TLTC kuondoka, vyama vitatu vya msingi vimekosa wanunuzi wa uhakika wa zao hilo, licha ya kulima tumbaku msimu huu.

Catherine, anavitaja vyama hivyo kuwa; Mzalendo, Kazibizyo, Idoselo Mwalo na Namsingili, ambavyo vimeshindwa kukopesheka na benki, kwani hazina kampuni wadhamini iliyoingia nazo mkataba, pia hazina ofisi wilayani Mbogwe au Masumbwe.



. Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dk, Titus Kamani akizungumza na wakulima wa Tumbaku na pamba kutoka Chama Kikuu cha Ushirika ya Mbonge na Bukombe (MBCU). **PICHA: SHABAN NJIA,**

**WANUNUZI WAOKOA**

Ally Hamisi, ni Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Ngokolo, anaipongeza kampuni ya Petrobena kwa kusambaza pembejeo kwa wakulima na kununua tumbaku jumla ya kilo 250,000 katika mwaka wa uzalishaji uliopo 2019/20.

Anasema, awali walima tumbaku walishakata tamaa kuendelea kulima zao hilo, baada ya kuona tumbaku zinazozalishwa nje ya kilimo cha mkataba zinakosa soko na wakataka kujikita kwenye pamba.

Hamisi anasema Chama cha Msingi Ngokolo kina wanachama hai 295, ambao baada ya kampuni kupanga kununua tumbaku kilo 250,000, wakulima hao wakiwa wamelima zaidi ya hekta 220 za tumbaku kwa ajili ya msimu ujao, iliwakatisha tamaa.

"Walipoteza imani ya kuendelea kulima tumbaku baada ya tumbaku iliyozidi kwenye mikataba yao kukosa masoko na kutishia kukimbilia kwenye kilimo cha pamba....sasa tumepata kampuni ya petrobena imerudisha imani ya wakulima na kujitokeza kwa wingi kulima tena," anasema Hamisi.

Pia anfafanua kuwa, aliomba uongozi wa kampuni hiyo kukiruhusu chama hicho kuongeza uzalishaji, hivyo katika msimu ujao wanatarajia kuzalisha kilo zaidi zitakazokuwa na ubora unaohitajika kwenye soko la dunia.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilayani Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, anaipongeza kampuni kwa kusambaza pembejeo kwa wakulima na wakifuata kalenda tena kwa bei ya chini itakayompa faida mkulima.

Charahani anautaka uongozi wa kampuni, kuelekea katika maeneo mengine kununua na kugawa pembejeo kwa wakulima akitaja kuwa Chunya, Kigoma, Mpanda na Serengeti, ambako wana changamoto ya ukosefu wa kampuni ya ununuzi wa zao hilo.

Pia, anawataka wakulima wa Shinyanga, kuendelea kulima tumbaku bora, ili kampuni ziendelee kujitokeza kwa wingi kununua tumbaku, na anaongeza kwamba zinapojitokeza kampuni nyingi, ndivyo mkulima anavyozidi kufaidika.

Charahani anasema, Kahama ina zaidi ya wakulima 8,900 kutoka katika vyama vya msingi 48, vinavyoweza kulima na kuuza tumbaku yenye thamani ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 13 (Sh. Bilioni 28.6) kwa msimu uliopita.



Viongozi wa vyama vya msingi na Mkaguzi wa Tumbaku Wilaya Kahama na Mkurugenzi wa kampuni ya Petrobena, Peter Kumalilwa, wakikagua shamba la mkulima wa tumbaku la uoteshaji zao hilo.

BIASHARA

# Mashimo yalipochimbwa saruji yalivyogeuzwa hifadhi ya kitalii

- Wanyama wa ajabu, kihistoria
- Kiwanda saruji nacho pale pale
- Miaka 68 imechimba tani mil. 25

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa Mombasa**

MAENEO mengi yanayotumika kuchimba malighafi ya viwanda vya saruji, hubaki bila ya kuendelezwa na kuwa mapango au sehemu zisizo salama, kwa kugeuka maficho ya wahalifu na mazalia ya mbu.

Kuna sehemu zingine zinazochimbwa kokoto, mchanga au madini, nayo hubaki mahandaki makubwa na uozefu unaonyesha hakuna utaratibu wa kuparejeshea uoto wake wa awali.

Kama ilivyo kawaida kwenye maeneo mengi nchini, baada ya kumaliza kuchimba malighafi za viwanda, maeneo hayo yanaachwa yameharibika, pasipo kuendelezwa na matokeo yake, watu wanabaki na maono kwamba viwanda ni tishio kwa ustawi wa mazingira.



Ndivyo ilivyo mbwembwe za kitalii, hifadhini Bamburi.

### DARASA KENYA

Bamburi Haller Park, iliyopo Mombasa, ilizaliwa kutokana na kiwanda cha saruji kilichoanzishwa mwaka 1952, uzalishaji wake ulifika tani milioni 25, kiasi cha kufanya eneo hilo kuharibika.

Hapo ndipo kiwanda hicho cha Saruji Bamburi, kikaamua kurejesha uoto kwenye eneo la hekta 300.

Leo hii, hifadhi hiyo iko umbali wa mita chache tu kutoka kilipo kiwanda na lango kuu la kuingilia limepakana na lango la kiwanda, huku barabara kuu ya Kilifi hadi Malindi, ikipita jirani na hifadhi hiyo.

Aidha, upande wa barabara kuu, kumejengwa ukuta mkubwa wa mawe kuzuia watu wanaoingia ovyo au wanyama kutoka.

Mtu anapoingia katika lango la barabara kuu, anateremka wastani wa mita 800 kutoka usawa wa bahari.

Uwepo wa kiwanda hicho, ndiyo umewezesha mji mdogo wa Bamburi kukua na sasa ni moja ya mji maarufu katika Pwani ya Mombasa. Pamekuwa, eneo la utalii kwa watu mbalimbali na upande wa pili wa barabara, kuna hoteli za kitalii.

### MAGEUZI YALIKOANZIA

Uongozi wa kiwanda hicho ulimteua Rene Haller kuwa Meneja wa Bustani hiyo mwaka 1970. Hapo alifanya kazi kubwa ya kutafuta miti itakayoweza kumea kwenye ardhi ya chokaa. Kati ya aina 26 zilizopandwa, ni tatu pekee zilimea, ikiwamo minazi.

Wanahabari kutoka nchi za Afrika, walikutana mjini Mombasa kwa mafunzo maalum ya namna ya kuandika habari zinazozuia majanga.

Hiyo ni chini ya uratibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa Kupunguza Majanga (UNDRR) kwa kushirikiana na Mtandao wa Waandishi wa Habari za Majanga Afrika (Daraj), mfadhili akiwa Jumuiya ya Ulaya kwa masuala ya Afrika (ACP).

Wanahabari hao 30 walitembelea hifadhi hiyo kujifunza namna maeneo yaliyoharibiwa kwa kuchimbwa malighafi, yalirejeshewa uhalisia wake.

Kiongozi wa Watalii wa Bamburi, Karima Nyinge, anasema baada ya kuchimbwa kwa malighafi hiyo, eneo hilo lilibaki kuwa jangwa na ndipo walipoamua kutunza mazingira.

Kazi kubwa iliyofanywa na Haller, aliyehakikisha anarejesha uoto kwa kupanda miti mingi kiasi cha kuvutia wanyama na kuweka miundombinu na kuwa msitu mkubwa wenye miti na miundombinu mizuri.

"Alianza mwaka 1971 na ilipofika mwaka 1999 wanyama, walianza kuonekana na ikawa kimbilio la wanyama ambao wasingetunzwa walikuwa katika uwezekano wa kutoweka," anasema.

Haller anataja wanayama walipo mahali hapo na kutalii hivi sasa, ni swala, ngiri, kobe, Twiga, mamba, nyati, kiboko, nyani na vipepeo vya aina mbalimbali.

Nyinge anasema, hifadhi hiyo inapokea wastani wa wageni 500 kwa mwaka na katika mgawanyiko huo, wageni kutoka nje wako 160 na wanafunzi 200 kutoka shule mbalimbali.

Anasema, fedha zinazopatikana zinatumika kulipa ujira na kusaidia gharama za uendeshaji wa hifadhi hiyo.

"Mradi siyo wa faida kwa kiwanda, bali kurejesha uoto wa asili baada ya kumaliza kuchimba malighafi. Fedha zinazopatikana zinasaidia kuendeleza utunzaji eneo hili na kiwanda kinaendelea kama biashara kuu," anaibainisha.

### WANYAMA KIHISTORIA

Nyinge anasema viboko walipo hifadhini humo kila mmoja ana historia yake. Anatajwa mmoja , aitwaye Sally, aliokotwa katika Pwani ya Malindi kwenye mwambao wa bahari ya Hindi,

Anasema, hiyo ni baada ya kuzolewa na kimbunga Tsunami mwaka 2004 na ilipobainika hana mwenyewe, ndipo Wizara ya Maliasili na Utalii ya Kenya, iliwakabidhi.

Pia, kuna kiboko dume aliyetolewa nchini Ujerumani mwaka 1986, alikoishi kwa muda mrefu na walipoona muda wake wa matumizi umeisha na hali ya hewa ya eneo hili inamwathiri, walitafuta pa kumpeleka. Walimpeleka hifadhini humo.

Anasema kiboko Owen mwenye miaka 46, alikuja wakati mmoja na kobe wa kwanza mwenye miaka 160.

Kwa mujibu wa Mhifadhi huyo, Kiboko Sally ana miaka 48 na licha ya kuwaweka pamoja kwa miaka mingi, hawajapata mtoto kwa kile kinachoelezwa kimetoka kwenye mazingira tofauti na wameshindwa kuendana.



Bwawa lenye wanyama mbalimbali. **PICHA ZOTE: SALOME KITOMARI.**

Kwenye hifadhi hiyo kuna twiga watano, ambao mgeni anaruhusiwa kuwalisha chakula maalum kinachozwa kwa bei Sh.15 ya Kenya, sawa na Sh. 350 ya Tanzania.

Mhifadhi huyo anataja sharti la kumlisha ni kuweka chakula hicho kwenye kiganja na hairuhusiwi kumshika sehemu yoyote, kiasi cha kuwa rahisi kwa mgeni kupiga picha.

Katika eneo la mamba, kuna bwawa lenye ukubwa wastani ambalo limejaa mamba, idadi yao ikiingatiwa kwa kukusanya mayai na kisha kuwapa idadi kamili ya kutotoa, ili wasisambae kwenye msitu na kuleta madhara.

"Tunawafuatilia kwa karibu na ikifika wakati wa kuzaliana tunawalisha vya kutosha, ndiyo tunaingia kukusanya mayai na kuacha machache tunayotaka yazalishe watoto. Bila kufanya hivyo tutazalisha mamba wengi sana," anabainisha.

Katika eneo la mamba limejengewa kwa seng'eng'e, na kuna waya maalum wa kupeleka chakula kwa mamba hao, ambao hutakiwa kuruka kukidaka.

Anaeleza kuwa wana uwezo wa kuruka kimo cha tatu juu mita kudaka chakula.

### CHANGAMOTO

Nyinge anataja changamoto kubwa kwao ni uharibifu wa mazingira kwa wananchi kuingia eneo hilo kwa ajili ya kuapata kuni, pamoja wanyama kama tumbili na nyani kuvuka ukuta na kwenda kwenye makazi ya majirani.

Pia, anataja matibabu ya wanyama hufanywa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Kenya na kwamba wakizaliana kwa wingi, hupunguzwa kwa kutumia utaratibu maalum.

### VIWANDA & MAZINGIRA

Mhifadhi huyo anasema viwanda na mazingira vinakwenda pamoja na ndiyo maana waliamua kuanzisha hifadhi hiyo, ikiwa ni fundisho kwa wanaoanzisha viwanda.

"Kampuni ya Bamburi iko kimataifa kwenye nchi zaidi ya 90 duniani chini ya kampuni ya Lafargeholcin Holding company, katika maeneo yote tunakochimba malighafi. Lengo ni kupanda miti ya asili ili kuongeza hifadhi ya mazingira Pwani," anabainisha.

UCHUMI



Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladialaus Mwamanga.

MIONGO MIWILI YA UHAI

# Mwamanga afunguka safari ya Tasaf, milima na mabonde

- Wapo vijana 'hatimaye' chuo kikuu
- Wababaishaji pia...dawa yao jikoni

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), ulianzishwa na serikali mwaka 2000, kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali, katika jitihada za kupunguza umaskini kwa kutumia dhana ya ushirikishwaji.

Programu ya Tasaf inatekelezwa katika awamu tatu, ikitumia miradi mbalimbali katika ngazi ya jamii, lengo ni kupunguza umasikini wa msingi, wa kutoa huduma za jamii katika sekta zote.

Utekelezaji huo umekuwa ukizingatia mahitaji halisi au kero za wananchi waliko, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya serikali.

**AWAMU ZAKE**

Awamu ya kwanza ya Tasaf, ilianza kwa miaka mitano kati ya mwaka 2000 mpaka 2005. Hapo ilijumuisha halmashauri 40 za Tanzania Bara, pia Unguja na Pemba, ikiwekezwa fedha Sh. bilioni 72 yenye jumla ya miradi 1,704

Katika awamu ya pili, ilikuwa kati ya mwaka 2005 hadi 2013, ikiwa na wanachama halmashauri 126 za Tanzania Bara na wilaya zote Zanzibar. Hapo ikawa na thamani y a Sh. bilioni 430 yenye miradi 12,347.

Katika awamu ya tatu inayotekelezwa sasa, ilianza Februari 2013 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2023. Ni awamu iliyogawanywa katika kipindi cha kwanza, kilichomalizika Desemba 31 mwaka jana, ikishatumia Sh. trilioni 1.46.

Hapo ilishirikisha serikali za mitaa 159 kwa Tanzania Bara na Zanzibar wilaya zote.

**MKURUGENZI TASAF**

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladilaus Mwamanga anasema katika kipindi hicho cha kwanza cha awamu ya tatu, Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini nchini, ulijikita katika utoaji ruzuku kwa masharti ya kuangalia kaya masikini zenye watoto.

Hapo iliangalia namna ya kuzipatia huduma za elimu, afya na kuimarisha lishe, kwa lengo la kuinua ubora wa rasilimali watu.

Pili, ilijikita kutoa ajira za muda kwa kaya hizo, kwa walewenye uwezo wa kufanya kazi, katika baadhi ya mahitaji.

Tatu, Mwamanga anasema walijikita kuongeza kipato cha kaya masikini kupitia uwekaji akiba na shughuli za kiuchumi kuwaboreshea maisha.

Nne, walijenga na kuboresha miundombinu inayolenga sekta ya elimu, afya na maji, kwa kulenga umma kujenga uwezo katika ngazi zote za utekelezaji.

**ILIVYOFANIKIWA**

Mkurugenzi huyo anasema, Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa kushirikiana na wadau nchini imefanikiwa sana, kufikia kaya masikini sana zenye watu milioni 1.1 kupatiwa ruzuku.

Pia, Mwamanga anasema, kuna wanafunzi 1,805,613 kutoka kaya masikini walioandikishwa katika shule za msingi, na kati yao 448, 409 ni wa sekondari.

> **"Tatu, Mwamanga anasema walijikita kuongeza kipato cha kaya masikini kupitia uwekaji akiba na shughuli za kiuchumi kuwaboreshea maisha.**

Anasema, walienda mbali mwaka jana, kuna wanafunzi 277 waliomaliza kidato cha sita kupata mkopo wa kuendelea na masomo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu(HESLB), wakaweza kujiunga na vyuo vikuu nchini.

Mwamanga anasema mafanikio mengine ni kaya 253,117 kutoka halmashauri 42 za Tanzania Bara na kwamba Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar nako walishiriki katika miradi inayotoa ajira za muda.

Anataja miradi hiyo kuwa ni pamoja na ya maji, uhifadhi miti, barabara za vijijini, kilimo na umwagiliaji, hifadhi ya mazingira, hifadhi za ardhi na maji, huku kukiwapo miradi mingine 386 mbali na hiyo, yenye thamani ya Sh.bilioni 29.6 ilitekelezwa.

**MANUFAA**

Mwamanga anasema, kutokana na utekelezaji miradi hiyo, wananchi wamenufaika kupata barabara za vijijini, madarasa, nyumba za walimu, mabweni ya wanafunzi, matundu ya vyoo, madawati, zahanati na nyumba za watumishi wa afya.

Pia, anataja mengine ni mifereji ya umwagiliaji, mabwawa ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo pamoja na uhifadhi wa mazingira na misitu kupitia upandaji miti ekari 39,745.

Vikundi vya 311,114 wanufaika wa Tasaf, waliwekeza akiba katika halmashauri 54 za Tanzania Bara na Zanzibar, wakikusanya fedha jumla ya Sh.bilioni 2.5.

Mwamanga anataja ufugaji kuwa juu, katika ng`ombe, mbuzi, kuku, nguruwe sambamba na miradi ya kilimo jumla yao 561,300 na biashara ndogo 91,745, wakiwa na makazi bora yaliyoboreshwa.

"Kupitia mafanikio hayo, ni dhahiri kipindi cha kwanza cha awamu ya tatu ya Tasaf kimewezesha kaya masikini kushiriki katika uzalishaji mali na kukuza uwezo wa kukabiliana na majanga ya asili," anajigamba Mwamanga.

Anaendelea: "Mpango umechangia kupunguza umasikini na kuongeza uwezo wa kaya kumudu mahitaji yake na kuboresha ustawi wa jamii hususani watoto."

**CHANGAMOTO**

Mwamanga anasema kipindi hicho cha kwanza, pia katika mapitio yake kina changamoto kadhaa zilizojitokeza kwenye utekelezaji wake, suala la ubabaishaji wa kugundulika kaya zisizo na sifa kuwapo katika mpango.

Anasema, baada ya kubainika hilo na serikali kutoa agizo la kufanyika uhakiki kwenye halmashauri zote za Muungano zinazonufaika, wasio na sifa waliondolewa mara moja.

Mkurugenzi huyo, anasema kwa sasa wana mikakati mipya ya kudhibiti tatizo hilo kwa kuandikisha kaya hizo kwa kutumia teknolojia ya mfumo wa dira ya mtandao (Tablets).

Anasema, tayari wameshafanya majaribio ya mfumo huo katika halmashauri tatu za Mtwara Vijijini, Nanyamba zilizoko Mtwara na Siha, Kilimajaro, zilikoonyesha mafanikio makubwa.

Februari 17 mwaka huu jijini Dar es Salaam, Rais John Magufuli alipozindua Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu- Tasaf, kinachotarajiwa kutekelezwa kwa miaka minne, Mwamanga alimhakikishia kudhibiti walakini huo uliojitokeza.

"Tumefanya majaribio ya kulipa kwa kutumia tekonolojia kwa halmashauri 16 na sasa tupo tayari kutumia kwenye maeneo yote ya utekelezaji, kwa wale walengwa ambao hawajui kusoma na kuandika, utambuzi sahihi utafanyika kwa kutumia vidole," anasema Mwamanga.



Mnufaika wa Tasaf mkoani Njombe, akiwa na mradi wa mifugo yake nyumbani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (katikati), akijadiliana jambo na baadhi ya wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), baada ya mkutano na waandishi wa habari, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dhahabu yaibeba Chunya miezi 7

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya imefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni tisa kutokana na makusanyo ya mapato ya madini ya dhahabu kwa kipindi cha miezi saba.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanzisha soko la madini wilayani humo.

Mahundi alisema tangu kuanzishwa kwa soko hilo, mwezi Mei mwaka 2019 hadi kufikia Desemba, walifanikiwa kukusanya shilingi bilioni tisa iliyopatikana kwenye biashara ya dhahabu kuanzia soko kuu na madogo waliyafungua baada ya Rais John Magufuli kuagiza wilaya hiyo kufungua soko la pamoja la kuuzia madini. "Tumepata faida kubwa tangu kuanzishwa soko la madini wilayani hapa, mbali na kukusanya shilingi bilioni tisa, pia halmashauri imeweza kupata Sh. milioni 400, fedha ambazo tunazitumia kwenye shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa na ukarabati wa zahanati na vituo vya afya," alisema Mahundi.

Aidha, Mahundi alisema makusanyo hayo ya fedha yalipatikana baada ya kamati ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na wachimbaji wa madini kudhibiti mianya ya uuzaji holela wa madini ya dhahabu.

Alisema katika kudhibiti biashara holela, walifungua vituo vidogo sita kutoka kwenye kila eneo linalopatikana madini kufanya biashara ya uuzaji kabla ya kufika soko kuu ambavyo ni Sangambi, Makongorosi, Itewe, Igodima Itumbi na Matundasi. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Bosco Mwanginde, alisema biashara ya madini imekuwa chanzo kikubwa cha mapato na kwamba wanaendelea na jitihada kuhakikisha wanadhibiti biashara holela za uuzaji wa madini ili wakusanya fedha nyingi.

Alisema wanaandaa utaratibu wa kufungua soko dogo katika kila kata au kijiji kinachojihusisha na shughuli za uchimbaji wa madini ili kukusanya mapato mengi zaidi.

Naye Ofisa Madini wa wilaya hiyo, Godson Kamihanda, alisema tangu kuanzishwa kwa soko la pamoja na madini wachimbaji wamenufaika zaidi kwa sababu serikali ilitoa bei elekezi.

Alisema licha ya biashara ya madini kuwa na tija, lakini bado kuna vikwazo kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara ambao hawataki kuuza madini kwenye mfumo wa soko badala yake wanauza kwa njia za panya.

# Kyela yashtukia taarifa za kupika

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

KAMATI ya Afya, Elimu na Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, imeishauri halmashauri kujiridhisha na taarifa za miradi zinazotolewa na wataalamu kabla ya kupokea ili kuepukana na taarifa zilizopikwa ambazo haziendani na uhalisia.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa kamati hiyo, ambaye ni Diwani wa Ikimba, Katule Kingamkono, ambaye alisema miradi mingi haifanikiwi kwa sababu ya kutoa taarifa zisizokuwa na ukweli na kuiomba serikali kuwa makini na taarifa hizo.

Alitoa angalizo kuwa miradi inaweza kukabidhiwa bila kukidhi ubora na kiwango kinachotakiwa. Kingamkono alisema miongoni mwa miradi inayotiliwa shaka ni ya elimu katika Kata ya Njisi, Ngana na Nkokwa, baada ya kamati kukagua miradi ikiwamo ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Msingi Njisi, vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Ngana na ujenzi wa matundu manne ya vyoo katika Shule ya Msingi Nkokwa.

"Lazima tujiridhishe na miradi ya maendeleo tunayokabidhiwa na wataalamu, sisi madiwani tulichaguliwa na wananchi ili tuwatumikie, lazima tusimamie na kukamilisha miradi ambayo tuliahidi... haipendezi kuona wataalamu wanapika taarifa za uongo, ambazo haziendani na uhalisia, serikali inatoa fedha kwa lengo la kuleta maendeleo ya umma na sio mtu binafsi," alisema Kingamkono. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, ambaye ni Mjumbe wa Kamati zote, Hunter Mwakifuna, alisema kila mtumishi wa serikali ana wajibu wa kutekeleza na kusimamia miradi, kwa ajili ya kumnufaisha mwananchi. Mwakifuna alisema sio uzalendo kwa mtumishi wa serikali kupika au kutoa taarifa za uongo katika utekelezaji wa miradi anayoisimamia.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo, walisema hawatakubali kukwamishwa na viongozi wachache wenye maslahi binafsi na kwamba jukumu lao ni kusimamia na kuona miradi ya wananchi inatekelezwa.

Walisema jukumu la Baraza la Madiwani ni kuunda kamati ambazo zitakuwa zinafuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya wilaya kwa kuhakikisha inakamilika kikamilifu.

# Wataka soko la pamoja mahindi, mpunga

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa zao la mpunga na mahindi mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wameiomba serikali kuanzisha soko la pamoja la mazao hayo kama ilivyofanya kwenye zao la korosho ili kujiongeza kipato.

Walitoa ombi hilo wakati wa kikao maalum cha kujadili namna watakavyoweza kutafuta masoko ya zao hilo ndani na nje ya nchi, kilichoandaliwa na umoja wa wakulima wa mpunga mkoa wa Mbeya.

Patrick Sanga, katibu wa chama cha wakulima wa mpunga kata ya Igurusi wilayani Mbarali (Umacu), alisema mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inazalisha kwa wingi mpunga na mahindi, lakini wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa soko la uhakika, jambo linalosababisha kukosa faida na kushindwa kukiendeleza kilimo hicho.

Sanga alitolea Bonde la Usangu lililopo katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, linaloongoza kwa kuzalisha mpunga na maeneo mengine ikiwamo Kyela, na kwamba ili kupata uhakika kwa soko lazima wachague eneo moja ambalo litatumika kama kituo cha kukusanyia mchele.

"Igurusi tuna soko kubwa ambalo limejengwa kwa gharama ya serikali na wafadhili kutoka Umoja wa Ulaya (EU) na lina miundombinu yote muhimu... kupitia soko hilo tunaomba iwe ni kituo kikuu cha kuuzia na kukusanyia mchele ili kila mmoja apate faida," alisema Sanga.

Mjasiriamali wa bidhaa ya kusindika unga kutoka mkoani Iringa, Ezra Francis, alisema miongoni mwa sababu zinazokwambisha bidhaa za wajasiriamali wengi kutouza nje ya nchi ni urasimu wa utoaji vibali.

Alisema baadhi ya taratibu za utoaji vibali kwenye wizara ya kilimo zina changamoto, hali inayosababisha wafanyabiashara na wajasiriamali kukosa vigezo vya kuingia kwenye soko la ushindani.

Ofisa Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Kanda ya Mbeya, Emily Malinza, aliwataka wafanyabiashara kuacha kutumia njia za panya kupitisha bidhaa zao badala yake warasimishe na kuthibitisha uasili ili kupunguziwa kodi ya mauzo mipakani.

Alisema biashara ya mipakani ina tija kubwa kwa mfanyabiashara na taifa, kwani itasaidia kuongeza kipato pamoja kuwa na uhakika wa soko nchini jirani.

Alisema wakulima wa mpunga ukanda huo, wanapaswa kuchangamkia fursa za kibiashara mipakani katika nchi za Malawi na Zambia kwa kuhakikisha mchele wanaouza unakuwa kwenye kiwango kizuri na kuwekwa kwenye vifungashio.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, alisema wakulima wamejitahidi kuzalisha kwa wingi na tija mazao yao, lakini changamoto inayowakabili ni uhakika wa soko.

Aliiomba wadau wengine kuendelea kuwaunganisha wakulima pamoja ili mazao yao yauzwe kwenye vyama vya ushirika, huku akizisisitiza mamlaka zinazohusikana na utoaji ubora kama vile Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwashauri namna ya kutengeneza na kuzalisha bidhaa yenye viwango.





# Bunge kuboresha elimu ya mtoto wa kike

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Bunge limedhamiria kuboresha elimu ya mtoto wa kike nchini kwa kuelekeza nguvu katika ujenzi wa shule ya sekondari ya mfano ya wasichana.

Shule hiyo inajengwa na Bunge la 11 chini ya Spika Ndugai katika eneo la Kikombo, jijini Dodoma na inatarajiwa kukamilika Juni, mwaka huu. Ndugai alitoa kauli hiyo jana alipoambatana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kukagua eneo linapojengwa shule hiyo.

Alisema shule hiyo ni maalumu kwa ajili ya wasichana itakayojulikana kama Shule ya Sekondari ya Wasichana Bunge.

"Nimeona ni vyema waziri anayehusika na uendeshaji na usimamizi wa shule akajua mapema sehemu inapojengwa na maendeleo ya ujenzi wake ili kama kuna maboresho aweze kuyatoa mapema na kufanyiwa kazi.

"Hapa tunajenga kwa kutumia 'Force Account' mfumo ule ule ulioasisiwa na Tamisemi na ramani za majengo ni zile zile za Tamisemi, lakini kuna baadhi ya maeneo tumeboresha kidogo hatujaenda nje ya maelekezo ya wizara hii kuhusu ujenzi wa miundombinu ya shule," alisema.

Spika Ndugai alisema fedha za kujenga shule hiyo zimetokana na changisho lililofanywa na wabunge kupitia matukio ya kijamii.

Alisema wadau mbalimbali walichangia, na fedha zingine ni sehemu ya posho za wabunge na kupatikana jumla ya Sh. bilioni 1.2.

"Lengo la awali lilikuwa kujenga vyoo vya mfano vya wasichana katika kila jimbo nchini, lakini baadaye tukaona tuunganishe nguvu tujenge kitu kimoja kikubwa kitakachoacha alama ya Bunge la 11, litakapomaliza muda wake," alisema. Alieleza kuwa Bunge la 11 limefanya kazi ya ziada tofauti na ilivyozoeleka kisheria ya kutunga sheria. "Wakati huu tumeamua tufanye kazi ya jamii itakayoboresha elimu ya mtoto wa kike wa Tanzania na tukaelekeza nguvu katika ujenzi wa shule hii ya mfano ya wasichana," alisema Spika Ndugai.

Alifafanua kuwa shule hiyo inayojengwa itakuwa na miundombinu yote inayohitajika kwa ajili ya Shule ya Sekondari, ikiwamo madarasa ya kutosha, maabara, mabweni, bwalo la kisasa, vyoo, ofisi za walimu, jengo la utawala pamoja na maktaba yenye miundombinu ya Tehama.

Ndugai alisema ujenzi wa shule hiyo utakamilika mwezi Juni, 2020 na Bunge litakabidhi Ofisi ya Tamisemi.

Kwa upande wake Jafo alisema atahakikisha shule hiyo inakuwa na walimu wenye ubora na wanafunzi wenye ufaulu mzuri.

"Nimefarijika sana kuona wazo hili limeanza kutekelezwa na ndoto ya Bunge la 11 sasa inaanza kutimia na kwa sababu Spika amekuja kunionyesha kuanzia leo na mimi nitakuwa napita mara kwa mara kuangalia maendeleo ya ujenzi huu ili kwa pamoja tuweze kuikamilisha ndoto hii ya Bunge letu," alisema Jafo.

Alisema ofisi yake itahakikisha wanafunzi watakaosoma shuleni hapo wanafaulu kwa viwango vya juu ili shule hiyo iingie kwenye shule kumi bora za Tanzania katika matokeo ya kidato cha sita.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia afya, Doroth Gwajima (katikati), akizungumza na viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano, baada ya kufanya ziara kwenye ofisini yake, katika mji wa kiserikali Mtumba, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Tujifunze' yawezesha wanafunzi kusoma, kuandika

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

ASILIMIA 53 ya wanafunzi wa shule za msingi katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Pwani kati ya 500 wasiojua kusoma wamefanikiwa kujua kupitia mradi wa Tujifunze unaowasaidia wanafunzi walioachwa nyuma kimasomo.

Mradi huo unatekelezwa katika mikoa mitatu ya Dodoma, Morogoro na Pwani katika shule 15 na Shirika la Uwezo Tanzania.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Meneja mradi, Benjamin Masebo, alisema lengo la mradi huo ni kuwainua wanafunzi wasiojua kusoma wala kuandika ili waende sambamba na wenzao.

Alitoa mfano kwa Dodoma mradi huo unatekelezwa katika Shule ya Muendaje, ambako wanafunzi wengi wanajua kusoma na kuandika.

Alisema mradi huo umeanza mwaka jana na unatarajia kukamilika Juni mwaka huu na wataendelea kuongeza shule nyingine.

"Tunatarajia kuongeza shule nyingine kama tutafanikiwa, lengo ni kuhakikisha wanafunzi wanajua kusoma," alisema Benjamin.

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Fatma Toufiq, aliwataka wazazi na walezi kufuatilia maendeleo ya watoto wao kwa kukagua madaftari yao ili kuongeza hali ya ufaulu katika masomo yao.

Toufiq ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika linalojishughulisha na masuala ya wanawake (Wowap), alisema mashirika hayo yameshirikiana kutoa mafunzo ya ziada kwa wanafunzi walioachwa nyuma katika kusoma na kuandika.

Alisema katika shule husika wanafunzi hao hupewa darasa na walimu ambao wanafanya kazi ya kuwafundisha kusoma na kuandika.

Kwa upande wake, Ofisa Tarafa Khanifa Abdul, aliwataka wazazi kujenga utaratibu wa kuwakagua wanafunzi kama wanafanya kazi za darasani.

Alisema hivi sasa wazazi wanapaswa kuwa kitu kimoja ili kusaidia kuendeleza wanafunzi badala ya kuwaacha nyuma.

## Katambi ataka wanafunzi kupimwa mimba

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma mjini, Patrobas Katambi, amewaagiza wakuu wa shule za msingi na sekondari kutenga siku maalum ya kuwapima wanafunzi ujauzito kila baada ya miezi mitatu ili kukabiliana na tatizo la mimba kwa wanafunzi.

Pia ametangaza siku tano za kupokea na kufanya tathmini ya taarifa kutoka Jeshi la Polisi na taasisi za serikali kuhusu mimba kwa wanafunzi 195 wa shule za msingi na sekondari ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika.

Akizungumza baada ya kupokea ripoti ya utekelezaji ya mradi wa magauni manne uliyotekelezwa na Taasisi ya vijana mkoa wa Dodoma (DOYODO), Katambi alisema amedhamiria kutokomeza mimba kwa wanafunzi kwa kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa kwa wahusika kutokana na kesi nyingi kukwama mahakamani.

Alisema wanafunzi hao walipata mimba kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia Januari 2019 hadi Januari 2020.

"Kuanzia tarehe 1 hadi 5 Machi, mwaka huu nitapokea taarifa kamili ya watoto hawa nijue hatua zipi zimechukuliwa dhidi ya wahusika, ifike wakati mimba wanazopata watoto chini ya umri wao zibaki historia badala ya kila mara kusikia kuwa tatizo hilo limepungua kwa asilimia kadhaa au kusikia bado kuna idadi ya mimba zinaendelea," alisema.

"Hili ni agizo langu kwa Polisi, Mkurugenzi, PCCB na vyombo vingine mkishirikiana na mashirika binafsi kuchunguza kuanzia Machi 1 mpaka 5 kuwa nani wanahusika kati ya walimu, wazazi, vyombo vya maamuzi au vijana wa bodaboda na wengine watakaobainika ndiyo mwanzo mzuri wa kuchukua hatua."

Alitaka katika taarifa watakayowasilisha waeleze ni kesi ngapi zilifikishwa mahakamani na kutolewa hukumu.

"Tunataka tujue nani wanakwamisha na kwanini na tukishawabaini nitawatangaza ili Rais Magufuli pamoja na jamii wawajue ili hatua dhidi yao zichukuliwe hatutaki kusikia mimba sisi," alisema.

Alisema baada ya uchunguzi huo yoyote atakayegundulika kuhusika kumpa mimba mwanafunzi atakwenda jela miaka 30 kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo Katambi aliwaagiza wasimamizi wa elimu, taaluma na walimu wakuu kutenga siku maalum ndani ya miezi mitatu au chini ya hapo kuwapima wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mimba na watakaobainika hatua zichukuliwe haraka.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang`anya, alisema halmashauri ya jiji hilo imejipanga pia kufanya ziara za kushtukiza kwenye shule kupima mimba wanafunzi.

Awali, Meneja wa Taasisi ya Vijana mkoa wa Dodoma (DOYODO), Charles Rubeni, alisema mimba zimepungua kutoka 208 kwa mwaka 2018 hadi kufikia 195 mwaka 2019.

Mwisho



## Uhakiki wapigakura waingia wilaya mbili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UANDIKISHAJI na uhakiki wa taarifa za wapigakura umeanza katika majimbo yote ya Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja pamoja na Kimbo la Tunguu kwa Wilaya ya Kati Unguja.

Ofisa uandikishaji wa Wilaya ya Magharibi 'B', Khamis Mussa Khamis, alisema matayarisho ya mapema na juhudi zinazochukuliwa na tume katika kuwapatia wananchi taarifa mbalimbali za kiuchaguzi zimesababisha wananchi kujitokeza kwa idadi kubwa katika vituo vyote 38 vya wilaya hiyo

Alisema mafanikio ya zoezi la uandikishaji yanatoka na ushirikiano uliopo kati ya ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzinar (ZEC) na wakala wa usajili wa matukio ya kijamii kwa kuendelea kuwapatia wananchi vitambulisho vipya vya Mzanzibar mkaazi katika kila Wilaya kufuatana na ratiba ya uandikishaji.

Baadhi ya masheha ambao ni mawakala wa ZEC katika vituo vya uandikishaji waliwataka wananchi kuzitumia nambari zilizotolewa na tume kwa ajili ya kuangalia vituo vyao vya kujiandikisha na kuhakiki taarifa kabla hawajafika katika vituo ili kuepuka usumbufu wa kutafuta vituo vyao kutokana na changamoto ya mgawanyo wa shehia.

Wananchi wa Wilaya ya Magharibi 'B' waliofika vituoni kujiandikisha na kuhakiki taarifa zao, walisifu juhudi zinazochukuliwa na tume kwa uamuzi wa kutumia mfumo mzuri wa kiuandikishaji, ambao unasaidia zoezi hilo lifanyike kwa haraka zaidi.

"Hadi sasa utaratibu wa uhakiki na uandikishaji wa daftari unaendelea vizuri hakuna usumbufu wowote ukiwa na vielelezo vinavyostahiki unapata haki yako," alisema Ziada Mkonde, mwananchi aliyefika katika kituo cha uandikishaji Kisauni Jimbo la Chukwani.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Rajab Ali Rajab, alisema katika zoezi hilo la uandikishaji na uhakiki wa daftari hakujaripotiwa tukio lolote la uhalifu na wananchi wanafuata utaratibu waliopangiwa. Alisema kuna baadhi ya changamoto zilizojitokeza ni baadhi ya wananchi taarifa zao kuwapo katika vituo vingine walivyojiandikisha katika uchaguzi uliopita. Alieleza kuwa wananchi hao waende wakajiandikishe katika vituo vya awali na sasa ZEC inafanya uboreshaji wa daftari na baadaye ndio watu watahamisha taarifa zao katika vituo vyao vya sasa.

# Sheria ya dawa za kulevya kusukwa upya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema serikali inakusudia kuifanyia marekebisho sheria ya dawa za kulevya kwa kuzidisha adhabu kwa waingizaji, wasafirishaji na wasambazaji wa dawa hizo zenye madhara.

Alisema hatua mbalimbali za kupambana, kukemea na kuchukia shughuli zote zinazoshajiisha matumizi ya dawa za kulevya zitapaswa kuchukuliwa kutokana na kuathiri nguvu kubwa ya vijana, wazee na watoto. Balozi Iddi aliyasema hayo wakati akiahirisha Mkutano wa 17 wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, uliojadili miswada na ripoti za kamati za kudumu.

Alisema programu maalum ya uchunguzi wa kontena bandarini pamoja na mizigo katika viwanja vya ndege imeanzishwa kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, lengo likiwa kuzuia bidhaa haramu zikiwamo dawa za kulevya zisiingizwe nchini. Balozi Iddi alieleza kwamba Serikali Kuu kupitia mradi wa Zanzibar Salama imeweka vifaa vya ukaguzi (X-Ray Mashine) kwa abiria na mizigo inayoingia na kutoka nchini katika maeneo ya bandari na viwanja vya ndege.

Makamu wa Pili huyo alisema elimu inaendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari, majarida na vipeperushi juu ya athari za dawa za kulevya katika maeneo tofauti zikiwamo shule ili kuitahadharisha jamii kutojiingiza katika janga la dawa hizo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na taasisi za kitaifa na kimataifa na za kikanda kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya," alisema.

Aliwashukuru wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi wa taasisi za umma na binafsi kwa kutumia nafasi zao za kidemokrasia katika kuishauri serikali kuwajibika ipasavyo kwa wananchi wake juu ya njia sahihi za mapambano dhidi ya janga hilo. Akizungumzia uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, Balozi Iddi aliwataka wananchi kujiandaa kwa kujihakiki pamoja na kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura litakalomwezesha aliyefikia umri na sifa sahihi anapiga kura.

Aliwataka wananchi kufuatilia kwa karibu maelekezo yote yanayotolewa na tume zote za uchaguzi kuhusiana na mchakato huo uliokwishaanza katika maeneo mbalimbali ili kutumia haki yao ya kidemokrasia.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi baada ya kuahirishwa kwa Mkutano 17 wa Baraza la Tisa la Wawakilishi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar yapata fursa elimu ya juu Oman

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu ya Juu ya Oman kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Suza), zimezindua mchakato wa maombi ya udhamini wa elimu ya juu kwa ajili ya wanafunzi wa Zanzibar.

Uzinduzi huo ulifanyika jana Suza na kuhudhuriwa na maofisa kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Elimu ya Juu Oman, wahadhiri wa Suza na watendaji wa ubalozi mdogo wa Oman uliopo Zanzibar, ambao uliongozwa na Balozi Mdogo, Dk. Ahmad Hamoud Al Habsi.

Mkurugenzi wa Elimu ya Juu katika Wizara ya Elimu Oman, Hilal El Azki, alisema jumla ya nafasi 20 zimetolewa katika udhamini huo wa pili kwa wanafunzi wa Zanzibar ambao utagharamiwa na Serikali ya Oman kwa asilimia 100.

El Azki alisema milango ya kuomba udhamini huo kwa njia ya mtandao ilifunguliwa Februari 25 na inatarajiwa kufungwa Aprili 5, 2020, kabla ya kamati maalumu kufanya uteuzi kwa wale watakaotimiza vigezo vinavyotakiwa.

Alisema nafasi hizo zimegawiwa katika ngazi mbalimbali ikiwamo shahada ya kwanza na ya pili, nane kila moja, na nne ni uzamivu (PhD).

Makamu Mkuu wa Suza, Dk. Zuleikha Mohammed Abubakar, alisema huo ni mwendelezo wa programu ya udhamini iliyoanza mwaka 2013 ambayo imelenga kutayarisha wataalamu watakaofanya kazi Suza hapo baadaye.

Alieleza katika programu hiyo ya kwanza, wanafunzi 35 kutoka Zanzibar walibahatika kupata fursa hiyo na tayari wamehitimu na wakirudi kuajiriwa na chuo kikuu hicho.

Alisema udhamini huo ni matunda ya ziara ya Makamu wa Pili wa Rais aliyoifanya nchini Oman, na baadaye Waziri wa Elimu ya Juu wa nchi hiyo, Dk. Rauya Al Busaidy, kuja Zanzibar kuanzisha mazungumzo yaliyozaa programu hiyo.

Aliishukuru Serikali ya Oman na Wizara yake ya Elimu ya Juu kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu, akisema ushirikiano kati ya nchi hizo unatokana na udugu wa kihistoria uliodumu kwa miaka mingi.

Aidha, alieleza kuwa, hatua hiyo imezidi kupata mafanikio chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Balozi Mdogo wa Oman Zanzibar, Dk. Ahmad Hamoud Al Habsi, alisema ofisi zake ziko wazi kwa kila Mzanzibari atakayehitaji mwongozo na msaada wa namna ya kujaza fomu za maombi ya ufadhili huo.



Wanafunzi 18 wa Chuo Kikuu cha Zanzibar, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kushiriki mdahalo wa wazi kuhusu ikolojia ya kilimo Zanzibar, uliofanyika Old Dispensary katika Mji Mkongwe, Zanzibar juzi, kwa udhamini wa Ubalozi wa Ufaransa hapa nchini, chini ya ofisi ndogo ya kisiwani humo. **PICHA: ZULFA HASSAN, ZANZIBAR UNIVERSITY**

# DC akataza michango 'uchwara' shuleni

**Na Hamisi Nasiri,**
TANDAHIMBA

MKUU wa Wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara, Sebastian Waryuba, amepiga marufuku michango 'uchwara' kwa shule za msingi na sekondari inayokwenda kinyume cha maagizo ya serikali.

Waryuba alitoa agizo hilo juzi wilayani Tandahimba, kufuatia kuwapo kwa malalamiko ya wananchi aliyoyakuta wakati wa ziara yake ya siku moja aliyoifanya kwa ajili ya kusikiliza kero zao na kukagua maendeleo ya shule.

Alisema kuwa uchangishaji michango kwenye shule za msingi na sekondari kuna miongozo maalumu inayotambuliwa na serikali, na kwamba hiyo haina shida kama michango inatolewa na wazazi kwa hiari yao. Waryuba alisema serikali haitakubali baadhi ya shule wilayani humo kuwa na michango mingi isiyo na utaratibu aliyoiita 'uchwara' kwa vile imekuwa ikileta adha kwa wazazi na walezi.

Alisema suala la michango lazima liwe linatambulika na wazazi wenyewe kukutana kwenye mikutano na uongozi wa shule kisha kwa pamoja kukubaliana kwa pamoja juu ya utoaji wa michango.

Waryuba alisema michango ambayo wazazi hawaitambuwi na hawaelewi ina lengo gani kwao haitambuliki kisheria na hakuna sababu ya kuwatwisha mzigo wazazi na walezi.

Alisema wazazi na walezi wanapaswa kuisaidia serikali katika kuboresha miundombinu ya shule wanazosoma watoto wao kama vile kuchangia nguvukazi katika ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo na miundombinu mingine.

"Napiga marufuku walimu wakuu wa shule wilayani hapa kuchangisha michango wazazi ambayo ni kinyume cha maagizo ya serikali kupitia miongozo ya elimu michango yote lazima wazazi na walezi wakubaliane kupitia mikutano ya wazazi," alisema Waryuba.

Alisema kupitia miongozo ya elimu imeweka wazi juu michango ambayo wazazi na walezi wanapaswa kuchangia katika maendeleo ya shule, hivyo walimu watumie miongozo hiyo kwa kukutana na wazazi.

Mustafa Mussa, mkazi wa Tandahimba, alisema baadhi ya shule wilayani humo zimekuwa na michango mingi kwa wazazi na walezi, jambo ambalo limekuwa likileta adha kwao na kuomba serikali iliangalie suala hilo.

# TCRA yaikuna Kamati ya Amani

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAKALA wa Mbegu Tanzania (ASA,) unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji ambayo ingewasaidia kuongeza uzalishaji, na kuwa na mbegu kwa wakati wote.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mtendaji Mkuu wa wakala wa mbegu Tanzania (ASA), Dk. Sophia Kashenge, alisema licha ya sasa kulima huku wakiendelea kuuza mbegu, lakini wangepata kilimo cha umwagiliaji wakalima kila wakati, wangeweza kuwa na mbegu nyingi.

Alisema kilimo cha umwagiliaji kingewasaidia kuwa na mbegu nyingi ambazo zingefanya upatikanaji wa mbegu katika mashamba yao yote tisa nchini na kuwa na uhakika wa wingi wa mbegu na kufanya serikali kuzuia uingizwaji wa mbegu kutoka nje ya nchi. Aidha, aliipongeza serikali kwa kufanikiwa kununua matrekta matatu ya zana za kilimo za kufanyia shughuli mbalimbali nchini mwaka jana yenye thamani ya Sh. bilioni moja kupitia ASA.

Dk. Kashenge alisema awali ASA walikuwa na matrekta matatu pekee ambayo hayakuwa na uwezo zaidi ya kulima na kulazimika kukodisha ndege za kumwaga dawa wadudu wanapozagaa shambani ili kulinda mbegu.

Dk. Kashenge alisema kwa sasa matrekta hayo matatu yenye zana zake zenye uwezo wa kumwaga dawa ya kupandia, mawili na la kupigia haro moja yanawasaidia katika mashamba tisa ya mbegu wanayomiliki yaliyopo mikoa mbalimbali nchini. Aidha, alisema pamoja na changamoto wanazopitia, bado wanaongeza uzalishaji ambapo mwaka 2018/19 waliweza kuzalisha tani 1,220 za mbegu za mazao mbalimbali wanayozalisha na kufanya ongezeko la tani 784. Alisema kwa mwaka 2018/19 walizalisha tani 1,436 za mbegu kupitia uzalishaji wa mawakala wao wa kilimo kwa kampuni nane wanazofanya nazo kazi kwenye mashamba yao nchini ambapo mwaka 2017/18 walizalisha tani 2,500 na kufanya uwepo wa tani 3,936 za mbegu.

Dk. Kashenge alisema mpango wa ASA ni kuzalisha tani 4,400 za mbegu mbalimbali kwa hekta ambayo ni sawa na ekari mbili na nusu kwa mwaka.

# TBS yanoa wadau wa mikutano mashauriano

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

MIKUTANO ya mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji imeendelea maeneo mbalimbali nchini, huku wadau hao wakipatiwa elimu kuhusu majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), fursa ya wajasiriamali kupatiwa bure alama ya ubora pamoja na kuzipatia ufumbuzi wa changamoto zinawakabili.

Mikutano hiyo ya mashauriano kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa inayojumuisha Mara, Simiyu, Shinyanga na Mwanza ilianza Jumatatu, na kuhudhuriwa na mawaziri na manaibu waziri zaidi ya nane ikiwa ni mwendelezo wa mikutano iliyotangulia inayolenga kuzipatia ufumbuzi changamoto zinaziwakabili wafanyabiashara na wawekezaji. Mkutano wa majumuisho ya mikutano hiyo ya Kanda ya Ziwa ulifanyika jana jijini Mwanza. Katika mikutano hiyo Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, alitoa elimu kwa wadau hao kuhusu fursa wanazopata wafanyabiashara na wazalishaji ambao bidhaa zao zimekidhi viwango vya ubora, kuhamasisha wajasiriamali kuthibitisha ubora wa bidhaa zao bure pamoja na kuzipatia majibu changamoto wanazokumbana nazo wadau mbalimbali. Dk. Ngenya alitaja fursa zinazotolewa na shirika hilo kwa wajasiriamali kuwa ni pamoja kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha bila malipo kwa miaka mitatu lengo likiwa ni kuwawezesha kupanua soko la bidhaa zao na kuwaondolea vikwazo vya kibiashara.

Alisema serikali imeanzisha utaratibu huo ili kuwasaidia wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora na kupanua wigo wa masoko hayo.

Alitoa wito kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kuchangamkia fursa hiyo hasa katika kipindi hiki ambacho serikali inasisitiza ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema kuwa endapo wajasiriamali hao watathibitisha bidhaa zao itawasaidia kuzalisha bidhaa endelevu ambazo zitakuwa na soko kila mahali ikiwamo masoko ya kikanda.

Dk. Ngenya, alifafanua kuwa lengo la TBS ni kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara zenye tija kwa taifa, bila kuathiri taratibu na sheria za nchi.

HABARI KIMATAIFA

# China yapeleka bata Pakistan kukabiliana na tishio la nzige

**BEIJING, China**

CHINA iko mbioni kupeleka bata 100 nchini Pakistan kukabiliana na idadi kubwa ya nzige waliovamia taifa hilo.

Hayo ni kwa mujibu wa gazeti la Ningbo Evening lililoripoti hayo jana.

Gazeti hilo limeendelea kuripoti kuwa bata hao watapelekwa kutoka mkoa wa Mashariki wa Zhejiang kufuatia kutangulia kwa kundi la wataalamu wa China nchini Pakistan kushauri kuhusu jinsi ya kukabiliana na nzige hao waliovamia nchi hiyo, katika kile kinachotajwa kuwa uvamizi mbaya zaidi katika muda wa miaka 20.

Kwa mujibu wa Lu Lizhi, mtafiti katika taasisi ya teknolojia ya kilimo mkoani Zhejiang, miongo miwili iliyopita, China iliwapeleka bata hao ambao lishe yao asilia inajumuisha wadudu kukabiliana na uvamizi kama huo wa nzige katika eneo la Xianjiag Kaskazini Magharibi mwa nchi hatua iliyotajwa kupata ufanisi.

Pakistan ilivamiwa na kundi la nzige mwaka jana ambalo lilivamia mmea wa pamba na sasa ni tatizo kwa kilimo cha ngano.

Kwa sasa nzige wamekuwa ni tatizo kubwa katika nchi za Afrika, mojawapo ya nchi iliyoathiriwa na wadudu hao na kuleta uharibifu katika mazao ni Ethiopia, Kenya na baadhi ya nchi za Magharibi.

*DW*

# Mtoto wa rais kufungwa miaka miwili jela

**ALGIERS, Algeria**

MWENDESHA Mashtaka Mkuu wa Jamhuri nchini Algeria ameomba kifungo cha miaka 10 jela dhidi ya Kamel Chikhi, mfanyabiashara mkubwa nchini humo.

Chikhi anatuhumiwa katika kesi ya kufanya biashara kwa ushawishi katika mali isiyohamishika.

Pia mwendesha mashtaka huyo ameomba kifungo cha miaka miwili jela dhidi ya mtoto wa rais wa sasa wa Algeria, Khaled Tebboune, anayehusishwa pia katika kesi hiyo.

Kesi ya Chikhi, anahusishwa katika kesi ya biashara ya dawa za kulevya iliyoanza juzi.

Wakati alipokuwa akisikilizwa mbele ya majaji, Chikhi alijaribu kumtetea mtoto wa Rais, Khaled Tebboune, akihakikishia mahakama kuwa hajawahi kumsaidia kuhusiana na shughuli zake haramu za mali isiyohamishika. Tebboune pia alikataa kuhusika kwake katika shughuli hiyo.

Tebboune anashtumiwa kuwa na uhusiano na Chikhi anayekabiliwa na mashtaka.

Hivi sasa akiwa kizuizini na washtakiwa wengine sita, Tebboune atakabiliwa na mashtaka kadhaa, pamoja na kufanya biashara kwa ushawishi, utumiaji mbaya wa madaraka, ukusanyaji wa zawadi zisizofaa na ufisadi.

Aliwekwa kizuizini Juni 2018, kabla ya uchaguzi wa baba yake kama Rais wa Algeria, Abelaziz Bouteflika, wakati huo alikuwa bado rais.

Chikhi ndiye mtuhumiwa mkuu katika kesi ya dawa za kulevya zenye uzito wa kilo 700 aina ya Cocaine zilizokamatwa katika Bandari ya Algeria Mei 2018.

**RIF**



Waandamanaji wakitawanyika baada ya mashambulizi ya kurushiana mawe, karibu na Mji Mkuu wa India, New Delhi Jumatatu iliyopita. **PICHA: REUTERS**

# Polisi yaua wahalifu 22 waliotaka kuleta machafuko

**BUJUMBURA, Burundi**

SERIKALI ya Burundi imesema mwishoni mwa wiki iliyopita imewaua wahalifu wasiopungua 22 katika eneo la milimani lililojirani na mji mkuu wa Bujumbura.

Taarifa zaidi zilizotolewa na Jeshi la Polisi zilieleza kuwa tukio hilo ni katika kile ilichoeleza kuwa ni uhalifu unafungamana na uchaguzi wa rais uliopangwa kufanyika Mei, 2020.

Vyombo vya usalama nchini Burundi vimesema wakati wa mashambulizi hayo askari wawili waliuawa na watu sita waliowashambulia walikamatwa.

Mapambano hayo yalitokea baada ya wakazi wa eneo hilo kutoa taarifa Polisi kwamba kuna idadi kubwa ya watu wenye silaha waliojificha katika mashamba ya kahawa wilaya ya Nyabiraba.

Polisi wamesema mapigano pia yalienea katika wilaya ya jirani ya Isare.

"Wahalifu walikuwa wanatumia fursa ya kipindi hiki cha uchaguzi wakidhani watu watakuwa hawako makini," alisema msemaji wa Jeshi la Polisi, Pierre Nkurikiye na kuongeza:

"Wananchi wametakiwa kuwa na utulivu kwa sababu maofisa wa usalama wanaendelea kuimarisha ulinzi."

Burundi, ambayo inajumuisha makabila kama yale ya nchi jirani ya Rwanda, imepitia misukosuko ya kiukabila na vurugu za kisiasa kwa miongo kadhaa, ikiwamo vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya 1993-2005 ambapo watu 300,000 wengi wao raia waliuawa.

Uchaguzi wa Mei utamchagua mrithi wa Rais Pierre Nkurunziza, kiongozi wa zamani wa waasi ambaye amekuwa madarakani tangu 2005.

Awamu tatu za utawala wake umeshuhudia uvunjifu wa amani mara kwa mara na tuhuma za kimataifa juu ya uvunjifu wa haki za binadamu, jambo ambalo serikali yake inakanusha.

Katika uchaguzi huu, mgombea wa chama tawala cha CNDD-FDD, Evariste Ndayishimiye, Jenerali wa Jeshi mstaafu ambaye anaongoza kitengo cha masuala ya kijeshi katika ofisi ya rais, atachuana na kiongozi wa zamani wa waasi, Agathon Rwasa, wa chama cha upinzani cha CNL.

*VOA*

# Ofisa idara ya ujasusi Uturuki auawa Libya

**TRIPOL, Libya**

MWISHONI mwa wiki Rais wa Uturuki, Reçep Tayyip Erdogan, alikubali kuwapoteza askari wake kadhaa nchini Libya na hapo alikiri kifo cha askari wawili, bila kutoa maelezo zaidi kuhusu tarehe wala mahali.

Jana, habari mpya zimesababisha kutambua Ofisa wa Idara ya Ujasusi wa Uturuki, (MIT), Kanali Okan Altinay, kwamba aliuawa nchini Libya.

Taarifa hiyo ilianza kusambaa wakati wapiganaji wa kundi la ANL la Marshal Khalifa Haftar walidai kuwa waliwaua askari 16 wa Uturuki katika mashambulizi ambayo yalilenga bandari ya mji mkuu, Februari 18.

Kanali Okan Altinay alizaliwa mnamo mwaka 1971, alikuwa anasimamia zoezi la kutoa silaha kutoka Uturuki kwenda Tripoli, makao makuu ya serikali ya umoja wa kitaifa inayotambuliwa na jumuiya ya kimataifa.

Kulingana na wapiganaji wa ANL, kanali huyo, ambaye kawaida alikuwa akiishi katika eneo la jeshi la uwanja wa ndege wa Matigua, alienda bandarini kupokea silaha.

Msemaji wa wapiganaji wa ANL wanaoongozwa na Marshal Khalifa Haftar alisema: "Tulifanya shambulio bandarini, kufuatia habari sahihi tulioipata".

Miili ya askari hao wawili ilisafirishwa kwa siri kubwa nchini Uturuki kwa kutumia ndege ya kiraia ya Libya usiku wa Februari 18.

Katika siku za hivi karibuni, vyombo vya habari vya Uturuki vimesema, vikinukuu familia na ndugu wa Kanali Okan Altinay, kwamba alizikwa kwa siri, bila sherehe ya kijeshi katika kijiji chake katika mkoa wa Aydin, magharibi mwa Uturuki.

*RFI*

# Wachimbaji wadogo waahidiwa fursa

**Na Mwandishi Wetu**

WACHIMBAJI wadogo wa madini wameahidiwa kuboreshewa huduma za kifedha.

Ahadi hiyo imetolewa na Benki ya NBC ambayo imejizatiti katika kuboresha huduma na bidhaa zake ziendane na mahitaji mahsusi ya wachimbaji wadogo.

Ahadi hiyo imetokana na uzoefu ambayo benki hiyo imeupata wakati wa kongamano la madini, ambalo lilifadhiliwa na benki hiyo.

Akizungumza katika kongamano hilo lililofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Wakala wa Mauzo Kitengo cha Hazina na Masoko ya Fedha za Kigeni wa benki hiyo, Emmanuel Charles Gasirabo, alisema: "Kongamano hili limekuwa na mafanikio sio tu kwa wachimbaji wadogo, bali pia kwa NBC ambayo hutoa huduma za kifedha."

Alisema kufuatia ufahamu wa ziada uliopatikana juu ya sekta hiyo, benki yake imeng'amua namna ya kujipanga kisawasawa ili kuhakikisha kuwa wanachangia kwa vitendo katika ukuaji wa sekta ya uchimbaji.

"Sisi tumebainisha uhitaji mkubwa sana miongoni mwa wachimbaji wadogo na wa kati. Tumechukua maoni yao kwa ajili ya kuyafanyia kazi, tuna msimamo kuwa kuna haja ya kukaa nao pamoja ili kubainisha njia za kutatua changamoto zao," alisema.

Akifafanua zaidi, Garisabo alisema: "Mbali na huduma zetu za kawaida ambazo huwanufaisha zaidi wachimbaji wakubwa, tunapanga kuja na bidhaa zanazohudumia wachimbaji wadogo na wa kati, sisi tunathamini mchango wa sekta ya madini kwenye uchumi na benki ipo makini sana kuona kwamba sekta ya madini inapata huduma rasmi za kifedha."

"Alisema wanafahamu mlolongo mzima wa thamani katika sekta ya madini kuanzia wachimbaji wadogo kupitia wa kati hadi wafanyabiashara wa madini.

Aidha, alisema benki hiyo inatambua kuwa wachimbaji wengi wanakumbana na changamoto nyingi ikiwamo kuendesha biashara kwa kutumia vyanzo vya mitaji visivyo rasmi.

Aliwashauri wadau wa sekta ya madini kulipa malipo yao ya serikali kupitia benki ya NBC, kwa kuwa imeunganishwa rasmi na mfumo wa malipo ya serikali, inayofahamika kitaalamu kama GePG.

Meneja masoko wa benki hiyo, Alina Maria Kimaryo, alisema benki inatambua wazi kuwa kuna wachimbaji wadogo, na kuongeza kuwa kundi hili linashabihiana sawia na mtandao wa NBC Club, ambao lengo lake ni kuwawezesha wafanyabiashara wadogo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya GT, Jubril Adeniji (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Viziwi Buguruni, Richard Kweka, kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wa shule hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mjumbe wa Bodi wa benki hiyo, Francis Nanai. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Benki ya Dunia kuendeleza uboreshaji wa mahakama

**Na Mary Gwera, MAHAKAMA**

BENKI ya Dunia imeonyesha nia ya kuongeza fedha za mkopo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za mahakama kutokana na utekelezaji mzuri wa mradi huo katika kipindi cha awamu ya kwanza kinachotarajia kukamilika mwaka wa fedha wa 2020/21.

Mahakama ya Tanzania na Benki ya Dunia, juzi zilifanya mazungumzo juu ya mchakato wa maandalizi ya kuongeza muda na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mazungumzo hayo yaliyoshirikisha ujumbe kutoka Benki ya Dunia na baadhi ya watendaji waandamizi wa mahakama yalifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Kitengo cha Maboresho ya Mahakama, Dar es Salaam.

Mkuu wa Kitengo cha Maboresho Mahakama ya Tanzania, Zahra Maruma, alisema miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa yatakayosaidia kupatikana kwa fedha hizo ni pamoja na kuibua maeneo yenye changamoto na kuona ni jinsi gani yanaweza kufanyiwa kazi na kuboreshwa ili kupata mwendelezo mzuri wa utekelezaji kutoka mwanzo hadi sasa.

"Miongoni mwa maeneo yaliyopendekezwa na Benki ya Dunia kufanyiwa maboresho zaidi na mahakama ni pamoja na kuongeza mafunzo kwa watumishi na kuwa usimamizi thabiti wa mifumo ya usimamizi wa fedha na kadhalika," alieleza Maruma.

Kwa upande wake, Mahakama imeihakikishia Benki ya Dunia kuwa watatekeleza maeneo yote yaliyopendekezwa ifikapo Aprili, mwaka huu.

Ujumbe huo wa Benki ya Dunia upo nchini kuanzia Februari 19 mpaka leo lengo ikiwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi huo unaotekelezwa na Mahakama ya Tanzania.

Katika kipindi hicho, ujumbe huo ulifanya mazungumzo na Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Kiongozi na baadhi ya viongozi na watendaji wa Mahakama ya Tanzania na kutembelea majengo mapya ya mahakama kuu kanda za Kigoma, Musoma na Arusha na ujenzi wa kituo jumuishi cha utoaji haki (IJC).

## Serikali yahakikisha mazingira bora ya ufugaji wa samaki

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewahakikishia wafugaji wa samaki nchini kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kuwawezesha kufuga samaki.

Ulega aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji wa Mkoa wa Shinyanga ambao ulihudhuriwa pia na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Uwekezaji, Angellah Kairuki.

Alisema mabwawa ya samaki yameongezeka kutokana na jitihada za serikali inavyoendelea kudhibiti uvuvi haramu baharini na kwenye maziwa.

"Kabla ya serikali ya awamu ya tano, katika Ziwa Victoria tulikuwa na vizimba vya ufugaji wa samaki visivyozidi 50 hivi leo tuna vizimba zaidi ya 400 vya ufugaji wa samaki maana yake mwitikio ni mkubwa," alisema.

"Mwanzo tulikuwa na tatizo la bima, lakini hivi sasa tupo kwenye hatua nzuri bima kwenye mifugo na uvuvi ili upatikanaji wa fedha kwenye eneo hili uwe wa uhakika kwa wafanyabiashara.

Alisema kwa upande wa Ziwa Victoria, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepata fedha nyingi kwa watu wenye lengo la kufuga samaki na kwa kuwa soko lipo la uhakika ndiyo maana watu wengi wameingia katika ufugaji na uvuvi.

"Tumeweka mazingira mazuri ya kuhakikisha Watanzania wanaoingia kwenye biashara za mifugo na uvuvi wapate soko. Mwanzo tulikuwa tunaagiza nyama nyingi kutoka nje ya mipaka yetu, lakini serikali imefanya kazi kubwa," alisema Ulega.

Alisema fursa kubwa iliyopo sasa ni biashara ya kunenepesha mifugo na kupeleka kwenye viwanda vya nyama vilivyoanzishwa na vinavyotarajiwa kuanzishwa.

"Hivi viwanda tunavyovianzisha hakika vitahitaji malighafi, ni lazima iwe malighafi ya uhakika kwa hiyo biashara iliyo nzuri sana sasa hivi ni ya kunenepesha mifugo yetu," aliongeza.

Vile vile, alisema serikali imeshawishi taasisi za fedha na zimekubali kuingia kwenye biashara za kunenepesha mifugo na uvuvi na kubainisha kuwa jambo hilo linahitaji ushirikiano kati ya serikali na wadau.

"Kwa upande wa ngozi bado tuna changamoto kubwa, jitihada kubwa zimefanyika kuhakikisha tunapata suluhu ya hili jambo la ngozi. Tunahakikisha viwanda vyetu vinaanza uzalishaji, kama tulivyofanya katika uvuvi," alisema.

Naye Kairuki alisema serikali itaendelea kuwaunga mkono wafanyabiashara na kuwakumbusha kufuata sheria na kanuni zilizopo katika biashara na uwekezaji na wanapokuwa na migogoro wasisite kuwasiliana na serikali ili kuitatua.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**SHULE YA CHEKECHEA INAKODISHWA**
Shule ya Chekechea inakodishwa au ubia, pia yaweza kubadilishwa na kuwa kituo cha Elimu au kituo cha Afya . Ipo Mbezi Luis. Kwa mawasiliano: **0712 480 836 / 0765 138 779.**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA MWANZA**

**SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA MADAI**

**NAMBA 47/2019**

**ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION.....................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**NICKSON APOLINARY MTABIRWA...WAJIBU MAOMBI**

**KWA: JOSEPHAT NYAMHANGA NYAMAGANA – MWANZA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa kuhhudhuria hapa mahakamani tarehe 2/3/2020 kuja kusikiliza shauri la maombi madogo ya madai yaliyofunguliwa na mwombaji dhidi yenu.

Unatahadharishwa kuwa endapo hautofika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 27/2/2020.

..................
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU TANZANIA MWANZA**

215649602

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**Grephson Shoo** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **Toyota Hilux- Pick Up** yenye Usajili wa namba **T619 AKW** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

115649701

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA: 63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya MJINI TANGA**
**Wilaya ya TANGA**
**MADAI NAMBARI: 33 ya 19**

**Mdai: MWANSHAMBA HASSANI NASRI**
**Mdaiwa: SHABANI ALLY SALEHE**
**Kwa: SHABANI ALLY SALEHE MZARAMO /MWENYEKITI WA MTAA MKURANGA PWANI**

Kwa kuwa mdai/mdaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba/Eleza hapa habari za madai

**TALAKA/ MGAWANYO WA MALI ZA NDOA**
Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 2/3/2020 saa 2:30 asubuhi alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukudhuria/hamkudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 24/2/2020

115648802

**KUPOTEA KWA CHETI**



**MAIMUNA KOMBO HABIBU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0188-0537 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIRINJIKO ISLAMIC SEMINARY** mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/MSI/RB/181024/2020.**

115648902


*NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA*

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BECKHAM

## - SOLSKJAER ANAFANYA VIZURI UNITED




**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer "anafanya kazi nzuri" pale Old Trafford, kwa mujibu wa nyota wa zamani wa klabu hiyo, David Beckham.

Solskjaer, yupo kwenye msimu wake wa kwanza kamili baada ya awali kuchukua mikoba kutoka kwa Jose Mourinho kama kocha wa muda Desemba mwaka 2018, amekuwa akishutumiwa kwa mwenendo mbaya wa United ambayo ipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

United imeifunga Manchester City, Chelsea, Tottenham na Leicester City msimu huu, na ametoka sare na vinara Liverpool, lakini mashetani wekundu hao bado wamepitwa pointi tatu kwenye nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya United kujikongoja, Beckham - ambaye alicheza na Solskjaer pale United amempigia debe kocha huyo raia wa Norway.

"Nafikiri anafanya kazi nzuri," amesema Beckham akiiambia Sky Sports. "Ukweli ni kwamba ameweza kuibadilisha timu, ameendelea kuwa kwenye nafasi nzuri akichukua nafasi ya Alex Ferguson.

"Hawezi kumshtumu mchezaji yoyote kutoka katika timu yake, mimi naona anaendelea vizuri tu.

"Bado anajifunza, lakini atawalinda wachezaji wake na Manchester United. Mashabiki wote watakuwa nyuma yake kwa sababu ni mtu mzuri."

## GUARDIOLA ASIFIA KIWANGO CHA JESUS



**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema hakuna mshambuliaji duniani mwenye nguvu akiwa hana mpira kama Gabriel Jesus baada ya raia huyo wa Brazil kuwa nguzo ya ushindi wao Jumatano dhidi ya Real Madrid.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alianza mbele ya Sergio Aguero kwenye mchezo huo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora na alilipa fadhira kwa kocha wake kwa kiwango alichokionesha.

Isco alianza kwa kufunga bao la kuongoza kwa Real Madrid, lakini Jesus akafunga kwa kichwa kusawazisha kabla ya Kevin De Bruyne kufunga la ushindi kwa mkwaju wa penalti.

Guardiola alimsifia Jesus baada ya mchezo huo wakati akizungumza na waandishi wa habari: "Hakuna mshambuliaji duniani mwenye nguvu akiwa hana mpira kama Gabriel.

"Ni mtu ambaye anaweza kupiga chenga na kukimbia. Lakini anakuwa hana kasi kubwa kama akiwa na mpira, ila ukimtangulizia uwezo wa kukimbia kumpita mlinzi yoyote na kuuwahi mpira ni mkubwa.

"Tuliamua kucheza bila ya kuwa na mshambuliaji halisi mbele kwa sababu ya staili ya ulinzi ya Madrid.

"Walikuwa wanalinda kwa staili ya aina yake. Walikuwa na uwezo mkubwa wa kumkaba mchezaji mmoja mmoja na ndio maana tukaamua kubadilisha mbinu."

# United, Barcelona zamwania Werner

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United na Barcelona zimewasilisha maombi ya kuwania saini ya Timo Werner katika kipindi cha majira ya joto, lakini inaonekana nyota huyo anasubiri kuona ofa ya kujiunga na Liverpool, taarifa mbalimbali zinasema.

Werner anaelewa kuwa ni mmoja wa wachezaji wanaotakiwa katika kikosi cha Jurgen Klopp licha ya kuwindwa na timu mbalimbali za barani Ulaya.

Wiki iliyopita, nyota huyo ambaye alisaidia RB Leipzig kupata ushindi dhidi ya Spurs aliweka wazi nia yake ya kutaka kujiunga na klabu hiyo.

Hata hivyo imeelezwa dau la kumnunua nyota huyo ni pauni milioni 51, lakini gazeti moja la Ujerumani liitwalo Sport1 limeandika thamani iliyotajwa kwenye mkataba wake ni pauni milioni 30.

"Ninajua kuwa Liverpool ni timu nzuri kwa sasa hapa duniani na ninajisikia fahari ninapohusishwa na timu hiyo," alisema Werner.

Kwa mujibu wa Athletic, Werner anasubiri kuona kama Liverpool itafanya mchakato wa kumsajili.

Taarifa zinasema zaidi kuwa ili kumpata mchezaji huyo, klabu itatakiwa kumsajili kabla ya Aprili haijamalizika, ambapo mkataba wa Werner utaboreshwa.

Lengo la kuweka kipengele hicho, kitasaidia klabu hiyo ya Ujerumani kupata nafasi ya kutafuta mchezaji mwingine ambaye ataziba pengo atakaloliacha kuelekea msimu ujao.

Kama Klopp bado ana nia ya kumsajili nyota huyo, atatakiwa kukamilisha mchakato huo katikati ya mwezi ujao.

## HABARI MICHEZO



# BECKHAM

## AWAITA MESSI, RONALDO MAREKANI

**MIAMI, Marekani**

DAVID Beckham amesema kwamba, timu ya Ligi Kuu Marekani, MLS, Inter Miami ina "nafasi kubwa" kuwasajili nyota Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Nahodha wa Barcelona, Messi na mshambuliaji wa Juventus, Ronaldo wote wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kwenda kumalizia soka lao nchini Marekani.

Na Beckham ambaye ni mmoja wa wamiliki wa klabu ya Inter Miami anaona kuna uwezekano mkubwa kwa wawili hao kutua huko.

Kuna uvumi kwamba Inter, ambayo itacheza mechi yake ya kwanza ya MLS dhidi ya Los Angeles FC Jumapili, inaweza kuwasajili wachezaji hao kutua Miami baada ya kocha wa Minnesota United, Adrian Heath kuzungumzia kuhusu uwezekano huo.

Mmiliki mwenza wa Inter, Beckham amebainisha kuhusu uvumi huo wakati akiwa kwenye kipindi cha televisheni cha 'The Tonight Show Starring Jimmy Fallon' Jumatano.

"Unajua nini, tuna nafasi kubwa hapa," alisema kocha huyo wa zamani wa Manchester United, Real Madrid na timu ya taifa ya England.

"Tumewasiliana na wachezaji wengi tofauti kuhusu uwezekano wa kujiunga na timu yetu.

"Kama ilivyo kwa mmiliki yeyote anataka wachezaji bora na kama tukiwa na nafasi ya kuwaleta wachezaji kama Cristiano au Leo, naamini itakuwa nafasi nzuri zaidi kwenye kuwapa hamasa wachezaji wengi zaidi kuja."

# Vinicius: Madrid mara zote inaonewa

**MADRID, Hispania**

MCHEZAJI Vinicius Junior anaamini mara zote maamuzi yote mabaya ya waamuzi yanakuwa dhidi ya Real Madrid baada ya timu yake kufungwa 2-1 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City.

Madrid walipoteza kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 kwenye dimba la nyumbani la Santiago Bernabeu Jumatano baada ya Kevin De Bruyne kufunga mkwaju wa penalti katika dakika ya 83 na kuiwezesha City kutoka nyuma na kupata ushindi huo.


Gabriel Jesus alisawazisha bao la Isco, ingawa Madrid walimlalamikia fowadi huyo wa City kumsukuma Sergio Ramos, ambaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumfanyia faulo mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

Vinicius alilalamikia kutoadhibiwa kwa Jesus ambaye alimfanyia faulo Ramos wakati akisawazisha.

"Uwanja wote uliona Gabriel Jesus akimsukuma Ramos. Hata kwangu hakutoa adhabu niliposukumwa na (Riyad) Mahrez kipindi cha kwanza," alisema.

"Wanatufanyia vibaya. Sisi ndio timu iliyoshinda mara nyingi zaidi taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na mara zote wamekuwa wakitufanyia hivyo.

"Ilikuwa faulo ya wazi kabisa na sielewi kwanini hakutoa adhabu kwa mchezaji na kuruhusu bao."




# Lacazette naye kutimka Arsenal

**LONDON, England**

ALEXANDRE Lacazette ana makubaliano na klabu ya Arsenal kwamba watamruhusu aondoke kwenye timu hiyo kama watashindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Raia huyo wa Ufaransa amebakiza miaka miwili katika mkataba wake wa sasa pale Arsenal baada ya kujiunga na miamba hiyo kwa ada ya pauni milioni 52 akitokea Lyon mwaka 2017.

Gazeti la The Times limebainisha kwamba, Lacazette ataruhusiwa kuondoka kama Arsenal itashindwa kufuzu kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa 2020-21.

Arsenal kwa sasa inashika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi saba nyuma ya nne bora na pointi 42 nyuma ya vinara Liverpool.

Lakini, kikosi hicho cha kocha Mikel Arteta hakijapoteza mchezo wowote tangu mwaka huu wa 2020 uanze, hivyo jambo hilo linawapa matumaini na nguvu ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Manchester City amefungiwa kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa misimu miwili na kama watafeli kwenye rufani yao basi jambo hilo litafanya timu itakayomaliza nafasi ya tano kupata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kama chama la Pep Guardiola kumaliza msimu ndani ya nne bora.

Lakini, Arsenal wanaweza kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2020-21 kama watabeba ubingwa wa Ligi ya Europa, ambako wamejiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya 16 bora baada ya kuwachapa Olympiacos 1-0 ugenini.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE: MADRID ILIPOTEZA UTULIVU

●●●Kocha huyo Mfaransa atamba kupindua meza katika dakika 90 zilizobakia za mechi hiyo...

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane amekilaumu kikosi chake cha Real Madrid kwa kutotulia mchezoni dhidi ya Manchester City, lakini amesisitiza bado wana nafasi kwenye mchezo wa pili wa mtoano wa timu 16 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, licha ya kichapo cha mabao 2-1.

Madrid walipoteza nyumbani dhidi ya kikosi cha kocha, Pep Guardiola, ambao walifunga mabao mawili ndani ya dakika tano katika kipindi cha pili cha mchezo huo wa kwanza uliochezwa juzi Jumatano.

Washindi mara nne kwa misimu sita iliyopita kwenye michuano hiyo, miamba hao wa LaLiga walianza kwa kuongoza kwa 1-0, bao lililofungwa na Isco kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la Santiago Bernabeu.

Lakini Madrid wakajikuta wakifungwa bao la kusawazisha na Gabriel Jesus kwa kichwa dakika ya 78, kabla ya Kevin De Bruyne kufunga bao la ushindi kwa penalti zikiwa zimesalia dakika tano mpira kumalizika, huku Sergio Ramos akitolewa kwa kadi nyekundu.

"Hatukutulia na tumepoteza, lakini tunajua kwamba hatua hii ina dakika 180, nusu ya dakika tumeshazitumia na imebaki nusu nyingine na tutaona nini kitakachotokea," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Hata kama tuko nyuma. Tulifanya kazi ya ziada kufunga, na baadaye dakika 10 wakafunga mabao mawili."

Nahodha wa Madrid, Ramos ataukosa mchezo wa pili wa marudiano mjini Manchester baada ya kumchezea rafu Jesus zikiwa zimesalia dakika nne mpira kumalizika na Zidane alisema: "Hiyo ndio soka. Hatuwezi kubadilisha. Tunatakiwa kuwa na mtazamo chanya.

"Katika matokeo kama yale kuna vitu vingi chanya vya kuviangalia, tulicheza vizuri, lakini dakika 10 au 15 za mwisho hatukuwa sawa.

"Tunahitaji kwenda pale na kushinda ili tuweze kufuzu hatua inayofuata, tutakwenda kufuata matokeo ya ushindi."

## KWA UFUPI

**MOURINHO AITAMBIA UNITED**
KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, anaamini ataishinda klabu yake ya zamani Manchester United katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Sweden, Emil Forsberg (28). ***(Express)***

**VERTONGHEN SOKONI**
KLABU inayoshiriki Serie A, Inter Milan imefanya mawasiliano na Tottenham kuhusiana na usajili wa beki wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jan Vertonghen (32), ambaye tayari alikuwa ameshakubali kusaini mkataba mpya. ***(Standard)***

**SALAH ATAJWA MADRID**
REAL Madrid inaamini itaweza kunasa saini ya mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah (27), kwa dau la pauni milioni 126 endapo itafanikiwa kumuuza mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale (30). ***(El Desmarque, via Express)***

**LINGARD, PEREIRA KUUZWA**
MANCHESTER United inajiandaa kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard (27), na kiungo wa Brazil, Andreas Pereira (24), ili kupata fedha za kufanikisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24). ***(Express)***

**ARSENAL, AUBAMEYANG KUTETA**
ARSENAL imeanza kuzungumza upya na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), kuhusiana na mchakato wa kusaini mkataba mpya baada ya ule wa awali ambao analipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Times, subscription required)***

**FIRMINO ANUKIA BAYERN**
MABINGWA wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayern Munich, wameanza mawasiliano na wawakilishi wa mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Brazil, Roberto Firmino (28), ili kunasa saini yake. ***(Echo)***

**WERNER AGOMBEWA ULAYA**
MANCHESTER United na Barcelona zimeanza mchakato wa kumwania mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (23), lakini anaonekana anahitaji kujiunga na Liverpool. ***(Mirror)***

**CONTE AMTAKA ALONSO**
KOCHA wa Inter, Antonio Conte amepanga kusaini mmoja wa mabeki wa kushoto wa Chelsea, na tayari Conte amebainisha ni kati ya Mhispania Marcos Alonso (29) au Mtaliano Emerson Palmieri (25), katika kipindi cha majira ya joto. ***(Tuttosport, via Mail)***

**WILLIAN MAMBO MAGUMU**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Brazil, Willian (31), amesema kitendo cha kutofikia makubaliano na klabu hiyo kuhusiana na ofa mpya aliyopewa kinafanya mazingira yake kuwa magumu. ***(Esporte Interativo, via Football 365)***

**DE GEA AWEKWA SOKONI**
GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea (29), huenda akauzwa ili kupata fedha za kusaidia usajili wa wachezaji wengine inaowahitaji, huku Dean Henderson (22) wa Sheffield United akitajwa kutua kwa mkopo. ***(Mirror)***

**SMALLING, MKHITARYAN SAFI**
ROMA imeweka wazi nia yake ya kumpa mkataba wa kudumu beki wa England, Chris Smalling (30) na kiungo wa Armenia, Henrikh Mkhitaryan (31). Nyota hao wako Roma kwa mkopo wakitokea Manchester United na Arsenal. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

# NIYONZIMA ARUDISHA UFALME WAKE YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na kiungo wake, Haruna Niyonzima ambaye juzi alifunga bao pekee katika mechi ya Kombe la FA na kuipeleka timu hiyo katika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Eymael alisema kiungo huyo alionyesha uzoefu katika mchezo huo uliokuwa na ushindani, lakini akawapongeza wachezaji wenzake kwa kupambana kusaka ushindi katika mchezo huo.

Eymael alisema kuwa mechi hiyo haikuwa rahisi kwa kila upande na kuongeza kwamba kikosi chake kinaendelea kujipanga ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo ujao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Alliance FC kutoka jijini Mwanza utakaochezwa kesho.

"Nimefurahishwa na matokeo tuliyoyapata na kuweza kusonga mbele katika michuano hii ya Kombe la FA, ingawa tulikuwa na mapungufu machache," alisema Eymael.

Kocha huyo aliongeza wapinzani wao walionekana kupoteza muda zaidi, lakini wachezaji wake walijipanga kutumia vema nafasi ili kukamilisha malengo yao ya kusonga mbele katika mashindano hayo.

Alisema kikosi chake kitaendelea na mazoezi kama kawaida kwa ajili ya mechi inayofuata na hii inatokana na ratiba kubana.

"Sitakuwa na mapumziko leo (jana), tumeendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwaweka sawa wachezaji wangu ili kukutana na Alliance kesho kutwa (kesho), nikiwa na lengo la ushindi tu," Eymael alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema baada ya kuondoa 'mzimu wa sare', sasa hivi kikosi chao kinajipanga kuendelea kutoa 'dozi' kwa kila timu watakayokutana nayo.

Mwakalebela alisema mikakati yao ni kuona wanaendeleza ushindani na bado hawajakata matumaini ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara.




Mshindi wa Jackpot bonasi ya SportPesa, Francis Mrema (kushoto) wa jijini Arusha akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 28.7 na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas baada ya kuweka mikeka yake ya Jackpot Double Combination. Jackpot ya wiki hii ni Sh. milioni 219.2, cheza ili uibuke milionea. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali Mwanza yawaita wasanii

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

ILI kunufaika na mikopo inayotolewa na Halmashauri ya Jiji, vijana wametakiwa kujiunga katika vikundi mbalimbali vya sanaa kwa lengo la kuwaepusha na tabia ya kutumia muda mwingi 'kuchat' kwenye mitandao ya kijamii.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Utamaduni wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Julius Kambarage, wakati wa utambulisho wa tamasha la wazi la bidhaa za wajasiriamali huru lililofunguliwa jana na litakalomalizika Jumapili.

Kambarage alisema kuwa mikopo inayotolewa ni kwa ajili ya kundi la wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na itaelekezwa katika kwa vikundi vinavyofanya kazi tayari.

Ofisa huyo alisema huu ni wakati mwafaka wa vijana kuchangamkia fursa hiyo na kuongeza nguvu katika kufanya kazi za sanaa na kujiajiri kuliko kutegemea ajira kutoka serikalini.

Mratibu wa tamasha hilo, George Isaac, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuhakikisha wanatoa fursa zaidi kwa vijana wa hapa nchini kuwa katika mazingira bora ya kujikwamua kiuchumi.

Airo alisema umefika wakati changamoto hiyo ikafanyiwa kazi na kubadilisha fikra za vijana na kuwasaidia kujitokeza kufanya biashara kwa lengo la kujiongezea kipato na kupata elimu ya kusaka soko la biashara.

## Gwambina yalia kukosa bahati

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, amesema wachezaji wake walishindwa kutumia vema nafasi walizozitengeneza na kupelekea kupoteza mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Yanga uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Gwambina inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Yanga na kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Novatus aliliambia gazeti hili kuwa Yanga ilipata ushindi huo kwa kutumia uzoefu wa baadhi ya wachezaji wake, lakini timu yake ndiyo ilitawala mchezo huo.

"Sijafurahishwa na matokeo haya, tulipata nafasi nyingi za wazi isipokuwa wachezaji wangu wameshindwa kuzitumia, bahati ikaangukia kwa Yanga," alisema Novatus.

Aliongeza licha ya kuwaheshimu Yanga kutokana na kuwa na wachezaji wazuri, kikosi chake kilijipanga kuwatoa 'vigogo' hao mapema.

Alikiri mchezo huo ulikuwa na ushindani na hali hiyo ilitokana na timu zilizokutana kuwa na uwezo unaofanana licha ya kushiriki ligi tofauti.

# Simba yajiimarisha kufikia malengo

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuingia katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, amesema wachezaji wa timu hiyo wanatakiwa kuendelea kupambana ili kupata matokeo bila kuangalia 'udogo' wa timu wanazokutana nazo.

Simba ilisonga mbele katika michuano ya Kombe na FA kwa ushindi wa penalti 3-2 dhidi ya Stand United baada ya kumaliza dakika 90 kwa sare ya bao 1-1.

Akizungumza na Nipashe, Senzo alisema katika soka kuna mambo matatu, lakini Simba inatakiwa kupambana ili kushinda mechi zake kwa ajili ya kufikia malengo waliyoyaweka msimu huu.

"Najua sio rahisi kupata matokeo mazuri kila mechi, lakini wachezaji wanatakiwa kupambana, hakuna kudharau timu, hakuna timu ndogo kwa sasa, hivyo kila mmoja anahitaji matokeo mazuri," alisema Senzo.

Alisema malengo makubwa ya klabu hiyo ni kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kwa sababu hiyo kila mechi kwao ni sawa na fainali.

"Tunatakiwa tujiimarishe zaidi, mechi zote ni ngumu na kila timu imejiandaa kusaka ushindi, ingawa kuna malengo tofauti, mikakati yetu ni kufanya vizuri kila mechi iliyoko mbele yetu, iwe ligi au kombe la FA," Senzo alisema.

Simba ndio mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatarajia kuendelea tena kesho kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini.

# Michezo

Ijumaa Februari 28, 2020

Nipashe




## Zidane: Madrid ilipoteza utulivu

HABARI UK 30




Nahodha wa Manchester City, Kevin De Bruyne (kulia), akifunga bao kwa penalti katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi usiku huku golikipa wa Real Madrid, Thibaut Courtois akishindwa kuzuia shuti hilo. City ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAPANIA KUIMALIZA KMC

●●● Ni katika mwendelezo wa operesheni yake ya kusaka pointi tatu katika kila mchezo wa Ligi Kuu Bara ulioko ...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi chake kikiwa kimerejea jijini Dar es Salaam salama kutokea Shinyanga, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema akili yake kwa sasa ni kuiimarisha timu yake ili kupata alama tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Taifa.

Hata hivyo Sven amesisitiza mchezo dhidi ya watani zao Yanga utakaochezwa Machi 8, mwaka huu si kipaumbele kwa sasa kwa sababu ana mechi nyingine mbili zinazowakabili kabla ya kukutana na vigogo hao walioko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mbelgiji huyo alisema anafahamu mchezo dhidi ya Yanga ni muhimu, lakini kwake kupata ushindi kwanza dhidi ya KMC ni bora na kupata matokeo chanya dhidi ya Azam FC.

Kocha huyo amesisitiza kuwa akili na mawazo yake ni kuhakikisha pia anapata ushindi katika mechi ya kesho na hiyo ndio sababu ya kutopumzisha kikosi hicho baada ya kurejea jijini.

**"Tuna michezo miwili kabla, kwa sasa akili yetu tunaiangalia KMC, tunajipanga kuhakikisha tunapata matokeo Jumapili, halafu tutacheza dhidi ya Azam, baada ya hapo tutaiangalia Yanga, siwezi kusema zaidi kuhusu mchezo huo," Sven alisema.**

Aliongeza anahitaji wachezaji wake kufikiria mechi hiyo iliyoko mbele yao kwa sababu matokeo ya ushindi yatawasaidia kupata nguvu ya kushinda michezo hiyo miwili itakayofuata ambayo pia ni migumu.

"Hakuna mechi rahisi, kila timu inajipanga na kujiandaa kufanya vema, KMC ni moja ya timu ngumu kwenye ligi, tutapambana kusaka matokeo mazuri, tumejiandaa kukabiliana na changamoto mbalimbali katika mechi hiyo," Sven alisema.

Naye kiungo Hassan Dilunga alisema ili watimize malengo yao, wamejipanga kucheza kwa umakini katika mchezo huo wa Jumapili na hii inatokana na nafasi ambayo wapinzani wao wako kwenye msimamo.

"Tunamshukuru Mungu tulifanya vizuri, tulipambana kwa kiwango kikubwa kwa sababu tulijua mechi ile (dhidi ya Stand United) ni ya mtoano, lakini mechi ya KMC ni ya ligi, pia tutaendelea kujituma ili tusipoteze pointi, hakuna mechi rahisi dunia ya leo," Dilunga alisema.

Baada ya mechi dhidi ya KMC, mabingwa watetezi na vinara hao wa ligi watakutana na Azam FC Machi 4, mwaka huu na mechi hizo ni moja ya michezo inayotabiriwa kuamua ubingwa wa msimu huu.

## Eymael: Yanga kuendeleza dozi

**Na Saada Akida**

TAMBO zimerejea! Baada ya kumaliza gundu la sare na kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema anaendelea 'kukisuka' upya kikosi chake ili kifanye vizuri katika mechi za Ligi Kuu Bara.

Yanga inatarajia kuikaribisha Alliance FC kutoka Mwanza katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Eymael alisema anahitaji kubadili mfumo na hiyo itatokana na mpinzani wanayekutana naye kwa sababu hahitaji kupoteza tena pointi.

"Tunashukuru kwa kuwa tumepata ushindi, wapinzani wetu (Gwambina FC), walikuwa na kasi na walifanya mchezo uwe wa kukimbizana mwanzo hadi mwisho, ila hilo hatujali tumepata matokeo na hilo lilikuwa lengo letu, kwa sasa tunajipanga upya kwa ajili ya mechi ya ligi, ninaendelea kukiimarisha kikosi ili tupate ushindi," alisema Eymael.

Hata hivyo kocha huyo alisema anafanyia kazi upungufu aliioubaini katika kikosi chake na kujipanga kupata ushindi kwenye michezo yao ya ligi inayofuata.

Naye kiungo wa Yanga, Niyonzima alisema ushindi walioupata imerejesha furaha kwa mashabiki na nguvu kwa wachezaji wa timu hiyo.

"Tulikuwa hatuna chaguo la kufanya licha ya wapinzani wetu kupambana kutafuta matokeo, nasi tulikuwa tunahitaji matokeo, hatukuwa na chaguo lingine zaidi ya kupata matokeo ukizingatia tumetoka kupata sare nne mfululizo," alisema Niyonzima.

Mnyarwanda huyo alifunga bao pekee la katika mechi dhidi ya Gwambina FC na kuipeleka Yanga katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake huiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >